Kitabu cha 2
**Hatua za Uamsho Binafsi**

Mafunzo ya Siku 10

# *Kaeni Ndani ya Yesu*

Yesu Kristo:

*"Kaeni ndani Yangu,
Nami ndani yenu."*

HELMUT HAUBEIL

Kitabu cha 2

**Hatua za Uamsho Binafsi**

# *Kaeni Ndani ya Yesu*

Yesu Kristo:

“Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu.”

*Unafanyaje hilo?*

# Maisha Yazaayo Matunda

**Yesu:**

"… akaaye ndani Yangu, Nami ndani yake, huyo HUZAA SANA …" Yohana 15:5

**Nawezaje kukaa ndani ya Yesu?**

Yesu anatualika: Njoni Kwangu! (Mat. 11:28) Yeyote ambaye amekuja kwa Yesu anaalikwa pia kudumu Kwake. (Yohana 15:4) Na hili linafanyikaje?

**"Kaeni ndani Yangu, *Nami ndani yenu*."**
**"Kukaa ndani ya Kristo" humaanisha:**

- **kumpokea Roho Wake daima,**
- **maisha ya kujisalimisha kikamilifu**
- **kwenye huduma Yake."** Desire of Ages 676.2

Maelezo haya hakika yalifumbua macho yangu na kunipatia ubayana kwa ajili ya mwenendo wangu pamoja na Mungu. Kwangu mimi, hii ni siri ya maisha ya Kikristo yenye furaha. (Yohana 15:11) Ni ombi langu na shauku yangu maalum kwamba hii pia itawaonesha wengi njia ya kupata maisha ya furaha na timilifu. Maneno haya ni msingi wa vitabu vitatu katika mfululizo unaoitwa/wa? *Hatua za Uamsho Binafsi.*

**Je kuna uhusiano gani kati ya vitabu vitatu katika mfululizo wa Hatua za Uamsho Binafsi?**

**Na. 1** *Hatua za Uamsho Binafsi* **-Kujazwa Roho Mtakatifu Unawezaje kupata Uzoefu huu?**

**Inahusu kuomba daima na kupokea Roho Wake.**

**Na. 2** *Kaeni Ndani ya Yesu*
**Hii hufanyikaje?**
**Inahusu maisha ya kujitoa kikamilifu kwa Yesu Kristo.**

**Na. 3** *Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho*
Unawezaje kuwa mshirika uliyejazwa Roho?
Inahusu kujitoa kikamilifu kwenye huduma Yake pamoja na matokeo yote mazuri.
(Available Autumn 2019)

**Na 4** *From lack to Abundance:* How to have more of the Holy Spirit? Two insights are at stake here: What is the cause of our lack? How can I live in the wealth and power that God o ers me?

**Neno la Faraja**

Uzoefu umeonesha kwamba usomaji wa kweli hizi za thamani huwa na baraka mahususi, pale ambapo, baada ya usomaji binafsi, ibada ya kila siku pamoja inafanyika kwa wawiliwawili. Kuna baraka maradufu kwa wanandoa! (Kwa wengine inaweza kuwa simu, Skype). Pia, muda wa kila siku ama juma kwa ajili ya majadiliano na maombi katika kikundi huchangamsha sana.

Haki miliki ©2023
Kibidula(Family Development International)
P.O. Box 17 Mafinga
Wachapaji ni Springs of Life, Poland

**ISBN 978-9987-726-22-6**

**www.mwangaza.info**

# Yaliyomo


Sura ya 1

Siku ya Kwanza
Siku ya Pili

**Karama ya Yesu Yenye Thamani Kuu Zaidi**

*Je unafahamu ujumbe madhubuti zaidi alionao Yesu?*
*Ni kazi zipi alizo nazo Roho Mtakatifu?. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6*
*Jinsi gani tabia zetu zinaweza kubadilishwa?*
*Yesu akizungumzia kuhusu Roho Mtakatifu katika Mfano wa Chachu. .18*

Sura ya 2

Siku ya Tatu
Siku ya Nne

**Jitoe kwa Yesu**

*Je ninapoteza utashi wangu?*
*Au nitakuwa imara zaidi?. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .31*
*Nini Kinachoweza Kutuzuia Tusijisalimishe?*
*Hivi kujisalimisha kwa Mungu humaanisha kwamba tunalazimika kuachilia utashi wetu?. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .41*

Sura ya 3

Siku ya Tano
Siku ya Sita

**Yesu Kukaa Ndani Yako**

*Ni matokeo gani ambayo"Kristo ndani Yangu" huwa nayo maishani mwangu?*
*Mafanikio ya Mwisho: kujazwa utimilifu wa Mungu. . . . . . . . . . . . . . . . . . .54*
*Matokeo ya "Kristo ndani Yangu"*
*Jinsi gani tunapata ukombozi dhidi yanguvu ya dhambi?*
*Je tutakuwa tena watu wa "mwilini" kwa kutenda dhambi? . . . . . . . . . 69*

Sura ya 4

Siku ya Saba
Siku ya Nane

**Utii Kupitia Yesu**

*Jinsi gani naweza kuishi katika utii wenye furaha?*
*Furaha ni nini?. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 87*
*Jinsi gani utii kupitia "Yesu ndani yangu" unatenda kazi?*
*Jinsi gani utii kupitia "Yesu ndani yangu" hutenda kazi? Mungu amekusudia: Ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu. . . . . . . . 104*

Sura ya 5

## Imani Yenye Mvuto Kupitia Yesu

Siku ya Tisa

*Jinsi gani umoja unaweza kupatikana miongoni mwa waumini?*
*Nini kinachofanya imani yetu ivutie kwa familia yetu na ulimwengu?* . . . . . 120

Siku ya Kumi

*Mabadiliko gani ndani yetu hutufanya mashahidi?*
*Jinsi gani uamsho huanzisha utume?* . . . . . 132

## Kiambatisho

*Mapendekezo kwa ajili ya kujifunza zaidi* . . . . . 148

Siku ya Kwanza

SURA YA 1

# Karama ya Yesu Yenye Thamani Kuu Zaidi

*Yesu alifundisha nini kuhusu Roho Mtakatifu?*

***Je unafahamu ujumbe madhubuti zaidi alionao Yesu?***
***Ni kazi zipi alizo nazo Roho Mtakatifu?***
***Jinsi gani tabia zetu zinaweza kubadilishwa?***

## Wito Maalum wa Yesu: omba umpate Roho Mtakatifu

Katika ibara moja maalum ya Biblia, Yesu anatuamuru kwa msisitizo tuombe kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Sijui andiko linginelo ambapo Yesu kwa upendo sana anatuhimiza kuzingatia kitu fulani moyoni. Aya hizi zinapatikana katika somo Lake kuhusu maombi katika Luka 11. Mahali hapo alisisitiza mara kumi kwamba tunapaswa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu:

*"Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akimwomba samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (Luka 11:9-13)*

Katika aya hizi chache, Yesu alitumia kitenzi "omba" mara sita; kisha alibadilisha "omba" na kuisisitiza kwa "tafuta" mara mbili—kitenzi —na mara mbili tena kwa "bisha"—pia neno

la kitenzi. Je i  kwa kufanya hivi hatuonyeshi wazi kwamba tunapaswa kuchukua hatua ili kujazwa Roho Mtakatifu?

"Omba" ya mwisho imetumika katika hali endelevu katika Kiyunani. Hii ina maana kwamba hatupaswi kuomba tu mara moja, ila hatuna budi kuendelea kuomba. Hapa Yesu anafanya suala la kuomba siyo tu liwe lenye uharaka, lakini pia kitu fulani anachotarajia tuendelee kukifanya daima. Anataka kumsha shauku yetu juu ya Roho Mtakatifu kwa mwaliko huu wa dhati. Mwaliko huu wa dhati  hutuonesha usadikisho wa Yesu kwamba tutakuwa tunakosa kitu fulani muhimu kama tusipoendelea kuomba kumwagiwa Roho Mtakatifu. Alikuwa akivuta usikivu wetu uelekee kwenye ukweli kwamba tunamhitaji Roho Mtakatifu kabisa. Kwa namna hii, anataka tuendelee kupokea baraka tele za Roho Mtakatifu.

Akifafanua sehemu ya mwisho ya Waefeso 5:18, Johannes Mager anasema: "Mkristo hajazwi kama chombo mara moja kwa ajili ya wakati wote, lakini anapaswa kuendelea kujazwa daima. Hivyo, sentensi katika [Efe. 5:18] inaweza pia kuandikwa hivi. 'Hebu mjazwe Roho upya daima na wakati wote.' Kujazwa Roho Mtakatifu, tunayepewa wakati wa ubatizo, kunaweza kupotezwa endapo karama hii maridhawa tuliyopewa isipodumishwa. Kama imepotezwa, uwepo wa Roho unaweza kupokelewa tena. Lazima ujazo huu ufanywe upya ili Roho Mtakatifu aenee sehemu zote za maisha yetu, na ili maisha yetu ya kiroho yasidhoofike.

"Kujazwa Roho haimaanishi kwamba tuna uwepo Wake zaidi na zaidi kwa wingi, bali kwamba Roho anatumiliki zaidi na zaidi. Kwa hiyo, Paulo anawaamuru waumini wote [katika Efe. 5:18] waendelee daima kujazwa Roho. Hii ni hali ya kawaida kwa Mkristo—ubatizo mmoja lakini kujazwa mara nyingi."[1]

Sehemu hii ya somo la Yesu kuhusu kuomba kupewa Roho Mtakatifu ni mchakato wa kipekee. Roho Mtakatifu ni karama kuu kabisa ya Mungu—karama iletayo karama zingine zote .. Hii ndiyo ilikuwa karama ya thamani ya Yesu kwa wanafunzi Wake na uthibitisho bayana wa upendo Wake.

---

1 Johannes Mager, Auf den Spuren des heiligen Geistes (Lüneburg, Germany, Advent-Verlag, 1999), S. 101.

Karama hiyo ya thamani isingeweza kushurutishwa kwa mtu fulani. Hukirimiwa tu kwa wale wanaoelezea shauku yao ya kupata karama husika na kuithamini. Hivyo nimejizoeza kuomba kila siku kupewa Roho Mtakatifu kwa mujibu wa Yohana 7:37: *"'Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe.'"* Hiyo humaanisha: Bwana mpendwa, nipatie shauku ya Roho Mtakatifu moyoni mwangu.

## Taarifa za kwanza za baadhi ya watu ambao wameanza kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

**Kuurudia "upendo wetu wa kwanza":** Dada mmoja aliniandikia: "Mimi na rafiki yangu hivi sasa tunajisomea kitabu kiitwacho 40 Days kwa mara ya tatu, tukikibadilisha na kitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi. Kabla hatujagundua nyenzo hii, imani, uzoefu, na maisha ya maombi yetu havikuwa vile ambavyo vimebadilika. Tulikuwa na shauku ya kurejesha upya 'upendo wetu wa kwanza.' Tumeupata! Tunamshukuru Mungu kwa mioyo yetu yote. Inastaajabisha sana Mungu wetu mwenye upendo anavyojibu maombi na kwamba anadhihirisha namna Roho Wake atendavyo kazi—ndani yetu na kwa watu tuwaombeao." M. S.

**Yesu aliingia maishani mwetu:** Mtu mwingine aliandika kuhusu vitabu hivi: ". . .vimekuwa baraka kubwa na iliyongojewa muda mrefu maishani mwangu. Kama tu ambavyo washiriki wengine wengi wa kanisa na dada mmoja kanisani mwetu wamepata uzoefu huu, daima kitu fulani kilikuwa kinakosekana katika uzoefu wetu wa imani. Sasa tumepata fursa ya kufahamu jinsi ambavyo Yesu ameingia maishani mwetu na ameanza kutubadilisha. Bado angali akitenda kazi ndani yetu na hatua kwa hatua anatuvuta tuje karibu Naye zaidi." S. K.

## Roho Mtakatifu ni Chanzo cha Maisha Timilifu

Kwa mujibu wa Yesu, kwa nini alikuja duniani hapa? Alisema: "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." (Yohana 10:10) Yesu anataka tufurahie maisha haya

mapya sasa na yaweze kuendelea katika nyanja tofauti kabisa baada ya ujio Wake wa mara ya pili ambayo ni uzima wa milele katika ufalme wa Mungu.

Pia anatuonesha kwamba Chanzo cha maisha timilifu ni Roho Mtakatifu: *"'Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe. Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.' Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho."* (Yohana 7:37-39)

"Mito ya maji yaliyo hai"—hivi huo si ulinganifu mzuri wa maisha timilifu?

Wakati wa maisha Yake duniani, hivi Yesu alitupatia kielelezo linganifu?

Tunajua kwamba Mariamu alichukua mimba ya Yesu kupitia Roho Mtakatifu (Mat. 1:18). Tunajua kwamba baada ya ubatizo Wake aliomba na "Roho Mtakatifu akashuka juu Yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua" (Luka 3:22). Je ilikuwa lazima na muhimu katika mazingira haya kwamba ampokee Roho Mtakatifu kila siku? Ellen White anasema, "Asubuhi kwa asubuhi aliwasiliana na Baba Yake aliye mbinguni, akipokea kutoka Kwake ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu."[2]

Yesu alikuwa kielelezo kwetu katika hili. Tunapaswa kujiuliza: Endapo Yesu kila siku alihitaji burudiko kutoka kwa Roho Mtakatifu, basi hilo ni muhimu mara ngapi kwa ajili yangu na wewe?

Mtume Paulo alifahamu shauku ya Yesu. Katika waraka wake kwa kanisa huko Efeso, Paulo anathibitisha kwamba walikuwa wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu pale walipokuwa waumini (Efe. 1:13). Katika Waefeso 3:16,17 anawahimiza wawe imara katika Roho; katika 4:30 anasema, *"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu";* na katika 5:18, kama mtume aliyepewa mamlaka, anawahimiza Waefeso, pamoja nasi, akisema "mjazwe Roho," au, kwa maneno mengine, "hebu ruhusuni nafsi zenu ziendelee daima na mara kwa mara kujazwa upya Roho."[3] Tunaona kwamba ni uzoefu muhimu wa kila siku kwa ajili ya

2 Ellen G. White, Signs of the Times, November 21, 1895.

3 Pub. Werner E. Lange, Unser größtes Bedürfnis (Lüneburg, 2011), S. 42

maisha ya kiroho na ukuaji wa Mkristo kujazwa kila siku na Roho Mtakatifu.

"Mungu hasemi, Omba mara moja, nawe utapokea. Anatuhimiza tuendelee kuomba. Dumu katika maombi bila kuchoka. Kudumu katika kuomba humleta mwombaji kwenye mtazamo wa dhati zaidi, na humpatia shauku kubwa zaidi katika kupokea mahitaji ayaombeayo."[4]

"Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu humaanisha chini ya mvuto wa Roho Mtakatifu—'kujazwa' kikamilifu na nafsi Yake. Hii siyo uzoefu wa wakati mmoja, bali badala yake ni kitu fulani kinachopaswa kurudiwa daima, kama ambavyo Paulo anabainisha katika Waefeso 5:18 b kwa njeo ya kitenzi cha Kiyunani 'mjazwe.'"[5]

### Maneno ya Yesu ya maagano kuhusu Roho Mtakatifu

Katika maneno ya Yesu ya maagano kwa wanafunzi Wake, alielezea furaha na tumaini kwa kuwaambia kwamba Roho Mtakatifu angewajilia ili kuwa katika nafasi Yake. Aliwasilisha kazi za Roho Mtakatifu katika Yohana 16:7–14 (NKJV):

*"Lakini Mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi Mimi niondoke, kwa maana Mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali Mimi nikienda Zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini Mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu Mimi naenda Zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa. Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza Mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo Yangu na kuwapasha habari."*

4 Ellen G. White, Christ's Object Lessons (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Associa- tion, 2003), uk. 145.3

5 Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Watu Wazima, Julai 17, 2014.

## Ufumbuzi mpya wenye manufaa

Yesu aliwaambia wanafunzi kitu fulani cha kustaajabisha: "Yawafaa ninyi Mimi niondoke." Hii humaanisha kwamba ufumbuzi mpya—kwamba angali pamoja nasi kupitia Roho Mtakatifu—una manufaa zaidi kuliko Yesu kuwepo binafsi. Kwa jinsi hii, hajawekewa mipaka, bali badala yake anaweza kuwa karibu na kila mtu, licha ya mahali alipo sasa.

## Kuongoza kutoka kwenye mashaka na kutoamini hadi kwenye imani katika Yesu

Roho Mtakatifu ana jukumu la kufumbua macho ya ulimwengu. Na hivi ulimwengu haumo kanisani kwa kiasi fulani? Roho Mtakatifu ndiye pekee awezaye kufumbua macho ya Laodikia. Huamsha shauku kwa ajili ya Mungu ndani ya watu waupendao ulimwengu na shauku ya uhusiano wa karibu pamoja na Yesu ndani ya Wakristo vuguvugu. Hutuonesha dhambi ambayo ni chanzo cha dhambi zingine zote: "Kwa sababu hawaniamini Mimi."

Je unamwamini Yesu? Kiini cha imani ni kumtumaini Yesu. Ishara kwamba tumwamini hasa na kumtumaini ni pale tunapojiadhimisha nafsi zetu Kwake kikamilifu. Ni suala la kujiadhimisha kikamilifu, la utayari wetu kumfuata katika kila kitu.

Roho Mtakatifu humtukuza Yesu. Tunapojazwa Roho Mtakatifu, Yesu atakuwa bora zaidi na mwenye thamani kubwa zaidi kwetu. Shukrani kubwa zaidi kwa ajili ya Yesu itajengeka ndani yetu.

## Kuokolewa na kuhesabiwa haki kupitia imani

Roho Mtakatifu hufumbua macho yetu ili yatambue haki ya Yesu. Yesu alipopaa kwenda mbinguni, kafara Yake ilikubaliwa na Baba. Hivyo, kisichowezekana kikawezekana, yaani kwamba Mungu alionesha upendo wakati huohuo alikuwa mwenye haki. Roho Mtakatifu anataka kufumbua macho yetu ili yatambue mbadilishano huu wenye thamani kubwa: Yesu anatwaa hatia yote kutoka kwa wale ambao wamekabidhi

nafsi zao Kwake, Naye huwapatia haki Yake. Hili ndilo fundisho kuu la Biblia: haki kwa imani katika Yesu.

### Roho Mtakatifu hutuonesha mbadala wa Mungu

Roho Mtakatifu pia hufumbua macho yetu ili yatambue ukweli kwamba mfalme wa ulimwengu huu amehukumiwa kabisa. Shetani ametupwa kutoka mbinguni, na hatima yake ya mwisho imekaribia. Tunapokuwa ndani ya Kristo, kimsingi hawezi kutudhuru, hata kama tukirudia kuanguka majaribuni na tukawa dhaifu hapa duniani. Waraka wa Kwanza wa Yohana 5:18 inasema: *"Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala Yule mwovu hamgusi.."* (NIrV) Badiliko la ubwana limefanyika maishani mwetu. Yesu anataka kutuokoa kutoka dhambini na kutulinda dhidi ya mashambulizi ya Shetani.[6]

Kwa upande mwingine, Roho Mtakatifu pia anataka kufumbua macho ya watu yatambue ukweli kwamba hukumu inakuja. Hakuna yeyote awezaye kukwepa hukumu isipokuwa kama ameikubali karama ya wokovu kwa kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu Kristo na kudumu ndani Yake. Siyo kusudi la Mungu kuwafanya watu wamwamini kupitia hofu ya kuwaonesha hukumu. Hata hivyo, utambuzi kwamba hukumu inakuja huweza kuwa kiamshi kwa ajili ya toba kwa watu wengine. Isingekuwa haki kama tungeshindwa kuwaonesha watu chaguzi zinazowakabili katika kile kinachokuja. Hukumu ni kisaidizi cha uamuzi kwetu.

### Roho Mtakatifu hutupatia ufahamu kuhusu kweli

Roho Mtakatifu atatuongoza katika kweli yote. Hutuweka huru dhidi ya fikra za uongo, kutoka kwenye makosa na vishawishi. Pia hutuongoza katika kweli kuhusu sisi wenyewe, ili kwa msaada wa Mungu, tuweze kurekebisha mwelekeo wetu popote unapohitajika.

6 Mada hii muhimu imefafanuliwa katika sura ya 4 ya kitabu cha Dennis Smith kiitwacho, 40 Days: Prayers and Devotions to Revive Your Experience With God, kitabu cha 2 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2011).

“Mfariji anaitwa ‘Roho wa kweli.’ Kazi Yake ni kufasili na kudumisha kweli. Kwanza anakaa moyoni kama Roho wa kweli, na hivyo anakuwa Mfariji. Kuna faraja na amani katika kweli, lakini hakuna amani au faraja halisi inayoweza kupatikana katika uongo.”[7]

### Roho Mtakatifu hufungua ufahamu wetu kuhusu wakati ujao

Roho Mtakatifu pia ana jukumu la kututangazia mambo ya wakati ujao. Yesu Mwenyewe alizungumza bayana kuhusu wakati ujao katika Mathayo 24, na Roho Mtakatifu ana jukumu la kutupatia hata nuru zaidi kuhusu wakati ujao. Tunapompatia nafasi, basi Naye anaweza kutufunulia unabii.

Inashangaza kwamba nyaraka zote saba katika Ufunuo 2 na 3 huhitimisha kwa changamoto ileile kutoka kwa Yesu: *“Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.”* (Ufu. 2:7) Yesu anaelekeza kwetu wito Wake, kanisa la siku za mwisho, kwamba tumsikilize Roho. Je tuko tayari na tunataka kufanya hilo?

### Nguvu kupitia Roho Mtakatifu

Yesu alirejelea kazi ya Roho Mtakatifu katika hotuba Yake ya maagano: “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.” (Matendo 1:8) Jukumu lingine muhimu la Roho Mtakatifu ni kutupatia nguvu na uwezo ili tuweze kuwa mashahidi kwa ajili Yake.

“Kristo ametukirimia Roho Wake kama nguvu ya kiungu ili kushinda mielekeo yote ya uovu ya kurithi na tuliyojijengea, na kuweka chapa ya tabia Yake juu ya kanisa Lake.”[8]

Nguvu kutoka kwa Roho pia ni muhimu kwa afya. Don Mackintosh, mkurungezi wa mafunzo ya uongozi wa uinjilisti wa afya katika Taasisi ya Weimar, anasema:

---

7 Ellen G. White, The Desire of Ages (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), uk. 671.

8 Ibid.

"Tunachohitaji ni taarifa kuhusu afya pamoja na nguvu ya kuitekeleza. Inahusiana na nguvu ya mabadiliko."[9] Hapa inahusiana na nguvu ya injili, kimahususi zaidi, nguvu ya Roho Mtakatifu. Yeye ndiye analeta badiliko. Tunaweza tu kuwaonesha wengine njia endapo tunavuka njia ya kwenda katika afya bora sisi wenyewe. Jambo moja ni hakika: baraka tele za Mungu zinatungojea.

## Kutekeleza vipengele vya uamsho

Kama kanisa tayari tumekuwa tukiombea uamsho kwa muda fulani. Kuombea uamsho ni muhimu, lakini kama asemavyo Mark Finley, ni muhimu pia "kutekeleza kivitendo vipengele vya kibiblia vya uamsho".[10]

Uamsho kanisani hutegemea uamsho kwa kila mtu binafsi. Naweza kukusihi uchukue hatua kwa ajili ya uamsho wako binafsi? Hii hukuongoza katika maisha thabiti na timilifu, kwenye maisha halisi na yenye furaha ya imani.

## Kwa nini moyo mpya ni muhimu?

Yesu aliwaambia wanawali wapumbavu, "siwajui ninyi" (Mat. 25:12). Ndiyo sababu hawakuruhusiwa waingie karamuni. Hao huwakilisha wale wasiokuja kuingia katika ufalme wa Mungu. Sababu ilikuwa kukosa mafuta, ambayo kwetu humaanisha kukosa uzoefu wa Roho Mtakatifu, ukosefu katika maisha ya kiroho ya mtu husika. Maneno "wanawali wapumbavu" hubainisha tabia ya watu wale ambao hawajapata badiliko la dhati la moyo kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu.

Tuna asili ya dhambi. Hivyo, sote ni wabinafsi, nasi tunakabiliwa na asili hii ya ubinafsi. Kwa vile hakuna mbinafsi yeyote atakayeuingia ufalme wa Mungu, badiliko la tabia ni muhimu hasa. Neno la Mungu hutuonesha kwamba kila mtu

9 Dave Fiedler, D'Sozo: Reversing the Worst Evil (Coldwater, MI: Remnant, 2000), "Foreword."

10 Mark Finley, Revive Us Again (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2010), uk. 26.

anaweza kuja kwa Yesu kama alivyo. Lakini tunajua kwamba hakuna yeyote atakayesalia kama alivyo.

Zingatia kwamba wanawali wapumbavu hawamjui Mungu kwa vile hawajayatoa kikamilifu maisha yao kwa Yesu na katika utendaji wa Roho Mtakatifu. "Wokovu wetu hautegemei nini tujuacho, bali nani tumjuaye… (Yohana 17:3). Kile tunachojua ni muhimu, lakini bila uhusiano binafsi unaookoa pamoja na Yesu , tunajaribiwa na mwishowe tunapotea. Ufahamu kuhusu Mungu siyo sawa na kumjua kwa undani na kwa udhati."[11] Hii ndiyo sababu ya msingi kwa nini Yesu anatuhimiza tuendelee kuomba daima tukirimiwe Roho Mtakatifu. Je unaomba kila siku kwa kujisalimisha kikamilifu na kuomba kwa imani kumiminwa kwa Roho Mtakatifu?

11 Dennis Smith, 40 Days, book no. 2, uk. 112.

Kamwe usidharau nguvu ya mtu mmoja katika kusaidia kuanzisha harakati za Roho wa Mungu katika namna yenye nguvu. Huenda Mungu anakuita wewe katika wakati kama huu.

*(Tafadhali soma: Esta 4:14-16)*

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Nini ambacho Yesu anakihimiza moyoni mwako kuhusu Roho Mtakatifu?*

   ______________________________

2. *Jinsi gani Yesu alikuwa kielelezo kwetu katika kuomba Roho Mtakatifu?*

   ______________________________

   ______________________________

3. *Ni kazi zipi mbalimbali alizo nazo Mfariji, ambazo Yesu aliwaahidi wanafunzi Wake na sisi pia?*

   ______________________________

   ______________________________

4. *Nini ambacho Roho Mtakatifu hukitimiza ndani yetu?*

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Mwombee mwanamaombi mwenzio:*
  1. *Kwamba kila siku tutatambua hitaji la kuomba tupewe Roho Mtakatifu na kumpokea kwa imani—na kudai ahadi kwamba Roho Mtakatifu:*
     - *atatuongoza toka kwenye imani dhaifu na kutoamini;*
     - *ataendelea kutubainishia wazi maana ya haki kwa imani;*
     - *atatuweka huru dhidi ya dhana potofu, makosa, na majaribu.*
  2. *Mwombee kujitoa kikamilifu kwa Yesu na huduma Yake.*

Siku ya Pili

# Jinsi gani tabia zetu zinaweza kubadilishwa?

### Yesu akizungumzia kuhusu Roho Mtakatifu katika Mfano wa Chachu

Katika mfano kuhusu chachu, Yesu anazungumzia nguvu ya Roho Mtakatifu ibadilishayo maisha. Unaposoma mfano huu mara ya kwanza, hata hufikirii unaweza kuwa na kitu fulani kinachohusiana na Roho Mtakatifu: "Akasema mara ya pili, Niufananishe na nini ufalme wa Mungu? Umefanana na chachu aliyotwaa mwanamke akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachacha wote pia." (Luka 13:20, 21)

Chachu, au hamira, hutumika katika kuokea aina mbalimbali za mikate. Inapoongezwa kwenye unga, huanza mchakato wa uchachushaji ambao hufanya donge kuwa laini na jepesi zaidi. Kwa namna hii hufanywa kuwa lenye kufurahisha zaidi kwa ladha ya mwanadamu.

Yesu anataka kutubainishia wazi kanuni kadhaa za ufalme wa Mungu kupitia kielelezo hiki. Chachu huwakilisha mchakato wa pekee ajabu ndani yetu, ambao huanza ukiwa mdogo sana lakini baadaye huwa na mwisho wa kushangaza, kama mfano usemavyo: "hata ukachacha wote pia." Yesu anataka kustawisha ndani yetu upendo Wake usio na ubinafsi katika mahali pa ubinafsi wetu.

Katika maana moja ya mfano huu, Yesu anataka kuonesha mvuto wa injili ulimwenguni. Japo injili ilianza ikiwa na mwonekano mdogo, itaenea ulimwengu wote mwishoni. Katika maana nyingine, Yesu anatuonesha jinsi nguvu ya Mungu ibadilishayo maisha inavyotenda kazi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Anasema katika Luka 17:20,21, " Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza, wala hawatasema, 'Tazama, upo huku au kule kwa maana, tazama ufalme wa Mungu umo ndani yenu." (NIV)

Kwa watu wa karne ya kwanza, ufalme wa Mungu ulikuwa ndani yao kupitia nafsi ya Yesu. Leo, ufalme wa Mungu huanza maishani mwetu tunapompokea Yesu kama Mwokozi na Bwana wa maisha yetu. Tunapodumu ndani Yake, Naye ndani yetu, basi wakati wa ujio wa pili wa Yesu ufalme uonekanao utaanza kwa ajili yetu. Hivi sasa, tunahitaji kuona maendeleo ya ufalme wa Mungu Yesu anapokaa ndani yetu. Anaweza tu kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Hapa chini yapo masomo muhimu kutoka kwenye mfano huu.

### Nguvu ibadilishayo hutenda kazi kwa utulivu

"Chachu hutumika kuwakilisha ufalme wa mbinguni. Huonesha nguvu ya neema ya Mungu ihuishayo na kubadilisha."[12] "Badiliko husika linaweza kufanywa tu na Roho Mtakatifu."[13] Hapa inahusiana na nguvu ya ndani inayopenya kila kitu na huweza kutubadilisha kabisa. Kwa namna hii, Mungu anataka kubadilisha tabia zetu ziwe bora zaidi kupitia Roho Mtakatifu.

Biblia inatuambia kwamba kipindi cha kwanza cha kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika nyakati za Biblia wakati fulani kiliambatana na ishara zilizosikika na kuonekana. Lakini badiliko la tabia ndani yetu hutokea kwa utulivu—alimradi tumejazwa Roho Mtakatifu. Halafu ghafla tunagundua kwamba badiliko chanya limefanyika ndani yetu.

Chachu iliyofichika kwenye unga hutenda kazi bila kuonekana ili kulifanya donge zima liwe katika mchakato wa uchachukaji; halikadhalika chachu ya neno la kweli hutenda kazi kwa siri, kimyakimya, kwa uthabiti, ili kuibadilisha nafsi. Mielekeo ya asili hulainishwa na kutiishwa. Mawazo mapya, hisia mpya, makusudi mapya, hupandikizwa. Kiwango kipya cha tabia huwekwa—maisha ya Kristo. Nia hubadilishwa; akili huamshwa katika utendaji kwenye shughuli mpya. Mtu hapewi akili mpya, bali akili alizo nazo hutakaswa. Dhamiri huamshwa.

12 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 96.
13 Ibid., uk. 96, 97.

Tunakirimiwa silika za tabia zinazotuwezesha kumfanyia Mungu huduma."[14]

Kwa nini Mungu anatubadilisha taratibu, na kwa namna isiyotambulika kiasi hicho hadi pale tuonapo matokeo? Muda tulivu unahitajika kwa ajili ya badiliko kama tu ambavyo asili inavyobadilika pale inapoibuka kutoka kwenye msimu wa baridi. Mimea imara kama vile mialoni hukua taratibu sana. Hivi Mungu anatupima kwa namna hii ili kuona kama kweli tuna shauku kwa ajili ya Roho Mtakatifu? Je huipima imani yetu? Nadhani ndivyo. Na anataka kutupatia maisha maridhawa (angalia Yohana 15:1–8; Gal 5:22).

**Nguvu ibadilishayo tabia yetu huja kutokea nje—haimo ndani yetu.**

Kwanza, tunapaswa kutambua: "Mwanadamu hawezi kujibadilisha mwenyewe kwa kutumia utashi wake. Hana uwezo wowote ambao kwao badiliko hili linaweza kufanyika. Chachu—kitu fulani ambacho chote kabisa hutokea nje—lazima iwekwe kwenye unga kabla badiliko hitajika halijafanyika ndani yake."[15] Yesu anatuonesha hapa kwamba tunahitaji nguvu itokeayo nje yetu kwa ajili ya badiliko la tabia.

Hivi hatupaswi kuzingatia maneno ya Yesu kuhusu suala hilo muhimu? "Maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." (Yohana 15:5) "Ili tuweze kuwa na haki ya Kristo, tunahitaji kila siku kubadilishwa na mvuto wa Roho Mtakatifu, kuwa washirika wa asili ya kiungu. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kuinua kipaumbele, kuutakasa moyo, na kuadilisha nafsi yote."[16]

Ushauri huu muhimu kutoka kwa Yesu ni kinyume kabisa na kile ambacho kwa kawaida hufundishwa leo. Ama katika nadharia ya elimu ya ubinadamu (inayohusu binadamu kwanza na mahitaji yake kuliko misingi ya dini) na elimu ya usiri, falsafa ya kibinadamu au baadhi ya maeneo mengine

14 Ibid., uk. 98, 99.

15 Ibid., uk. 96.

16 Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Associa- tion, 2007), uk. 374.

ya ufundishaji, ujumbe ni kwamba nguvu inayotufanya tuendelee iko ndani yetu. Inapaswa tu kuamshwa kwa mbinu hii au ile. Mara nyingi "kujitambua nafsi" huzungumziwa. Mtume Paulo alisema kuhusu yeye mwenyewe, na inahusika kwetu sote: "Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu… halikai neno jema." (Rum. 7:18). Katika hali kama hizi, nini kingekuwa matokeo ya kujitambua nafsi? Tunaweza kusoma kuhusu hilo katika 2 Timotheo 3:1: "Siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari." (NIV). Ubinafsi utatawala. Kwetu sisi siyo suala la kujitambua nafsi, bali badala yake ni kumtambua Kristo. Mtu fulani aliniambia: "Nimeipata hali yangu ya kujitambua nafsi katika Kristo." Jambo kuu ni kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani yetu na kutubadilisha kwa namna chanya.

Peke yetu hatuna uwezo wowote wa kuibadili tabia yetu. Lazima utokee nje. Hiyo ndiyo sababu Yesu kwa uwazi kabisa alielekeza fikra zetu katika Luka 11:9– 13 kuhusu ukweli kwamba tunapaswa kuomba tupewe Roho Mtakatifu—daima. Wakati Yesu akiwa hapa duniani, siku kwa siku alijazwa upya kwa Roho Mtakatifu. Kwetu sisi hata ni muhimu zaidi. Ninapofikiria kile ambacho Mungu anataka kutupatia kila siku kupitia Roho Mtakatifu, basi nafikiri kwamba Mungu wetu wa pekee ajabu anataka kutukumbatia kila asubuhi, kama tu ambavyo wanandoa wanavyokumbatiana kila asubuhi.

Ellen White anasema kuhusu mfano huu: "Mafunzo na elimu yote ambayo ulimwengu unaweza kuwasilisha yatashindwa kumfanya mtoto wa dhambi mpotovu awe mtoto wa mbinguni. Nguvu ifanyayo upya lazima itoke kwa Mungu. Badiliko hilo linaweza kufanywa tu na Roho Mtakatifu. Wote ambao wangependa kuokolewa, wakubwa au wadogo, matajiri au maskini, lazima wajisalimishe chini ya utendaji wa nguvu hii."[17]

Winston Churchill, waziri mkuu katika Himaya ya Uingereza wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, anadhaniwa kwamba alisema: Tumefanikiwa kutawala kila kitu isipokuwa kimoja: watu. Watu hawawezi kubadilishwa kikamilifu kwa mvuto wa mwanadamu. Ili jambo hili litokee, nguvu kutoka nje ya

17 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 96, 97.

ulimwengu huu ni lazima. Inahusu nguvu ya Mungu, ambayo pekee huweza kutenda kazi kifanisi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu.

Neno la Mungu hutuambia kwamba utu wa ndani hufanywa upya siku kwa siku (2 Kor. 4:16). Ni muhimu sana kila siku—kitu cha kwanza kilicho bora asubuhi—kuomba katika imani ili kukirimiwa Roho Mtakatifu.

### Roho Mtakatifu huanza kutenda kazi Yake mioyoni mwetu kisha hutenda kuelekea nje

Somo muhimu linalofuata alilofundisha Yesu katika mfano kuhusu chachu ni kwamba tunapokuwa na matokeo ya uchachuaji wa Roho Mtakatifu, tutaanza kufanya mambo kwa namna tofauti kutoka ndani kwenda nje: "Kama ambavyo chachu, inapochanganywa na unga, hutenda kazi kutoka ndani kwenda nje, ndivyo ilivyo pia kwa ubadilishwaji wa moyo ambao neema ya Mungu hutenda ili kubadilisha maisha. Hakuna badiliko la nje tu litoshalo kutuleta katika upatanifu na Mungu. Wapo wengi wanaojaribu kufanya matengenezo kwa kurekebisha mazoea mabaya haya au yale, nao wanatumaini kwa njia hii kuwa Wakristo, lakini wanaanzia mahali pasipo sahihi. Kazi yetu ya kwanza ni kwenye moyo."

Na zaidi: "Ujuzi wa imani na kuwa na ukweli nafsini ni mambo mawili tofauti. Kuujua tu ukweli hakutoshi. Tunaweza kuwa na hii, lakini mwelekeo wa mawazo yetu pengine ukawa haujabadilishwa. Lazima moyo uongolewe na kutakaswa.

Mtu anayejaribu kushika amri za Mungu kwa hisia ya wajibu tu—kwa sababu anatakiwa kufanya hivyo—kamwe hawezi kuingia katika furaha ya utii. Anakuwa hatii. Maagizo ya Mungu yanapoonekana kama mzigo kwa sababu hupingana na mwelekeo wa mwanadamu, tunaweza kujua kwamba maisha hayo siyo maisha ya Kikristo. Utii wa kweli ni utendaji wa kanuni kuanzia ndani."[18]

Kadiri uamsho unavyoendelea ndani yetu, kile tunachowaza na kutenda na kusema hutokana na kazi ya Roho Mtakatifu.

18 Ibid., uk. 97.

Wengine wataona tofauti kwa jinsi tuishivyo. Ralph Luther anafafanua: "Yesu alikataa kwa dhati kukiri imani ambayo ni mtazamo wa kidini wa ndani tu, unaoacha maisha halisi bila mabadiliko yoyote kwenye mzizi."[19]

Katika The Desire of Ages tunasoma: "Roho Mtakatifu ni pumzi ya maisha ya kiroho nafsini. Kukirimiwa Roho Mtakatifu ni kukirimiwa uhai wa Kristo. Humjaza mpokeaji kwa silika za Kristo. Ni wale tu wanaofundishwa hivyo na Mungu, wale wenye utendaji wa ndani wa Roho, na ambao ndani ya maisha yao maisha ya Kristo hudhihirika, ndio watakaosimama kama watu wawakilishi, ili kuhudumu kwa niaba ya kanisa."[20]

Kwa muhtasari, Yesu alifundisha yafuatayo kuhusu Roho Mtakatifu:

- ► Nguvu ya Roho Mtakatifu ibadilishayo maisha hutenda kazi ndani yetu bila kutambulika. Mara nyingi huwa tunaona matokeo tu.
- ► Nguvu ibadilishayo ndani ya maisha yetu inapaswa kutokea nje yetu.
- ► Nguvu ibadilishayo huanzia mioyoni mwetu na kisha hutenda kazi kwenda nje.

Napendekeza kwa dhati usome sura inayohusu mfano wa chachu katika kitabu kiitwacho Christ's Object Lessons.

### Maneno ya Mwisho ya Yesu: Msikilizeni Roho Mtakatifu

Je unajua ni maneno gani ya mwisho Yesu aliyazungumza akiwa katika utukufu Wake mbinguni kwa kanisa la siku za mwisho? "Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa." (Ufu. 3:22) Yesu anatuita kila mmoja wetu tumsikilize Roho Mtakatifu, na hilo ndilo tunalotaka kufanya.

### Nibadilishe!?

Hivi Yesu anaweza kweli kunibadilisha? Hebu tuufikiri mchoro mzuri kama mfano. Thamani yake haitokani na ubora wa vitu vilivyotumika. Rangi kidogo tu, wakati mwingine

19 Ralph Luther, Neutestamentliches Wörterbuch, S. 71, quoted in O. S. von Bibra, Der Name Jesus (Wuppertal, 1964), S. 98.

20 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 805.

hata ni ya kiwango duni, mkononi mwa bingwa huweza kubadilishwa kuwa mchoro wa thamani. Vilevile, sisi tuna asili ya dhambi, vitu vya "hali duni." Ni muhimu tu kwamba "vitu" hivi vinatengenezwa na msanifu mahiri. Yesu anataka kufanya hili. Na anaweza kulifanya. Anaweza kuniumba mimi na wewe kuwa nafsi inayompatia heshima. Kabidhi nafsi yako kila siku mikononi Mwake na uombe kwa imani ukirimiwe Roho Mtakatifu. Utashangaa kwa kile atakachofanya kwa ajili yako, ndani yako, na kupitia kwako.

Mzee mmoja aliketi kwenye Daraja la Landani (London Bridge) na alikuwa akipiga fidla. Mlikuwepo sarafu chache tu kwenye kofia yake. Mtu mmoja akatembea kumpita lakini baadaye akarejea na kumwambia mtu huyo: "Nipatie fidla yako kwa muda kitambo." Alianza kuipiga kwa namna ya kuvutia sana kiasi kwamba watu wengi zaidi na zaidi wakasimama ili kusikiliza. Hata ilisababisha tafrani barabarani. Jina la mtu huyo ni Niccolò Paganini, mpiga-fidla mashuhuri.

Ni uchaguzi wako endapo unataka kupiga kwanza fidla maishani mwako au unataka kuweka maisha yako mikononi mwa Bwana mahiri.

## Ushuhuda binafsi kutoka kwa mwalimu na mmojawapo wa wanafunzi wake

"Wakati kitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi kilipogawanywa katika kanisa la nyumbani takriban mwaka mmoja uliopita, nilikisoma chote haraka sana. Tayari wakati nakisoma nilikuwa na uzoefu mwingi zaidi pamoja na Mungu kuliko wakati mwingineo uliopita. Hili lilinivutia na kunihamasisha. Katika kiambatisho cha I cha kitabu hiki, nilipata pendekezo lifuatalo: 'Utafiti wa kiufundishaji umeonesha kwamba ni lazima kusoma au kusikiliza mada fulani muhimu mara sita hadi kumi hadi tunapokuwa tumeielewa kikamilifu.' Maneno haya ya hamasa yalivuta mawazo yangu: 'Jaribu hilo angalau mara moja. Matokeo yatakushawishi.'

Nilitaka kupata uzoefu huo, na tayari kufikia kukisoma mara ya tatu kiliniteka nami nikahisi upendo mkuu kwa ajili ya

Mkombozi wangu, jambo ambalo nimelitamani sana maisha yangu yote. Ndani ya miezi miwili nilikuwa nimekisoma mara sita na matokeo yalikuwa yenye manufaa husika. Ni kana kwamba ningeweza kuelewa jinsi ambavyo hali ingekuwa pale Yesu anapokuja karibu nasi na tukaweza kuyatazama macho Yake safi, yenye ukarimu, na yenye upendo. Tangu wakati huo na kuendelea, sikutaka kukaa pasipo furaha hii ndani ya Mwokozi wetu.

Nilipoamka asubuhi, tayari nilikuwa nimetamani muda wangu wa ibada asubuhi ili kwa mara nyingine tena nipate uzoefu wa ushirika pamoja na Mungu, na wakati wa kutwa niliomba kwa utulivu kwamba Roho Mtakatifu aweze kunisaidia mawazo yangu wakati wa mazungumzo na katika mwenendo wangu wakati nikifundisha na kuwasiliana.

Pale mtoto alipotamani kupewa usikivu na kutenda hivyo, Mungu alinipatia nguvu na hekima ya kushughulikia hilo. Tangu wakati huo siku za kazi yangu zimejawa uwepo wa Muumbaji. Kimsingi ananisaidia katika maisha yangu kila siku. Tangu wakati naomba asubuhi na nyakati za kutwa kwa ajili ya kumwagiwa Roho Mtakatifu. Ni kana kwamba mtu yuko karibu sana na mbinguni na tayari ni kana kwamba anaweza kuonja namna itakavyokuwa huko.

Wakati nikisoma kitabu hicho wazo lilinijia kwamba wanafunzi wangu shuleni wanapaswa kushiriki katika uzoefu huu. Nawafundisha watoto wenye umri wa miaka kumi hadi kumi na tano katika shule ya Kiadventista ya Elijah huko Vorarlberg, Austria. Hivyo nilimwomba Mungu anipatie fursa mbalimbali. Muda si mrefu baadaye nilipata mojawapo ya uzoefu wangu wa kipekee ajabu kwa jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kutenda kazi mioyoni mwa vijana wadogo."

### Kijana mtukutu wa miaka 13 na Roho Mtakatifu

"Uzoefu huu ulianza mwaka mmoja kabla sijasoma kitabu kuhusu Roho Mtakatifu. Mwanafunzi mgeni alikuja kwenye shule yetu na ndani ya siku chache kisiwa chetu cha amani kilibadilika kuwa chumba cha ugomvi. Mvulana huyu alikuwa na umri wa miaka kumi na tatu wakati huo. Alikuwa ndiye

mkubwa zaidi miongoni mwa wanafunzi wote na mwenye nguvu zaidi. Mambo mengi yaliyokuwa yamefundishwa wakati wa mwaka wa masomo na kuleta matokeo mema ajabu yalionekana kutoweka ndani ya muda mfupi.

Hebu asimulie kwa maneno yake mwenyewe: 'Nilipokuja katika shule yangu ya sasa, sikujua nini kilichoningojea. Katika siku yangu ya pili shuleni niliruhusu kuchokozwa, hivyo nilijipanga na kuanza ugomvi dhidi ya mmoja wa wanadarasa wenzangu. Nilimpiga japo alikuwa dhaifu kuliko mimi, nikamkaripia na sikutaka kumwona tena kamwe. Baadaye nilitambua kosa langu na kuomba msamaha, kama ambavyo daima nilikuwa nimefanya zamani. Baada ya hapo nilikuwa na mazungumzo na mkuu wa shule. Katika miezi iliyofuata, mchakato fulani ukaanza ndani yangu. Inashangaza kwamba hili halikuwa kamwe limetokea hapo kabla, kwa vile nilikuwa mtoto wa mchungaji! Nilianza kutumia muda mwingi zaidi pamoja na Yesu.'

"Nilidhani mvulana huyu angehitaji uangalizi maalum wa ziada. Alikuwa akitambua makosa yake, aliyajutia, na kujaribu tena, lakini hakuwa na mafanikio ya kudumu katika nguvu yake mwenyewe. Mwanzoni, kwa nadra siku ingepita bila yeye kuwa kwenye ugomvi, lakini taratibu aliendelea vizuri. Baada ya miezi sita, alisema anadhani maombi ndiyo yaliyomleta karibu zaidi na Mungu. Wakati huohuo, alikuwa ameanza kuomba kupewa nguvu asubuhi. Milipuko yake ya ghadhabu na ugomvi wake vikapungua..

Miezi kumi na moja sasa ilikuwa imepita tangu alipokuja shuleni kwetu, na tuliweza kuona mabadiliko zaidi. Hata hivyo, hasira yake, maapizo, milipuko na kupiga ngumi havikuwa vimedhibitiwa kabisa. Lilikuwa jambo la asili—alijaribu kushinda kwa nguvu na ufahamu wake. Wakati mwingine hili lilifanikiwa na wakati mwingine halikufaa kitu. Maombi yetu yalikuwa yamepata mafanikio kiasi, lakini bado mtazamo wake wa akili haukuwa sahihi, pamoja na ukweli kwamba nguvu ibadilishayo ya Roho ilikosekana.

Inafaa nini pale mtu anapoona makosa yake, akajaribu kudhibiti hasira zake, lakini muda kitambo baadaye anashi-

ndwa tena? Wakati hasa nilipotambua kwamba nimefikia mwisho wa werevu wangu, nilipokea kitabu nilichotaja hapo juu. Kilikuja kwa wakati mwafaka hasa. Ndipo nikatambua kile tulichokuwa tunakikosa. Ilikuwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Hata hatukuwa tumemwomba atusaidie!

Kwa vile nilikuwa nimeguswa na ujumbe wa Hatua za Uamsho Binafsi, nilipata ujasiri wa kumuuliza mvulana huyu endapo alikuwa amewahi kuomba akirimiwe Roho Mtakatifu. Hapana, alisema, hakuwa amefanya hivyo kamwe. Ndipo nikajaribu kuamsha shauku yake kuhusu kitabu hiki.

Hata hivyo, sikumpatia. Nilidhani kwamba lazima akihitaji hasa. Na muda si mrefu aliomba kitabu hicho.

Tena, kwa maneno yake mwenyewe: "Mnamo mwezi Novemba 2012 mwalimu wangu alinipatia kitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi. Nilianza kukisoma kwa shauku. Wakati huo sikuwa hata nafahamu kazi ya Roho Mtakatifu."

Ndani ya siku ya kwanza tayari alikuwa amemaliza kusoma takriban sura mbili kisha akaniuliza mara ngapi nilikuwa nimekisoma. Mara akaanza kusoma sura hizo tena na alitaka kufanya vilevile ambavyo kiabu hicho kilipendekeza: kukisoma mara sita hadi kumi.

Tangu wakati huo mengi yamebadilika. Desemba 2012 na kuendelea hayakuwepo tena mapigano ya ngumi wala ugomvi—nilichelea kuliamini hilo. Wavulana aliokuwa amewapiga kila siku wakawa marafiki zake, na wakapatana vizuri. Amebadilika kabisa—ni mpole, na hata yu radhi kusaidia, na hali ya amani imetawala silika yake ya hasira. Wanafunzi wenzake wanaweza kuthibitisha kwamba Mungu alikuwa kazini. Anamruhusu Mungu atende kazi ndani yake. Unaweza kuona matunda kila siku. Kwa utukufu wa Mungu nataka kutaja kwamba mvulana huyu aliamua kubatizwa mnamo mwezi Juni 2013. Kama huyo hakuwa Roho Mtakatifu…

Daima nilikuwa nikidhani kwamba ningeweza kumdhibiti mtoto na kumfanya aone mantiki ya jambo. Subira, uangalifu, na mazungumzo mengi yangefanya hivyo, lakini haikusaidia kwa muda mrefu kwa mvulana huyu. Mungu alipaswa

kuingilia kati na kunifundisha kwamba Roho Mtakatifu ndiye afanikishaye yasiyowezekana. Siku moja mvulana huyu akiwa mbinguni, ndipo nitajua kwamba Mungu alitimiza hilo. Nilipokuwa nimefikia mwisho wa hekima yangu na hatimaye nikaelewa kwamba nisingeweza kumwongoza, ndipo Mungu akaanza kutenda kazi kwa dhati juu yake. Ilinitia hamasa kuona kwamba hakuna hali zinazoshindikana kwa Mungu."—C. P.

***Sala:*** *Baba uliye mbinguni, asante kwa ajili ya karama ya Roho Mtakatifu yenye thamani kuu. Tafadhali nisamehe kwa kumpuuza Roho Mtakatifu. Kuanzia sasa na kuendelea nisaidie ili nimpatie heshima ya juu kabisa. Nakuomba uyainue maisha yangu ya kila siku hadi kiwango kipya. Tafadhali tenda kazi juu yangu ili kila siku niombe kupewa Roho Mtakatifu. Yesu aliomba kila siku kupewa Roho Mtakatifu. Tafadhali nisaidie niufuate mfano Wake.*

Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.

*Wakolosai 4:6*

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Ni mafundisho gani kuhusu huduma za Roho Mtakatifu tuwezayo kujifunza kutoka kwenye mfano wa chachu?*
   a) *Jinsi gani mabadiliko ya tabia yetu hutokea?*

   ---

   b) *Je kauli ya Yesu, "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote" humaanisha nini kwa ajili ya badiliko la tabia zetu?*

   ---

   c) *Tunaelewa nini kuhusu namna Roho Mtakatifu atendavyo kazi kwenye mabadiliko ya tabia zetu?*

   ---

2. *Yesu ni Msanifu, nasi ni michoro Yake. Je somo gani tuwezalo kujifunza kutokana na wazo hili?*

   ---

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*
  1. *Kwamba kwa neema kamilifu ya Mungu tuweze kupata uzoefu wa ukuaji endelevu.*
  2. *Kwamba tutatambua kwamba nguvu ibadilishayo huja kutoka nje na siyo kutoka ndani yetu, hata kama tungekuwa na nia thabiti kiasi gani.*
  3. *Kwamba nguvu ya Roho Mtakatifu iweze kuendelea kuwa bayana maishani mwetu.*
  4. *Kwamba tuweze kutambua dhahiri nguvu ya Mungu ibadilishayo ndani ya watu wengine.*
  5. *Kwamba tuweze kuwasaidia watu pale Mungu anapotaka kututumia kama mkono Wake wa msaada.*

SURA YA 2

# Jitoe kwa Yesu

*Je ninapoteza utashi wangu? Au nitakuwa imara zaidi? Nini kinachoweza kunizuia nisijitoe kwa Yesu? Hivi kujisalimisha kwa Mungu humaanisha kwamba tunalazimika kuachilia utashi wetu?*

Hatuwezi kusisitiza vilivyo ujumbe huu wenye tumaini: tunaokolewa kwa imani (Yohana 3:16; Matendo 16:31, na mengine). Sifa ya msingi ya imani ya Biblia ni tumaini. Yeyote amtumainiye Yesu atajikabidhi Kwake. Hii humaanisha kwamba tunaokolewa kwa sababu tunajikabidhi sisi wenyewe kwa Mungu kupitia Yesu Kristo. Hatua yetu ya kujitoa yenye tumaini ni ishara bayana, ionekanayo ya imani ya kweli.

Kujitoa kikamilifu ni ufunguo wa wokovu, kuzaliwa upya, ushindi dhidi ya dhambi na majaribu, na utimilifu wa Roho Mtakatifu. [21]

“Wale wamwaminio Kristo kama asemavyo katika neno Lake, na kusalimisha nafsi zao chini ya uangalizi Wake, maisha yao ayaongoze Yeye, watapata amani na utulivu. Hakuna lolote la ulimwengu linaloweza kuwahuzunisha Yesu anapowafanya wawe na furaha kwa uwepo Wake. Katika ridhaa kamilifu kuna pumziko kamilifu.”[22] Roho Mtakatifu ni karama adhimu ambayo Yesu aliwapatia wanafunzi Wake. Mungu asingeweza kutukirimia zaidi ya hii. Roho Mtakatifu ni karama iletayo karama zingine zote. “Lakini kama ilivyo kila ahadi nyingineyo, hii pia hutolewaa kwa masharti. Wapo wengi waaminio na kukiri kudai ahadi ya Bwana; wanazungumza kuhusu Kristo na kuhusu Roho Mtakatifu, lakini hawapokei manufaa yoyote.

21 Garrie F. Williams, How to Be Filled With the Holy Spirit and Know It, German version (Lüneburg, 2007), uk. 78.

22 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 331.

Hawasalimishi nafsi iongozwe na kutawaliwa kwa mawakala wa kiungu."[23]

Upokeaji wa karama hii umefungamanishwa kwa masharti. Mara nyingi huwa tunamzungumzia Kristo na Roho Mtakatifu na bado hatupokei baraka. Kwa nini?

Hatujisalimishi kikamilifu Kwake, ili aweze kutuongoza. Wengi hawajajisalimisha nafsi zao kwa Mungu—mara nyingi kwa sababu ya kutojua—lakini badala yake wamejiamulia wenyewe masuala ya maisha yao. Hii inaweza kuwa sababu ya ukosefu wao wa Roho Mtakatifu. "Wote wanaweza kuwa na hakika kwamba uaminifu katika mambo madogo ni ushahidi wa kustahili majukumu makubwa zaidi. . . .

". . . [Isipofanyika wakati huo] hushindwa kupata neema, uwezo, uthabiti wa tabia, ambavyo hupokelewa kupitia kujisalimisha kikamilifu."[24]

Safari yangu ya kujitoaNilikuwa mfanyabiashara, umri wa miaka thelathini, wakati rafiki fulani aliyekuwa mchungaji alipofariki ghafla. Hili liliibua swali akilini mwangu: Nini kingetokea iwapo Mungu angeniita niwe mchungaji? Sikupenda jambo hili kabisa. Kwa juma zima, nilipambana vita vikali. Nilijadiliana na Mungu asubuhi, adhuhuri, na wakati wa jioni. Kila wakati nilimweleza kwa nini sikutaka niwe mchungaji na kile ambacho ningefanya badala yake. Baada ya juma moja, nililazimika kukiri kwamba bila shaka Mungu hakusikikiza mapingamizi yangu. Wakati nikipiga magoti pembeni mwa kitanda changu na sikuwa na hoja zaidi, wazo tulivu lilinijia akilini: "Mungu anakupenda!" Nami nikawaza: Ndiyo, naamini hili.

Baada ya dakika chache, tumaini katika upendo wa Mungu liliniongoza kujitoa kikamilifu kwa Bwana. Baada ya hapo, nilikuwa na amani kubwa. Kwa kweli, Bwana aliniita mwaka mmoja na nusu baadaye ili kuwa mchungaji. Leo bado ningali na shukrani za dhati Kwake. Ulikuwa upendo na hekima isiyokoma vilivyonionesha njia tofauti kabisa kuliko

23 Ibid., uk. 672.
24 Ellen G. White, Prophets and Kings (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), uk. 218, 219.

ile niliyokuwa nayo akilini. Nikitazama nyuma, naona bayana kwamba kujisalimisha huku kuliniletea baraka tele maishani mwangu. Mungu aliniongoza katika njia bora iwezekanayo maishani mwangu.

### Kwa nini kujitoa?

Neno kujitoa/kujisalimisha linafafanuliwa vilivyo katika kitabu kiitwacho Njia Salama: "Mungu ana shauku ya kutuponya, kutuweka huru. Lakini kwa vile hili huhitaji badiliko kamilifu, ubadilishwaji wa asili yetu yote, lazima tusalimishe nafsi zetu kikamilifu Kwake. …

. . . Huweka mbele yetu kimo cha baraka anachotamani kutupitisha kwenye neema Yake. Anatualika tujikabidhi Kwake, ili aweze kutenda mapenzi Yake ndani yetu. Inabaki kuwa wajibu wetu kuchagua endapo tutawekwa huru kutoka kwenye kifungo cha dhambi, ili kushiriki uhuru wa utukufu wa wana wa Mungu."[25] Kujisalimisha kwetu kwa Mungu huleta baraka tele ajabu. Anatualika kujisalimisha nafsi zetu Kwake kwa sababu anataka kutuponya na kutuweka huru. Dhidi ya nini? Kila nafsi inayokataa kujisalimisha kwa Mungu iko chini ya utawala wa mamlaka nyingine. Siyo mali yake mwenyewe. Anaweza kuzungumzia uhuru, lakini lakini yu katika utumwa uliopindukia. Haruhusiwi kuona uzuri wa neno la kweli, maana moyo wake uko chini ya utawala wa Shetani. Ilhali akijikosha kwamba anafuata matakwa ya maamuzi yake, uhalisia ni kwamba anatii utashi wa mkuu wa giza. Kristo alikuja kuvunja vifungo vya utumwa wa dhambi kutoka nafsini. "Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli." "Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu" hutuweka "huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti." (Rum. 8:2)"[26] Sheria ya Roho wa uzima ni nguvu ya Roho Mtakatifu itupatiayo uzima.

. . . Roho huleta uzima na uhuru, tofauti na sheria ya dhambi, ambayo husababisha tu mauti na hukumu."[27]

---

25 Ellen G. White, Steps to Christ (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 1999), uk. 43, 44.

26 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 466.

27 Seventh-day Adventist Bible Commentary, Vol.6, uk. 560 hadi Rum. 8,2

Yesu anaporuhusiwa kuongoza maisha yetu, ndipo anaweza kutuweka huru dhidi ya ukatili wa nafsi yetu (chuki, kinyongo, ugomvi, ulafi, uraibu, hasira, kiburi, majivuno, kufa moyo, kujiona hufai, na kadhalika). "Katika badiliko linalofanyika pale nafsi inapojisalimisha kwa Kristo, kuna hisia kuu kabisa ya uhuru."[28] Kumbuka: kila mwanadamu ni tatizo lake kuu yeye mwenyewe. Wewe ni tatizo lako kuu zaidi. Mungu pekee ndiye awezaye kutuongoza katika uhuru halisi.

Lakini mfinyanzi anaweza tu kufinyanga udongo ulioko mikononi mwake. Ndiyo sababu tunajisalimisha kwa Mungu. Hivi ndivyo namna Mungu anataka kutuweka huru kutoka katika nguvu ya dhambi na kutupatia uongozi na ulinzi wa kiungu.

"Mungu ana shauku ya kutuponya, kutuweka huru. Lakini kwa vile hili linahitaji badiliko kamilifu, uumbwaji upya wa asili yetu yote, lazima tujisalimishe Kwake kikamilifu."[29] "Usalimishwaji wa nguvu zetu zote kwa Mungu hurahisisha kwa kiasi kikubwa sana tatizo la maisha. Hudhoofisha na kufupisha mapambano elfu dhidi ya tamaa za moyo wa asili."[30]

## Biblia inasema nini kuhusu kujitoa?

Warumi 6:13 inasema, "Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi, bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha ya haki." (NIV). Kwa mujibu wa andiko hili, kujitoa humaanisha kuitoa nafsi yako kwa Mungu na kuiweka chini ya mamlaka Yake.

Hanna W. Smith, mwandishi Mkristo, anafafanua kuhusu andiko hili kama ifuatavyo: "Kutoa kitu fulani humaanisha sawa na kukabidhisha kitu fulani, kuweka kitu fulani katika umiliki na utawala wa mwingine. Kutoa nafsi zetu kwa Bwana humaanisha jambo hilohilo. Kufuatia hilo, Bwana ana

28 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 466.
29 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 43.
30 Ellen G. White, My Life Today (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 1999), uk. 6.

uwezo wa utawala na umiliki wetu. Hii humaanisha kujikana wenyewe na kutoa nafsi zetu."[31]

Warumi 12:1 inasema: "Basi, ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana," (NIV). Je ni sababu gani ambayo andiko hili hubainisha kwa ajili ya kutoa maisha yetu kwa Mungu? "Rehema za Mungu." Kujitoa ni jibu letu kwa Mungu wa rehema, Mungu wa upendo.

Kujitoa humaanisha kuweka nafsi zetu kikamilifu mikononi mwa Mungu, kuwepo katika himaya Yake, kumpatia maisha yetu kama dhabihu, siyo kama kafara za Agano la Kale zilizokuwa zikiteketezwa, bali kama dhabihu hai zinazoishi kwa ajili Yake tangu wakati wa kujitoa.

Nitazamapo nyuma katika maisha yangu, naweza kusema kuwa kabla ya kujitoa ilionekana kwangu kwamba kujitoa ilikuwa kafara. Baadaye, nilitambua kwamba haikuwa kafara, bali baraka halisi.

Johannes Mager anafafanua: "Kujitoa, kutelekeza, kujiadhimisha, kuwa chini ya mamlaka ya Mungu kikamilifu—haya ni maneno ya dhati, lakini yainuayo. Kujitoa hakuhusiani kwa vyovyote vile na hisia au hali ya moyo. Humaanisha kumkabidhi nafsi zetu Yule tumpendaye."[32]

Wakorintho wa Pili 5:15 inasema yapi matokeo ya kujitoa: "Tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao. . " (NIRV). Kujitoa humaanisha kuishi kwa ajili ya Yesu.

Kuishi kwa ajili ya Yesu haimaanishi tu kumtumikia wakati wote, bali: "Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa Yeye" (Kol. 3:17, NIV).

Charles T. Studd alisema, "Endapo Yesu Kristo ni Mungu na alikufa kwa ajili yangu, basi hakuna dhabihu iliyo kuu

---

31 Hanna W. Smith, Christsein täglich (To Be a Christian Daily) (Asslar, 1994), uk. 38.

32 Johannes Mager, Unser größtes Bedürfnis (Our Greatest Need) (Lüneburg, 2011), S. 47,

sana kwangu kiasi cha kushindwa kumletea."[33] Mtu huyu alitekeleza alichosema. Alikuwa mwanariadha bora huko Uingereza. Alipokuwa Mkristo, aliachana na kazi yake, akatoa mamilioni yake kwenye jumuia ya kimishenari, kisha akaenda China kama mmishenari, baadaye India, na hatimaye Afrika. Jumuia ya kimishenari aliyoianzisha bado ingali imara yenye wamishenari 1,800 watendao kazi ulimwengu mzima. Alitoa maisha yake kwa Yesu.

### Yesu alijitoa Mwenyewe kwa ajili yetu na kwetu

Ukweli muhimu haupaswi kupuuzwa. Kujitoa siyo suala la upande mmoja. Yesu alijitoa kwetu kwanza. Alitupatia kila kitu ambacho Mungu angeweza kutupatia, Naye anatualika kutoa kila kitu tunachoweza kukabidhi. Ni suala la kila kitu kwa ajili ya kila kitu. Ila tu kuna tofauti kuu kati ya kila kitu atoacho Mungu na kila kitu nitoacho mimi. Hata hivyo, hakuna yeyote awezaye kutoa takriban kila kitu.

- ► Kujitoa hupeleka uhusiano adhimu/mzuri sana pamoja na Yesu na Baba. (Unakaa ndani Yake—Yohana 14:23; Yesu atajidhihirisha kwako— Yohana 14:21.)
- ► Kupitia kujitoa tunafikia hatua ya kuujua ukweli. (Yohana 7:17—Kama nia ya mtu yeyote ni kufanya mapenzi ya Mungu, atajua... ESV)
- ► Kupitia kujitoa tunapata nguvu kuu katika maombi. (1 Yohana 3:22—Lolote tuombalo, tutapokea.)
- ► Kujitoa ni njia ya furaha timilifu. (Yohana 15:11—Furaha yenu itimizwe.)
- ► Kujitoa ni ufunguo wa uzima tele. (Yohana 10:10; Efe. 3:19.)
- ► Kujitoa ni msingi kiasi kwamba Mungu anaweza kutenda kupitia maisha yangu. (Yohana 7:38—mito ya maji hai; Yohana 14:12—kazi kubwa zaidi; Yohana 15:4, 5— matunda tele.)
- ►Shetani amenyimwa fursa ya kuwafikia wale ambao wamejitoa kwa Mungu. (1 Yohana 5:18—yule mwovu

33 Norman B. Grubb, Charles Studd, Kein Opfer zu groß (No Sacrifice Is Too Great), "Introduction."

hawagusi hao, isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Mungu, kama ilivyokuwa kwa Ayubu. Mambo yote hutenda kazi pamoja kwa ajili ya manufaa yao na kamwe hayawi zaidi ya kile tuwezacho kustahimili.)

Viwango vitano vya kujitoaMwandishi mmoja anazungumzia viwango vitano vya kujitoa:

- ► Kutoa fedha ni kiwango cha chini kabisa cha kujitoa.
- ► Halafu kutoa muda.
- ► Kisha huja kutoa uwezo na stadi zetu, huduma yetu.
- ► Baada ya hilo, kutoa hofu na matumaini yetu yote, ambayo ni pamoja na kila kitu kilichotajwa hapo awali.
- ►Kutoa nafsi yetu yote, ambapo humaanisha kutoa kikamilifu utashi na maisha yetu kwa Yesu.[34] Dondoo hii ya mwisho huelezea maana halisi ya kujitoa.

Ni jambo la pekee ajabu tunapotoa nafsi zetu kwa Baba yetu wa mbinguni, kwa sababu tunatumainia upendo Wake hatuachi mambo yaende mrama kama alivyofanya mwanampotevu katika mfano wa Yesu. Alijisalimisha pale alipogonga msingi wa mwamba maishani mwake, na ni wakati huo pekee ndipo alipoamua kurudi nyumbani. Alipokaribia nyumba ya wazazi wake, babaye alitoka kuja kumlaki na kumzungushia mikono yake kwa kumkumbatia. Alimkubali kikamilifu kama mwanawe. Ni wakati huo ndipo mwana huyu alitambua upendo wa babaye. Hii iligeuza utii wake kuwa usalimisho wa upendo.

### Tukio baya sana

Tukio lifuatalo lilitokea huko Ufaransa na husaidia kuonesha hili: Mke wa Mfaransa tajiri alimwambia mtu fulani siri. Alikuwa amebeba chupa ndogo ya sumu mikononi mwake. Alikuwa anapanga kujiua kwa sababu ya matatizo katika ndoa yake. Alisema, “Jana tu nilimlalamikia mume wangu, lakini alijibu kwa mshangao na butwaa: ‘Unataka nini zaidi? Una kitabu changu cha hundi [ikimaanisha alikuwa na pesa zake akizimiliki], unamiliki nyumba yangu, unakula mezani

34 Dean M. Kelley, “How Adventism Can Stop Growing,” Ministry, February 1983, uk. 4.

kwangu. Kila kitu ambacho mali na cheo kinaweza kunipatia ni mali yako, na bado unalalamika?' Nikamwambia," mwanamke huyo akaendelea, "'Nautaka moyo wako, nataka unipende.' Naye akatamka kwa mshangao: 'Huwezi kupata hiyo. Unajua kwamba moyo wangu ni mali ya mwanamke mwingine. Kila kitu ninachomiliki ni chako, lakini moyo wangu, upendo wangu, haiwezekani wewe udai hilo kutoka kwangu.'"[35]

Hakuna yeyote ampendaye mtu fulani angefurahia jibu kama hilo. Mwanamke huyo hakujali kiasi gani mumewe alimiliki. Kilichokuwa na umuhimu kwake ni yeye kama mtu binafsi.

"Bwana wetu mkuu hataki kitu fulani kutoka kwangu. Ananitaka mimi. Yesu hataki sehemu ya muda wangu au sehemu ya mali zangu, wala vipaji au uwezo wangu mbalimbali."[36] Ananitaka mimi, kwa sababu ananipenda na anataka kunifanya niwe na furaha.

Hatuna budi kujitoa wenyewe; tunapaswa kutoa nafsi zetu pamoja na kila kitu tulicho nacho na vyovyote vile tulivyo. Tunapaswa kujitoa wenyewe katika uangalizi, uongozi, mwelekeo, na utashi wa Mungu. Hii ni huduma yetu ya maana ambayo Warumi 12:1 inatuitia.

Neno la Mungu linaposema kuhusu kujitoa kikamilifu, "[Hii] ni huduma yenu yenye maana," basi inaweza tu kuwa na maana kwamba kujitoa kwa Mungu ndilo jambo lenye maana zaidi tupaswalo kufanya. Nini cha maana zaidi kuliko kuweka hali yetu mikononi mwa tabibu bingwa pale tunapokuwa wagonjwa? Nini cha maana zaidi kuliko kukabidhi nafsi zetu kwa kiongozi mwenye uzoefu pale tunapokuwa tumepotea?

Kujitoa kikamilifu siyo hasara, bali faida kuu. Nikilinganishwa na Mungu mimi ni maskini, mpumbavu, na nisiye na msaada. Hivi isingekuwa busara kuikabidhi nafsi yangu mikononi mwa Mungu? Napaswa kumtumaini Yule aliyeniumba, aliyetaka niwepo, anipendaye na awezaye kukidhi mahitaji yangu yote. Kupitia kujitoa kwetu, upendo wa Mungu usio na kikomona

35 Oswald Smith, The Man God Uses (New York: The Christian Alliance Publishing Company, 1925), uk. 26.

36 Johannes Mager, Unser größtes Bedürfnis (Our Greatest Need) (Lüneburg, Werner E. Lange, 2011), S. 48.

nguvu viko upande wetu. Huku ni kuingia kwenye maisha yaongozwayo na Mungu.

Kujitoa kwetu kikamilifu ni mwanzo wa uzima tele (Yohana 10:10) ambao Yesu anataka kutupatia. Na kujitoa huku huleta ushindi dhidi ya uovu, kama Ufunuo 12:11 ithibitishavyo: "Nao wakamshinda [1] kwa damu ya Mwanakondoo, na [2] kwa neno la ushuhuda wao; ambao [3] hawakupenda maisha yao hata kufa." Hii huonesha kwamba kujitoa kikamilifu ni lazima ili kushinda dhambi na Shetani, na kwamba hili ni jambo bora tupaswalo kufanya.

Katika *Christ's Object Lessons*, tunasoma yafuatayo: "Hebu yeyote asiseme, siwezi kurekebisha kasoro zangu za kitabia. Ukifikia uamuzi huu, hakika utashindwa kupata uzima wa milele. Kutowezekana kupo kwenye nia yako mwenyewe. Endapo usipokuwa na nia ya kushinda, basi huwezi kushinda. Ugumu halisi unatokana na upotovu wa moyo ambao haujatakaswa, na kutokuwa radhi kujisalimisha chini ya utawala wa Mungu."[37] "Kwa Yesu, aliyejivua nafsi ya utukufu kwa ajili ya wokovu wa jamii ya wanadamu waliopotea, Roho Mtakatifu alitolewa bila kipimo. Ndivyo atakavyotolewa kwa kila mfuasi wa Kristo pale moyo wote utakaposalimishwa ili aweze kukaa ndani yake."[38]

**Tunaona kwamba:**

- ► Roho Mtakatifu alikaa ndani ya Yesu kwa wingi bila kipimo.
- ► Anatamani tuishi katika hali ya kujitoa kikamilifu ili Roho Mtakatifu aweze kuishi ndani yetu kwa kiwango hicho.
- ► Kwa sababu hii, Yesu alitupatia amri: "Mjazwe Roho." Katika andiko asili la Kiyunani, hii humaanisha: "Hebu ruhusuni nafsi zenu ziendelee daima na mara kwa mara kujazwa upya Roho Mtakatifu" (angalia Efe. 5:18).
- ► Lengo Lake ni kwamba tutakuwa na uzima tele (angalia Yohana 10:10; Kol. 2:10).

---

37 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 331.

38 Ellen G. White, Thoughts From the Mount of Blessing (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Associa- tion, 1999), uk. 20

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Yapi masharti ya kiungu ya kumpokea Roho Mtakatifu?*

2. *Je kujitoa kikamilifu humaanisha nini, na kuna matokeo gani?*

3. *Hivi kujitoa kikamilifu ni ufunguo? Ni baraka ninazoweza kupokea tu kupitia hilo?*

4. *Vipi viwango vitano vya kujitoa? Ni kiwango kimoja tu ambacho ni kujitoa hasa. Ni kipi hicho? Hebu fikiria kuhusu kujitoa kwako.*

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*
  1. *Kwa ajili ya uelewa bora wa nini maana ya kuokolewa kwa imani.*
  2. *Katika kumshukuru Mungu kwa ajili ya baraka za kujisalimisha ambazo tayari umezipata.*
  3. *Kwamba Roho Mtakatifu atakuongoza kwenye njia ya maisha yako na katika maamuzi yote ya maisha yako.*

Siku ya Nne

# Nini Kinachoweza Kutuzuia Tusijisalimishe?

## *Hivi kujisalimisha kwa Mungu humaanisha kwamba tunalazimika kuachilia utashi wetu?*

Kwangu mimi, kikwazo cha kujitoa ilikuwa hofu kuhusu kazi yangu. Kwa usahihi, nilihofu kwamba baada ya kujitoa kwangu, Mungu angeniita kuwa mchungaji.

Edwin Orr alikumbana na vikwazo tofauti. Hii ilikuwa wazi kwake katika ujana wake. Alisema:

Nilipaswa kujitoa kikamilifu kwa Bwana. … Kwa mara ya kwanza maishani mwangu nilitambua kwamba Mungu alikuwa akizungumza nami. Roho Mtakatifu alinena na moyo wangu. Nilimwambia Bwana kwamba nilikuwa radhi kabisa kutoa kila kitu Kwake. Sauti moyoni mwangu ikauliza: "Vipi kuhusu dhambi zako uzipendazo sana?" … Niliziungama na kuahidi kutozirudia tena kamwe. Sauti ndani yangu ikaendelea: "Vipi kuhusu utashi wako?" Hii ilikuja kama mshangao kamili kwangu. … Hivyo, nikamwambia Bwana: Niko tayari kwenda popote unapotaka niende au nibaki nyumbani. … Kisha Roho wa Mungu akazungumza nami kuhusu sanamu niliyoipenda sana maishani mwangu. Alikuwa binti niliyempenda sana. Bwana aliniuliza endapo ningekuwa radhi kumwacha binti huyu kama angetaka nifanye hivyo. Ghafla nikatambua kwamba utashi wangu uliweka kizuizi hapa. Sikutaka kutoa dhabihu ya namna hiyo.

… Katika hatua hii Roho Mtakatifu akaacha kuzungumza nami. Mara moja, moyo wangu ukawa mtupu kiasi cha kutisha. Mara nilitambua hili, kisha tena nikahisi shauku ya kujazwa Roho. Wakati huu nilijitoa kikamilifu kwa Bwana. Nilikuwa tayari kuitoa Kwake hata sehemu hii ya maisha yangu. …

Moyo wangu ulijawa upendo, furaha, na nguvu isiyoelezeka. … Kwa mara ya kwanza maishani mwangu, kwa kweli nilihisi kwamba hakika namjua hasa Mungu na Mwokozi wangu na kwamba Ukristo ulikuwa zaidi ya mafundisho au falsafa.[39]

Mungu alifanikisha mambo mengi kupitia maisha ya Edwin Orr.

Kwa upande wangu, kikwazo kilikuwa kazi yangu, wakati ambapo kwa Edwin Orr, ilikuwa binti. Vyovyote vile iwezavyo kuwa kwako, kama bado hujajitoa kikamilifu kwa Bwana, iweke nafsi yako pamoja na tatizo lako mikononi Mwake. Bwana atakubariki sana.

### Bwana huyaheshimu maamuzi yetu

Endapo ungekuwa unajua mambo yote, ungechagua njia ileile ambayo Mungu anataka kukuongoza kwayo. Tunaweza kutupilia mbali kila hofu na udhuru tunapojitoa kikamilifu kwa Mungu mwenye upendo usio na kikomo.

Kamwe Mungu hatatenda kinyume na utashi huru wa mwanadamu. Mungu wetu wa pekee ajabu anaheshimu hulka zetu. Uhuru ni mojawapo ya karama za thamani sana ambazo Mungu ametupatia. Ndiyo maana Mungu anangojea ukubali wetu na hutenda tu pale tunapomwomba afanye hivyo. Uhuru ni sharti la kiungu. Upendo unaweza tu kujengeka kwenye uhuru.

### Hivi kujitoa kwa Mungu humaanisha kwamba tunapaswa kuachilia utashi wetu?

Je tunapoteza kabisa utashi wetu tunapojitoa kwa Mungu? Hivi tunakuwa vikaragosi halafu Mungu anaongoza kwa kuvuta nyuzi? HAPANA!

Kwa nini siyo? Sababu kwa kujitoa kikamilifu kwa Mungu tunabadilisha utashi wetu mpumbavu, uliopotoshwa, mjinga, na usiokomaa ili kupewa utashi wa Mungu ambao ni kamilifu, mkuu, na wenye busara. Tunajiweka chini ya uongozaji wa kiungu.

39 J. Edwin Orr, Volle Hingabe (Full Surrender) (Kassel, 1965), S. 108ff., imefupishwa.

Hatupaswi kuachilia utashi wetu, lakini badala yake kuachilia matumizi yake mabaya. Utashi unaopaswa kuachiliwa ni ule unaotofautiana na utashi wa Mungu. Ile hali ya kutekeleza ukaidi wetu.

Ellen White aliandika, “Lakini mmoja anasema, ‘Hivi siwezi kuwa na njia yangu, na kutenda mwenyewe?’—Hapana, huwezi kuwa na njia yako halafu ukauingia ufalme wa mbinguni. Hapana ‘njia yangu’ itakuwepo hapo. Hakuna njia za mwanadamu zitakazopata nafasi katika ufalme wa mbinguni. Njia zetu hazina budi kupotelea kwenye njia za Mungu.”[40] (Angalia pia Isa. 53:6.)

Yeyote akataaye kuongozwa na Mungu na Neno Lake, anaishi kwa msingi wa akili yake finyu badala ya kutegemea “mwongozo wa kiungu.” “Pale ambapo utashi wetu utakuwa patanifu na utashi wa Mungu, hubaki bila kuguswa; kwa kweli ingekuwa kosa kuutupilia mbali.”[41]

“Kadiri utashi wa mwanadamu unavyoshirikiana na utashi wa Mungu, huwa na nguvu isiyokuwa na kikomo. Chochote kinachopaswa kufanywa kwa amri Yake, huweza kutekelezwa katika uwezo Wake. Maagizo Yake yote ni wezeshi.”[42]

“Tunapomruhusu Roho Mtakatifu atuongoze, basi hatujafungwa au kuwekewa mipaka. Badala yake, tunaishi katika uhuru mkuu zaidi. Katika 2 Wakorintho 3:17 tunasoma: ‘*…walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.*’”[43]

## Baraka zingine za kujitoa kwetu

Yule atakayejitoa kikamilifu kwa Mungu ataongozwa kwa mkono wa kiungu. Anaweza kuwa mtu wa hali ya chini na asiye na karama bayana; hata hivyo, ikiwa kwa moyo wa upendo na tumaini akitii kila maagizo ya mapenzi ya Mungu, nguvu zake zitanyooshwa, zitaadilishwa, zitaimarishwa, na uwezo wake

40 Ellen G. White, The Review and Herald, Februari 23, 1892.
41 H. W. Smith, Christsein täglich (Being a Christian Daily), S. 73.
42 Ellen G. White, Christian Service (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 1999), uk. 258.
43 David Wolkwitz, Der Weg zu einer kraftvollen Erweckung, (NRW-Vereinigung), S. 25.

utaongezeka. Kadiri anavyothamini masomo ya hekima ya kiungu, utume mtakatifu utakasimishwa kwake; atawezeshwa kuyafanya maisha yake yawe heshima kwa Mungu na baraka kwa ulimwengu. *"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga."* (Zaburi 119:130 NIV).

Wapo wengi leo wasiojua kazi ya Roho Mtakatifu moyoni kama walivyokuwa waumini hao kule Efeso; lakini hakuna ukweli ambao umefundishwa wazi zaidi ya hapo katika neno la Mungu."[44]

### Maisha chini ya uongozi wa kiungu

Hivi Mithali 3:5, 6 inakinzana na jambo hili? Inasema, *"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako"* (NIV).

Wengi hudhani hii humaanisha kwamba wanapaswa kuzimisha akili zao au, kwa kuweka kivingine, kuzimisha nguvu zao za kufikiri. Hakuna lolote liwezalo kuwa kosa zaidi ya hapo. Mungu anataka tutumie fikra zetu. Anatualika tuunganishe fikra zetu pamoja na fikra Yake isiyo na kikomo.

Hivi Mungu hampatii Danieli na marafiki zake, waliokuwa watii kwa mioyo yao yote katika mambo madogo pamoja na mambo makubwa, maarifa makubwa mara kumi zaidi? Mungu anataka tutumie uwezo wote wa akili zetu na wakati huohuo tujiungamanishe na akili Yake isiyo na kikomo.

Ni kama kuendesha gari kwa kifaa ongozi. Napaswa kutumia fikra zangu zote ili kuendesha, lakini hushauriwa sana niiamini GPS kuhusu kupinda, vikomo vya spidi, kutaarifiwa kuhusu msongamano wa magari, njia-michepuko, njia bora ya kufikia ukomo wa safari yangu, au ni muda gani hadi nifike niendako. Nakumbuka vema nilipoazimu ili kujaribu kifaa ongozi wakati nikihitaji kuhudhuria msiba katika eneo lifahamikalo huko Munich. GPS ilifanya kazi yake, nami niliweza kufika mwisho wa safari yangu bila matatizo yoyote.

44 Ellen G. White, The Acts of the Apostles (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), uk. 283, 284.

Mtegemee Mungu, tegemea maagizo Yake, viwango Vyake, mashauri Yake, halafu nenda zako chini ya uongozi wa kiungu.

**Mashaka kuhusu vifaa**

Wakati wa Vita ya Pili ya Dunia, ndege ya Uingereza iliruka kutoka Sisili na kuelekea Afrika Kaskazini. Kwa vile viwanja vyote vya ndege vilikuwa vimezima taa, marubani walipaswa kutegemea vifaa vyao tu. Japo hawakuwa bado wameruka muda uliopangwa, vifaa vilikuwa vikionesha kwamba walikuwa wamefika mwisho wa safari yao. Walidhani hili haliwezekani, hivyo marubani wakaendelea kurusha ndege.

Ni mpaka walipokuwa wamefika mbali juu ya Sahara ndipo wakagundua kosa lao. Waliishiwa mafuta na hivyo walilazimika kushuka kwa dharura jangwani. Kwa vile hawakuwa na maji ya kutosha ndani, watendakazi waliishia kufa kwa kiu. Baadaye, ndege hiyo ilipogundulika, waokoaji walibaini kwamba vifaa vyote vilikuwa vikifanya kazi kwa usahihi. Ndege hiyo ilikuwa ikikata mawimbi kwa kasi na hivyo ikafika kituo chake haraka zaidi kuliko kawaida. Hata hivyo, marubani waliamini maamuzi yao kuliko vifaa vyao, jambo ambalo lilikuwa kosa baya sana kwao. Walifanya uamuzi wao wenyewe, na ulikuwa uamuzi mbaya.[45] Tunaweza kutegemea uongozi wa Mungu. Ni heri kutegemea Neno la Mungu kuliko makisio yetu wenyewe.

**Watu wenye ujasiri**

Kupitia kujitoa kwetu kwa Yesu Kristo, hatuwi dhaifu katika utashi; badala yake tutakuwa watu wenye ujasiri, wanaotetea msimamo wao kwa hekima na upole.

Fikiria tena kuhusu Danieli na marafiki zake. Wakiwa vijana, walithibitisha kwamba walikuwa na ujasiri na walikuwa watiifu kwa Mungu wakati wa jaribu la chakula chao katika Danieli 1. Au fikiria kuhusu uamuzi wao wa kushangaza mbele ya tanuru liwakalo moto, kama iliyoelezewa katika sura ya 3, wakati wakiwa na umri wa kati. Halafu fikiria kuhusu mtazamo wa Danieli akiwa mzee alipokuwa mbele ya tundu la simba, kama ilivyotajwa katika sura ya 6.

45 Aller Diener (Bern, Euro-Africa Division, 1983) II/III, S. 142.

## Thamani au heshimaipatikanayo kupitia Kristo

Yeyote anayejitoa kwa Kristo hana sababu ya kuhofia thamani yake, kwa sababu ana heshima kubwa zaidi kupitia Kristo. Katika kitabu kiitwacho The Ministry of Healing tunasoma: “Wengi wenye sifa ya kufanya kazi bora hutimiza kidogo kwa sababu wanathubutu kidogo. Maelfu hupita katika maisha haya kana kwamba hawana lengo lolote kuu ambalo kwalo wanaishi, kana kwamba hawana kiwango cha kufikia. Sababu mojawapo ya hili ni kiwango cha chini wanachojiwekea. Kristo alilipa gharama kubwa kwa ajili yetu, na kadiri ya gharama hii iliyolipwa anatamani tuthamini nafsi zetu.”[46] Dada mmoja alinieleza ushuhuda baada ya kuwa ameanza kuishi katika Roho Mtakatifu: “Nimepata thamani yangu katika Kristo.”

## Mashauri kwa sababu ya matatizo katika kujitoa

Kijana mmoja alifuata huduma ya ushauri kwa mchungaji, kwa sababu alitaka kujazwa Roho Mtakatifu na alikuwa akipambana na hali hiyo. Mchungaji akamuuliza, “Je umetoa kwa Mungu utashi wako kikamilifu?”

“Siyo kikamilifu, nasikitika.”

“Naam,” mchungaji akajibu, “haifai kitu kuomba kupewa Roho Mtakatifu kabla hujatoa kikamilifu utashi wako kwa Mungu. Hivi hupendi kuutoa kwa Bwana sasa hivi?”

“Siwezi,” kijana huyo akajibu.

“Je uko tayari Mungu akufanyie hilo?” “Ndiyo,” lilikuwa jibu lake.

“Basi, mwombe Bwana sasa.”

Kijana akaomba: “Ee Bwana, niondolee utashi wangu binafsi. Nifikishe hatua ya kujitoa kikamilifu chini ya mapenzi Yako. Nishushie chini utashi wangu. Naomba katika jina la Yesu.”

Kisha mchungaji akamuuliza: “Je imetokea?”

“Lazima imetokea,” alijibu. “Nimemwomba Mungu kitu fulani kadiri ya mapenzi Yake, nami najua kwamba maombi yangu yalisikiwa na kwamba nimepokea kile nilichoomba (1

46 Ellen G. White, The Ministry of Healing (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2003), uk. 498.

Yohana 5:14,15). Ndiyo, imetokea. Utashi wangu unadanganya hapa."[47] Kisha akaomba kupewa Roho Mtakatifu, naye akampokea. Ni jambo la pekee ajabu kwamba Baba yetu mwenye upendo hata yuko tayari kuunda na kuwasilisha masharti ndani yetu pale tumwombapo.

Tunaweza kujifunza mambo mawili kutokana na ombi la kijana huyu. Kwanza, kijana huyu tayari alikuwa anafahamu kuomba kwa ahadi. Katika maombi yake, alitegemea ahadi za Bwana kwamba maombi yanayowasilishwa kadiri ya mapenzi ya Mungu hujibiwa muda uleule yanapotamkwa. Pili, kijana huyu aliamua kukubali msaada wa Mungu katika kuitoa nafsi yake.

## Kuongoza maisha yetu kwa maamuzi

Tunapaswa kujua kwamba uwezo wa kufanya maamuzi ya utashi huru ndiyo mamlaka ongozi maishani mwetu. Nataka kukupatia mfano ili kuelezea vema maana kamili ya uwezo huu. Kumvi ya meli ya abiria iitwayo Queen Elizabeth ina uzito mara 1,300 kuliko usukani wake. Hii humaanisha kwamba usukani una uwezo wa kuendesha shehena ambayo ni mara 1,300 zaidi kuliko yenyewe. Usukani maishani mwetu ni uwezo wetu wa kufanya maamuzi. Kama tukiamua kusalimisha nafsi zetu chini ya mapenzi ya Mungu, basi huweka misaada yote muhimu ndani ya uwezo wetu.

## Changamoto

Katika suala la kusalimisha nafsi zetu kwa Kristo, uamuzi tunaokabiliana nao ni ama kuishi kwa ajili ya nafsi zetu au kuishi kwa ajili ya Mungu. Kila mtu, lakini hususan kijana, anapaswa kujiuliza endapo ubinafsi wake unapaswa kutawala maisha yake au kama anataka kumtumikia Mungu. Mali na starehe za mapenzi zinaweza kuleta ghiliba ya furaha, lakini mambo haya hayaleti ridhaa halisi—wakati wote tunataka zaidi. Kadiri alivyo navyo vingi ndivyo anavyotaka vingine zaidi, malalamiko yake hayakomi, ndivyo isemavyo mithali mashuhuri ya Kijerumani.

47 R. A. Torrey, Der Heilige Geist—Sein Wesen und Wirken (Frankfurt: 1966), S. 151; (The Holy Spirit— His Nature and Ministry).

Mwisho, tunatambua kwamba vitu hivi vimetutawala.

Changamoto nyingine zaidi tunayopaswa kuizingatia ni ukweli kwamba watu wengine wenye kiasi fulani cha mamlaka juu ya maisha yetu, mathalani familia yetu, shule, kanisa, kampuni au jamii, hutegemea mambo kutoka kwetu yanayokinzana na matarajio ya Mungu. Tunaposalimisha maisha yetu kwa Yesu, ndipo tutakuwa na nguvu na ujasiri wa kuyapatia matarajio ya Mungu kipaumbele cha juu zaidi na kuweza kutetea msimamo wetu kwa hekima na upole (Tafadhali soma Danieli 1:8 uamuzi wa Danieli; msaada wa Bwana wa aina mbalimbali katika aya ya 9, 14, 15, 17, 20)

## Je inatosha kusalimisha maisha yangu kwa Mungu mara moja?

Tunaanza na hali ya awali ya kujisalimisha kwa Yesu Kristo wakati wa uongofu wetu. Kujisalimisha huku, ambako hufanyika katika maombi na baada ya mafundisho sahihi ya Biblia na usadikisho, hutiwa muhuri kwa ubatizo na huwa halali milele. Neno la Mungu huliita hili hali ya msingi ya kusalimisha kwa Yesu agano letu pamoja na Mungu. Kujisalimisha kila siku ni jambo tofauti kabisa. Kwa vile mara nyingi inaitwa uwakifishwaji, uongofu, au utakaso, maneno haya yanaweza kusababisha mkanganyiko fulani. Ili kuyapambanua mambo, nitaiita kuwa ni utakaso. Utakaso wa kila siku (au kujisalimisha au uongofu) humaanisha kwamba leo nataka kuishi kwa kufuata agano la msingi ambalo nimefanya pamoja na Mungu; nataka kusimama kwa ajili ya agano hilo leo. Ndiyo sababu ni jambo la thamani sana kuomba kila siku: “Bwana, nasalimisha nafasi yangu Kwako leo pamoja na vyovyote nilivyo na kila kitu nilicho nacho.”

Biblia hufananisha na ndoa agano letu pamoja na Kristo. Kama nikibaki kwenye agano hili, basi sina sababu ya kuhofia kuhusu lolote kabisa. Mungu ana uwezo wa kulinda kila kitu ambacho kimekabidhiwa Kwake. Daima hushika neno Lake. Hawezi kuandika hati ya talaka.

Morris Venden anafafanua, “Ni bayana, kufunga ndoa haina maana kubwa kama hatupangi kudumu kwenye ndoa. Na

huwezi kudumu kwenye ndoa ikiwa kamwe hukuwahi kufunga ndoa kwanza."[48] Ili kudumisha matokeo chanya ya hali yetu ya awali ya kujisalimisha, ni muhimu kukaa katika Yesu. Hii ndiyo sababu Yesu anazungumzia "kukaa" mara tisa katika Yohana 15, pamoja na, mathalani, aya ya 5 na 7. "Akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

Maisha maridhawa huja kwa kukaa ndani ya Yesu. Kupitia kufanya ushirika pamoja Naye, tunaweza kuishi maisha yenye manufaa—maisha ya furaha, nguvu, na ushindi. Mungu anaweza kutenda mambo makuu maishani mwetu. Tunapotawaliwa na ukweli huu, utakuwa wa kimapinduzi maishani mwetu.

**Washa miali:** Nikiwa natokea kwenye msingi wa Ki-adventista, wakati wote nimezamishwa kwenye mambo ya dini. Nikiwa na umri wa miaka 13, niliamua kubatizwa. Hata hivyo, maisha yangu ya kiroho yaliendelea kuwa kinaifu, yachoshayo. Hakuna miali yoyote iliyoangaza ndani yangu. Mungu alinipatia fursa ya kusafiri hadi Marekani kwa mwaka mmoja. Nilienda huko tu kujifunza Kiingereza na kufurahia. lakini jioni moja, Roho Mtakatifu aliniita na kusema, "Mael, hivi una hakika kwamba uko mahali sahihi?" Nilipotoka Marekani, nilitaka kwenda Swideni. Lakini milango yoyote ilikuwa imefungwa. Nikuwa chini kabisa, bila kujua nini cha kufanya maishani mwangu wakati siku moja rafiki wa karibu aliponipatia kitabu cha Helmut Haubeil "Kaeni Ndani ya Yesu". Wakati wa jioni ya kwanza ya usomaji, sikuweza kukoma. Sauti ile mashuhuri ilikuwa imerejea. Jioni baada ya jioni wakati nikisoma, hatimaye miali ikaangaza. Kadiri nilivyozidi kusoma, ndivyo nilivyoelewa zaidi kosa nililokuwa nikitenda—kukosa Roho Mtakatifu! Baada ya kukisoma kitabu hiki mara kadhaa, sikuelewa jinsi badiliko lingetokea. Mungu alijua jibu na bila kulitambua, maneno yangu, mawazo yangu

48 Morris Venden, 95 Theses on Righteousness by Faith (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Associa- tion, 2003), uk. 133.

na mwenendo wangu vilibadilishwa. Yote haya yalikuwa tu kazi ya Roho Mtakatifu aliyeakisiwa ndani yangu. Na hatimaye milango ya hatua ya taaluma ikafunguka huko Ufaransa. Kwangu mimi ilikuwa kazi ya Mungu, ila daima ulisalia ndani mwangu mfadhaiko wa kutoenda Swideni. Mwali ulikuwa bado ungalipo lakini haukung'aa kikamilifu. Helmut Haubeil akaja Dammarie, Parisi. Nilienda huko Ijumaa jioni, Jumamosi asubuhi na jioni…lakini bado halikuwepo jibu. Jinsi gani ya kuwasha upya miali ya moto?

Jumapili asubuhi jibu likafika. Hii ilikuwa siku ya mwisho. Tatizo langu lilikuwa kutojisalimisha kikamilifu chini ya mapenzi ya Mungu. Nilielewa kwamba wito wa Roho Mtakatifu ulikuwa ukifanyika daima, lakini baada ya kuupokea, ilikuwa muhimu pia kujisalimisha Kwake na kuifisha nafsi. Bila kujisalimisha kikamilifu kwa namna hiii, Mungu asingetenda kupitia sisi kama Mathayo 6:33 isemavyo. Nimeelewa tangu wakati huo kwamba kujisalimisha huku ni muhimu sana katika uhusiano wetu pamoja na Mungu. Hadi wakati huo tu ndipo miali inaweza kuangaza. Maël (L. R.)

**Tuombe:**

"**Baba,** tunakushukuru sana kwamba unataka tujisalimishe Kwako ili tuweze kubarikiwa. Tuwezeshe kurahisisha maisha yetu na tuishi katika namna itayokuruhusu kutufanya tuwe viumbe wapya. Tafadhali nisaidie ili kila siku nisalimishe Kwako maisha yangu bila vizuizi vyovyote na kukufuata Wewe katika mambo yote kwa njia ya nguvu Zako. Amina."

**Furaha kupitia Roho Mtakatifu**

"Bwana Yesu hutenda kupitia Roho Mtakatifu; maana ndiye mwakilishi Wake. Kupitia Yeye hupenyeza maisha ya kiroho nafsini… Kamwe moyo wa mwanadamu hautaweza kujua furaha hadi utakapojisalimisha ili uumbwe kwa Roho wa Mungu." Ellen White, RH August 25, 1896, par. 6

## Vijana na Roho Mtakatifu

**Idara ya Vijana kutoka Konferensi**

**Matokeo yalikuwa ya pekee ajabu.** Mimi ni Katibu wa Vijana wa Konferensi ya Queensland Kusini [washiriki 12,200]. Mwanamama mmoja alinipatia kitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi. Maudhui yake yalinistaajabisha. Niliweza kuelezea uzoefu wangu mwingi. Tulibarikiwa sana kwa kitabu hiki kidogo. Tuligawa vitabu 300 kwa viongozi wa vijana kwenye mkutano wa viongozi wa vijana wa konferensi yetu. Matokeo yalikuwa ya kushangaza kabisa. A.v.R. imefupishwa, #138

**Mvulana wa miaka 14 ashinda uraibu**

Mwanangu mwenye umri wa miaka 14 ameanza kuomba kupewa Roho Mtakatifu na amekuwa mvulana tofauti. Ameshinda uraibu wake. Sasa anaishi maisha ya ushindi. Tunamshukuru sana Mungu kwa vile alitumia kitabu hiki kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi katika maisha ya mwanangu. Pastor A., #77

**Matatizo yasuluhishwa – Ubatizo**

Mwanawe wa mwisho alikuwa na matatizo mengi kanisani. Hivyo alimwombea kwa namna maalum wakati wa siku 40 za muda wa maombi akiwa pamoja na mwanamaombi mwenza. Matokeo yalikuwa kwamba mwanawe alibadilishwa maisha yake naye akaanza kujiandaa kwa ajili ya ubatizo. I.G., #16

**Maisha ya kijana mwenye umri wa miaka 18 yabadilishwa**

Mmojawapo miongoni mwa wenyeviti wetu wa konferensi alimpatia mwanawe mwenye umri wa miaka 18 kitabu kidogo.

Hii ilibadili maisha yake. Hivyo, baba yake akagawa nakala za vitabu zaidi ya 200 kwa wanadarasa wa mwanawe katika Shule ya Upili. C.H., #133

**Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja**
Isa. 60:1

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Je ni changamoto gani inayokabili mwaliko wa kiungu wa kusalimisha maisha yangu?*

   ______________________________

2. *Nini kinachoweza kumzuia mtu fulani asijisalimishe? Inaweza kuwa jambo gani kwako?*

   ______________________________

3. *Ni manufaa gani yaliyomo katika maisha yenye uongozi wa kiungu?*

   ______________________________

4. *Ni jambo gani? la muhimu sana katika kudumisha uhusiano wangu pamoja na Kristo kuwa imara na wa karibu?*

   ______________________________

5. *Ni sababu gani ya msingi itawalayo maisha yetu?*

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*
  1. *Kwamba Mungu aweze kuonesha mambo ambayo pengine huzuia kujisalimisha kikamilifu.*
  2. *Kwamba Mungu aweze kutukirimia hekima na nguvu ya kutumia vema utashi wetu na kuupatia kipaumbele sahihi maishani mwetu.*
  3. *Kwamba Mungu aweze kutukirimia utambuzi zaidi na kwamba utashi wetu wenyewe usichukue hatamu.*
  4. *Kwamba Mungu atupatie ushindi dhidi ya majaribu na dhambi.*

Siku ya Tano

SURA YA 3

# Yesu Kukaa Ndani Yako

*Ni matokeo gani ambayo"Kristo ndani Yangu" huwa nayo maishani mwangu? Mafanikio ya Mwisho: kujazwa utimilifu wa Mungu.*

**Dumu ndani ya Kristo**

"Dini humaanisha kukaa kwa Kristo moyoni."[49]

"Ni kupitia Roho ndipo Kristo anakaa ndani yetu; na Roho wa Mungu, akipokelewa moyoni kwa imani, ni mwanzo wa uzima wa milele."[50]

**Zingatia yafuatayo:**

► Kupitia Roho Mtakatifu, Kristo anaishi ndani yetu.
► Tunampokea Roho Mtakatifu kwa imani.
► Huu ni mwanzo wa uzima wa milele.

Ufahamu kwamba Yesu anahitaji kuishi ndani yangu kupitia Roho Mtakatifu, na ndivyo afanyavyo hasa ninapojazwa Roho Mtakatifu, ni wa thamani sana kwangu. Huu ni ukweli adhimu wa Biblia.

Siyo tu kwamba Yesu anataka kuwa na ushirika wa kina pamoja nasi kwa kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, lakini pia anatamani uthabiti na kuimarika kwa uhusiano wetu pamoja na Mungu. Anasema, "Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu" (Yohana 15:4). Huu ni mwaliko adhimu na, wakati

49 Ellen G. White, The Review and Herald, Mei 24, 1892, par. 4.
50 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 388.

huohuo, ni amri. Hii humaanisha kwamba maisha thabiti ya Mkristo yanawezekana kupitia nguvu ya Mungu.

Yesu alisisitiza neno kukaa mara kumi na moja katika Yohana 15:1–17. Anataka tuwe na uhusiano wa kudumu pamoja Naye. Anafungamanisha ahadi bora na za ajabu kwenye wazo hili. "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" (aya ya 7).

"Hayo nimewaambia, ili furaha Yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe" (aya ya 11).

Ellen White anafafanua wito wa Yesu wa "kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu": **"Kukaa ndani ya Kristo humaanisha** [kwanza] **kuendelea daima kumpokea Roho Wake,** [na pili] **maisha ya kujitoa kikamilifu kwenye huduma Yake."**[51] Mahali pengine anasema, "Muunganiko na wakala wa kiungu kila wakati ni muhimu sana kwa maendeleo yetu. Pengine tumewahi kuwa na kipimo cha Roho wa Mungu, lakini kwa maombi na imani tunapaswa kuendelea daima kutafuta ujazo zaidi wa Roho."[52] Na "Yesu ataishi kupitia wao, akiwapatia uvuvio wa Roho Wake atakasaye, akipandikiza nafsini shinikizo hai la nafsi Yake Mwenyewe."[53] Tunaweza kuona sala ya Daudi kama namna ya ahadi kwa ajili yetu: "Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu." (Zab. 51:10)

### Kuteka katika chanzo cha nguvu ya Mungu

Watu wengi hawajui jinsi ya kuteka kwenye chanzo cha nguvu ya Mungu. Wanaishi katika umaskini wa kiroho, japo "uweza Wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa" (2 Pet. 1:3).

Eneo mashuhuri la mafuta katika jimbo la Texas linaitwa Yates Pool. Wakati wa zahama ya kiuchumi Marekani, mtu mmoja aitwaye Yates alikuwa na ranchi ya kondoo. Hakuwa na uwezo wa kujipatia fedha za kutosha kwa ufugaji wa kondoo ili kulipia madeni yake. Ndipo watu kutoka kwenye kampuni ya mafuta wakafika na kumtaarifu kuwa wanadhani

51 Ibid., 676.
52 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Associa- tion, 2012), Oktoba 24 uk. 306.
53 Ibid., Oktoba 23; uk. 305.

wanaweza kupata hazina ya mafuta kwenye shamba lake. Kampuni hiyo ilipendekeza kufanya utoboaji wa majaribio, na hivyo Yates akasaini mkataba.

Takriban kina cha futi 1,200, mchakato wa utoboaji uligundua hazina kubwa ya mafuta. Na yote ilikuwa mali ya Yates! Katika siku aliyokuwa amenunua ardhi hiyo, alikuwa pia amepokea haki ya kumiliki mafuta yoyote au rasilimali zozote ndani yake. Hakuwa ametambua kwamba alikuwa milionea mkubwa aishiye katika umaskini. Tatizo lilikuwa nini? Hakujua kuhusu uwepo wa mafuta hayo.[54]

Je unajua kilichoandikwa katika 2 Petro 1:3, 4? "Kwa kuwa uweza Wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake Mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." Hebu nikwambie sehemu iliyobaki ya andiko hili kwa maneno yangu mwenyewe: kupitia uhusiano wa kina pamoja na Yesu, na ilhali tukiwa kwenye uhusiano huu, tukiomba ilhali tukiwa na "ahadi kubwa mno, za thamani."

Wakati ule ambapo, kwa imani katika Kristo, tunapokuwa watoto wa Mungu, pia tunakuwa warithi, na rasilimali Zake zote ziko himayani mwetu. Kila kitu tunachohitaji ili kuwa wanaume na wanawake wa Mungu na kuwa mashuhuda wenye mafanikio kwa ajili ya Kristo—pamoja na hekima, upendo, na nguvu—viko katika himaya yetu. Hata hivyo, Wakristo wengi wanaishi katika umaskini wa kiroho, sababu hawajui jinsi ya kutumia utajiri wa kiroho ambao tayari Mungu amewakirimia! Kama ilivyokuwa kwa Bw. Yates kabla mafuta hayajagundulika kwenye shamba lake, wanaishi kwa kutojua milki zao zisizokuwa na ukomo.

Na hilo humaanisha nini? "Bila muunganiko huu, hakuna mtu anayeweza kuokolewa. Bila maisha ya Kristo ndani yetu, hatuwezi kuhimili dhoruba za majaribu. Usalama wetu wa

54 Dr. William R. Bright, Erfüllt mit dem Heiligen Geist—Wie erfährt man das? (Neuhausen, 1971), S. 27.

milele hutegemea kujenga kwetu juu ya mwamba imara. Watu wengi leo wanajenga kwenye misingi ambayo haijajaribiwa. Mvua inaponyesha, na tufani kuvuma, na mafuriko yakaja, nyumba yao huanguka, sababu haikukitwa juu ya Mwamba wa milele, jiwe kuu la pembeni Kristo Yesu."[55]

### Omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu

Kuna ujumbe wa pekee katika Biblia ambapo Bwana wetu Yesu anatuhimiza mara kumi tuombe kukirimiwa Roho Mtakatifu. Sijui andiko linginelo ambalo Yesu anaelekeza mawazo kwenye kitu fulani kwa uharaka wa kina kiasi hicho, isipokuwa kwa mwaliko Wake wa kukaa ndani Yake. Andiko hili ni somo juu ya maombi. Andiko linalohusu kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu liko katika Luka 11:9–13. Siyo tu kwamba tunataka kurudia kauli hii muhimu, lakini pia kwa namna mahususi kuzingatia yafuatayo kwenye sura hii: "Na ninyi mmetimilika katika Yeye." (Kol. 2:10)

Ellen White alisema: "Kwa Yesu … Roho Mtakatifu alikirimiwa [kila siku] bila kipimo. Ndivyo atakavyokirimiwa kwa kila mfuasi wa Kristo pale moyo wote utakaposalimishwa ili aweze kukaa ndani yake [na amwombaye Bwana kila siku ili amkirimie Roho Mtakatifu]. Bwana wetu Mwenyewe ameamuru, 'mjazwe Roho (Efe. 5:18), na amri hii pia ni ahadi ya utimizwaji wake. Ilimpendeza Baba kwamba katika Kristo ndipo 'utimilifu wote ukae' na 'katika Yeye ninyi mmetimilika' (Wakolosai 1:19, R.V.; 2:10, R.V.)."[56]

**Hapa tunajifunza:**

- ► Roho Mtakatifu alikaa ndani ya Yesu kwa wingi pasipo kipimo.
- ► Anatamani nasi tuishi katika kujisalimisha kikamilifu ili Roho Mtakatifu aweze kuishi ndani yetu kwa kiwango hicho.
- ► Kwa sababu hii, Yesu Mwenyewe aliamuru: "Mjawe Roho" (Efe. 5:18).

55 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 599, 600.
56 Ellen G. White, Thoughts From the Mount of Blessing, uk. 21.

► Lengo Lake ni kwamba tutapata uzima tele hapa (Yohana 10:10; Kol. 2:10) na uzima wa milele (Yohana 3:16).
► Hivyo, ni lazima kuwa ndani Yake. Yesu akiwa ndani yetu huleta matokeo na manufaa makuu na yenye thamani.

**Kuomba kwa imani**

Tunaomba kwa imani "tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani" (Gal 3:14). "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza" (Ebr. 11:6). "Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani" (Efe. 3:17).

Ni muhimu kujua kwamba baada ya maombi yangu ili kukirimiwa Roho Mtakatifu, tayari nimempokea. Mungu wetu wa pekee ajabu ametuonesha jinsi tunavyoweza kuwa na imani katika Yeye kwa namna rahisi. Ni kupitia kuomba kwa ahadi. (Angalia kitabu kidogo kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi, sura ya 5, "Ufunguo Kwa Uzoefu wa Utendaji," ambapo mada husika hufafanuliwa kwa upana zaidi.)

Ellen White hata anasema, "Roho hungojea kudai na kupokea kwetu."[57]

**David Wolkwitz anaongeza:**

Hivi unaweza kufikiri kuhusu "kudai" kitu fulani kutoka kwa Mungu? Kwa muktadha huu, karama maalum ya Roho Mtakatifu. Wazo la namna hiyo hutufanya tutetemeke kwa hofu. Husikika kana kwamba ni kukosa heshima na hata kufuru hata kufikiri kitu cha jinsi hiyo. Na bado, neno hili hutumiwa na mjumbe wa Mungu katika ibara mbalimbali za maandishi yake. Anamaanisha nini? Kwanza, tunapaswa kutambua kwamba Mungu hufurahia sana kutukirimia tunu hii, sababu anatupenda na tunaihitaji sana. Pili, humaanisha kwamba karama hii ni muhimu sana kwetu. Kwa vile tunaambiwa kwamba karama hii inangojea hatua yetu ya kuidai, basi ni bayana kabisa hutuonesha kwamba tunapotamani uwepo endelevu wa Yesu maishani mwetu ili aweze kutuongoza na kuelekeza, na tukijua kuwa tumejisalimisha kikamilifu kwa

57 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 121.

Mungu, ndipo tunaweza katika tumaini na ujasiri kuwasilisha dai letu. Tunahitaji kufikiri kwa makini kuhusu hili.[58]

Kudai kitu fulani hudokeza shauku thabiti katika kitu hicho unachohitaji au kutaka kuwa nacho hasa; hudokeza umakini kwa upande wa mtu aombaye. Tunapaswa kuweka pembeni vikwazo vyetu vituzuiavyo "kudai" kitu fulani. "Mungu hupendezwa sana tunapoweka madai makubwa kabisa juu Yake, ili yaweze kulitukuza jina Lake."[59]

Kwa kusalimisha nafsi zetu pamoja na moyo wetu wote kwa Yesu kila siku, kwa imani, tunapata karama kuu ya Mungu—Roho Mtakatifu.

## Maombezi Adhimu ya Mtume Paulo

Kwa ajili ya mada hii, tunataka kuangalia katika Waefeso 3:14–21, ambapo tunapata maombezi adhimu ya kutoka kwa Paulo kwa ajili ya kanisa huko Efeso. Muhtasari wake ni kama ifuatavyo:

1. Anaomba kwa ajili ya nguvu ya ndani ya Roho Mtakatifu kwa ajili yao
2. ili kwayo Kristo aweze kukaa mioyoni mwao
3. ili kwamba uweze kupitia uzoefu wa kipimo kamili cha upendo Wake na kwamba upendo huu wa kiungu uweze kupandikizwa na kuimarishwa ndani yao
4. ili waweze kujazwa utimilifu wa Mungu.
5. Hapa tunaona bayana njia ya Mungu kwetu: Kupitia kujazwa Roho Mtakatifu, Kristo anaishi ndani yetu nasi tunapata badiliko chanya la tabia yetu—matunda ya ukuaji katika Roho.

"Kwa hiyo nampigia magoti Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa jina Lake familia yote ya mbinguni na duniani inaitwa, kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, **mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani;** kwamba ninyi ilhali mmekita

58 David Wolkwitz, Der Weg zu einer kraftvollen Erweckung (The Way to a Powerful Revival) (NRW, Abt. Heimatmission), S. 205.

59 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 668.

mizizi na kujenga msingi katika upendo, mweze kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo wake Kristo upitao ufahamu, ili mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu." (Efe. 3:14–19, KJV)

## Ninawezaje kupata nguvu ya ndani?

Msingi wa maisha yetu ya kidini umeoneshwa katika Waefeso 3:16: "Kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake." (KJV)

Tunahitaji nguvu kila siku. Maisha yaliyojaa nguvu hutuletea furaha. Bwana wetu wa pekee ajabu anataka tuwe na nguvu tele maishani mwetu. Nguvu hii kwa ajili ya utu wa ndani hukirimiwa kwa Roho Mtakatifu. Kitabu kidogo kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi, ukurasa wa 60, huonesha kwa nini ni muhimu kuweka wakfu nafsi zetu kila siku kwa Yesu na kuomba kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Na kwa kuomba kwa ahadi tunaweza kuwa na hakika ya kumpokea Roho Mtakatifu mara tu tuombapo. Tena, napendekeza usomaji wa kitabu hiki—ni muhimu sana.

## Kristo ndani yetu

Nini kinachofuata, kwa mujibu wa aya ya 17? "Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani."

Je tunafahamu vilivyo ukweli huu adhimu? Tunapoishi pamoja na Roho Mtakatifu, basi ni ukweli kwamba Yesu anaishi mioyoni mwetu. Hatuwezi kuhisi wala kupima hili. Tunapaswa kuliamini. Kama unaamini jambo hili, basi zungumza Naye tena na tena, na kumwambia: "Asante, Bwana Yesu, kwamba unakaa moyoni mwangu." Au, "Bwana, nina furaha sana kwamba unaishi ndani yangu."

Andrew Murray anasema: "Kwa jinsi hii Yesu hukutwaa kuingia katika ushirika pamoja Naye kwa lengo kwamba maisha Yake yawe sehemu ya maisha yako."[60]

Ellen White anaongeza: "Mvuto wa Roho Mtakatifu ni

---

60 Andrew Murray, Bleibe in Jesus (Remain in Jesus) (Leun, 2012), S. 149.

maisha ya Kristo nafsini."[61] Na "katika mpango wa kumrejeshea mwanadamu sura ya kiungu, ilikusudiwa kwamba Roho Mtakatifu aweze kugusa nia za wanadamu, na kuwa kama uwepo wa Kristo, wakala aumbaye tabia ya mwanadamu."[62] Na pia: "Mkristo mwenye afya ni yule ambaye Kristo amefanyika ndani yake, tumaini la utukufu [Kol. 1:27]."[63]

Andiko hilo linasema kwamba Kristo hukaa mioyoni mwetu **kwa imani**. Tumaini ni msingi wa imani. Ni suala la kukabidhi maisha yetu kwa Yesu—hatua yetu ya msingi ya kusalimisha maisha yetu, halafu, baada ya hapo, kujisalimisha kila siku kwa Yesu Kristo.

### Ni uhusiano gani ulipo kati ya imani na hisia?

Neno la Mungu linasema: *"Kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake,* ***mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake****; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu* ***kwa imani;*** *kwamba, ninyi, ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo."* (Efe. 3:16,17) Tunajazwa Roho Mtakatifu ili Yesu Kristo aweze kukaa mioyoni mwetu, na hili halina budi kufanyika kupitia imani.

Yesu alisema, "***Aniaminiye Mimi***, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake." (Yohana 7:38) Ni muhimu kwamba daima tuzingatie kwa makini jambo hili. Kwa nini? Kiini cha imani ni tumaini. Natumaini kile ambacho Yesu amesema. Alisema kuhusu Baba Yake, "Neno Lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17). Ellen White alisema, "Imani hujipandikiza yenyewe kwenye ahadi za Mungu, na huzidai kama dhamana kwamba afanye vile alivyosema angefanya."[64]

Kumtumaini Mungu humaanisha kutegemea Neno Lake. Nalitumaini Neno la Mungu.

Inakuwaje pale ninapotenda kwa kufuata hisia zangu? Hapo

---

61 Francis D. Nichol, ed., Seventh-day Adventist Bible Commentary, vol. 6 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2001), uk. 1112.

62 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, Februari 8; uk. 47.

63 Ibid., Februari 4; uk. 43.

64 Ellen G. White, The Signs of the Times, May 22, 1884, par. 3.

nitakuwa natumainia kitu fulani nafsini mwangu. Roger J. Morneau, ambaye Mungu alimwokoa kutoka kanisa la Shetani, anafungua macho yetu: "Zile roho za mapepo zingependa kuwahimiza watu wasikilize hisia zao badala ya neno la Kristo na manabii Wake. Hakuna njia nyingineyo ya hakika zaidi ambayo kwayo mapepo wangefanikiwa kutawala maisha ya watu bila wao kutambua kinachotokea."[65] Hatutafuti uzoefu wa kihisia au uzoefu wa kuwa na muunganiko na uungu.

Imani humaanisha kumtumaini Mungu na Neno Lake, kuidumisha Biblia kuwa yenye mamlaka na siyo tu kiambato au kijalizo. Wengi hudai kwamba hatuwezi kulitii Neno la Mungu kwa nguvu zetu wenyewe. Hiyo ni kweli kwa mtu wa mwilini. Lakini yeyote aishiye pamoja na Roho Mtakatifu ana Yesu moyoni mwake na amewezeshwa kulitii Neno la Mungu. Warumi 8:4 inasema: "ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho." (Mengine zaidi kuhusu mada hii katika Sura ya 4: Utii kupitia Yesu)

Kumtumaini Mungu na kupitia uzoefu jinsi ahadi Zake zinavyotimizwa maishani mwetu vitaimarisha imani yetu katika Yeye na kutupatia mizizi ya kina katika upendo Wake. Hatimaye, upendo huu wa Mungu hutosheleza mahitaji ya kina zaidi katika mioyo yetu. Ni kama mtoto mdogo mikononi mwa babaye akipata faraja na usalama. Hisia za mtoto huyo zinaweza kubadilika kwa vile bado hajakomaa. Lakini hisia za mtoto huyo zinapobadilika, hii haibadili upendo wa babaye. Kadiri tunavyoimarika katika upendo wa Mungu, tunatambua kwamba hisia zetu hafifu haziwezi kutupatia hakika yoyote kuhusu uhusiano wetu na Mungu. Hisia zetu hazitumainiki sababu siyo thabiti. Uhakikisho wetu hutokana na tumaini letu katika Mungu na Neno Lake daima.

Hatuhitaji kuchunguza hisia kwa kukata tamaa. Kristo anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo matunda ya Roho yataumbika kwa wingi ndani yetu. Hizi ni tunu za hisia za kina zaidi zitokazo kwa Roho Mtakatifu. Furaha ina sehemu

65 Roger J. Morneau, A Trip Into the Supernatural, (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 1999), uk. 43.

dhahiri hapo. “Furaha ya Bwana ni nguvu zenu.” (Neh. 8:10) Katika maisha ya imani, furaha haitapungua, bali itakuwa imara ndani yetu kupitia maisha yetu pamoja na Mungu.

Baadaye, itakuwa muhimu sana kwetu kutofautisha kati ya uanafunzi kwa kumtumaini Mungu na uanafunzi kwa hisia. Mjaribu mkuu atatuonesha mambo yastaajabishayo, hata yamhusuyo Yesu, lakini nyuma ya ufunuo huu kuna ushawishi kupitia hisia na kuhisi kuwa karibu na uungu. Itaenda mbali kiasi kwamba watu wataonekana kuwa na mivuto adhimu ya “uzoefu wa imani” na kufikia hatua ya kutegemea kikamilifu hisia zao badala ya Neno la Mungu. Hata wanaweza kudhani kwamba hawahitaji Neno la Mungu, kwa vile hujiona kama wanaongozwa na Roho kupitia uzoefu wao wa kihisia. Maneno ya Yesu hupinga bayana jambo hili katika Mathayo 7:21–23: “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina Lako, na kwa jina Lako kutoa pepo, na kwa jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.” Tunaweza tu kusema: Tumaini na kutii, maana hakuna njia nyingineyo ya kuwa na furaha katika Yesu, zaidi ya kutumaini na kutii. (Angalia Testimonies for the Church, vol. 5, sura ya 21, “Kumtazama Yesu.”)

### Kwa nini kuendelea kujitoa kwa Mungu daima na kikamilifu ni muhimu sana?

Katika Warumi 12:1, Mungu anahimiza yafuatayo kupitia mtume Paulo: “Basi, ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. (NIV) Na katika Mithali 23:26 kuna mwaliko: “Mwanangu, nipe moyo wako.”

Maana ya kujitoa imeelezewa kwa kina zaidi katika sura ya 2 “Jitoe kwa Yesu”. Pia imeelezewa vizuri katika kitabu kiitwacho “Njia Salama” katika sura ya 5 “Usahimisho”.

Kujisalimisha kwetu chini ya upendo wa Mungu huleta baraka kuu. Kama Yesu akiruhusiwa kuyaongoza maisha yetu, basi anaweza kutuweka huru dhidi ya udhalimu wa ubinafsi wetu (husuda zetu zote, hasira, mashindano, na kadhalika). Ellen White anasema, "Ukirimiwaji Roho ni ukirimiwaji wa maisha ya Kristo. Humpatia mpokeaji silika za Kristo."[66] "Hatutaweza kupata ushindi kupitia idadi, bali kupitia kusalimisha nafsi kwa Kristo kikamilifu."[67]

## Kufahamu siri iliyofunuliwa

Hebu tuendelee kwenye Waefeso 3:18, sehemu ya kwanza: "Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote." Nini tunachopaswa kutambua? Kile hasa ambacho kimeelezewa na aya iliyotangulia: siri kwamba Kristo anaishi ndani yetu (kupitia Roho Mtakatifu) na kwa jinsi hiyo maisha yetu yanabadilishwa, sababu tumepandikizwa na kuimarishwa katika upendo wa Mungu. Hii humaanisha kwamba Yesu Kristo hukuza tabia Yake ndani yetu.

Ndugu fulani anaandika: "Ukweli kuhusu 'kuwa ndani ya Kristo' na 'Yesu ndani yetu' ni rahisi sana lakini ngumu sana kuutambua kiasi kwamba Wakristo wengi hawajauelewa kikamilifu."[68]

Paulo anasema katika Wakolosai 1:25,26: *"Ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize neno la Mungu. Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake.."* (NIV) **Siri gani?** Aya ya 27 inasema: *"ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa,* ***nao ni Kristo ndani yenu****, tumaini la utukufu.."* (KJV)

Siri iliyofichwa kwa zama nyingi na sasa imedhihirishwa ni kwamba Yesu Mwenyewe anataka kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Andiko husika linasema kwamba hili ndilo

66 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 805.
67 Ellen G. White, Sons and Daughters of God (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2003), uk. 279.
68 Dennis Smith, Spirit Baptism and Abiding in Christ (2010), uk. 12.

tumaini letu la utukufu. Hii humaanisha kwamba utimilifu wa maisha ambayo Mungu anataka tuwe nao kwa ajili ya maisha yetu ya sasa, na wakati huohuo kutukirimia uzima wa milele, umehakikishwa kwa jinsi hiyo.

Ellen White anafafanua kwa upana zaidi kuhusu siri hii, iitwayo "Kristo ndani yenu," tumaini kwa ajili ya utukufu (Wakolosai 1:27), kama ifuatavyo: **"Ufahamu wa siri hii hutupatia ufunguo kwa ajili ya kila moja nyingineyo. Huifungulia nafsi hazina za ulimwengu, uwezekano wa maendeleo yasiyo na kikomo."**[69] Biblia mara nyingi hutumia maneno kama vile "Kristo ndani yako" na istilahi sawia kama vile "katika Kristo," "katika Yeye," "katika Bwana," na "katika mpendwa." Virai hivi vimetumiwa mara 170 katika Agano Jipya. Mfano, maneno haya ni nenokuu katika waraka wa Paulo kwa Waefeso. Hebu fikiria ushuhuda huu: "Wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu" (Gal 2:20). Katika Warumi 15:18, anaandika: *"Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu."*

Maandiko mengine yajulikanayo vyema ni pamoja na: *"Sasa Mungu ashukuriwe, atufanyaye tushangilie daima katika Kristo."* (2 Kor. 2:14, KJV) *"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya."* (2 Kor. 5:17) Msisitizo hapa umewekwa kwenye badiliko la tabia lifanywalo kupitia Roho: *"Tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema."* (Efe. 2:10) *"Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza."* (1 Thes. 4:16) *"Lakini yeye alishikaye neno Lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kwelikweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani Yake."* (1 Yohana 2:5) *"Mungu, kwa kumtuma Mwanawe Mwenyewe… ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi"* (Rum. 8:3, 4). Kama tukiangalia itifaki, tutapata aya zingine za namna hiyo zenye thamani chini ya nenokuu "katika Kristo," "katika mpendwa," "katika Bwana," "katika Yeye" (Kristo).

---

69 Ellen G. White, Education (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), uk. 172

### Aidha "katika Kristo" au "nje ya Kristo"

E. Stanley Jones amesema, "Paulo… hutilia mkazo kwenye kirai 'katika Kristo' na hukitumia mara 97 katika nyaraka zake… Kwa uangalifu mkubwa, alitambua kwamba maneno haya mawili huigawa jamii ya wanadamu katika makundi mawili, 'katika Kristo' na 'nje ya Kristo' … Yule 'aliye katika Kristo' yu 'katika uzima,' na aliye 'nje ya Kristo' yu 'katika mauti.'"[70]

70 E. Stanley Jones, In Christ (London: Hodder and Stoughton, 1961), uk. 9; imefasiriwa upya kutoka Kijerumani

Sasa, basi, hakuna
hukumu ya adhabu juu yao
walio katika Kristo Yesu,
wale wasioenenda kwa
kuufuata mwili, bali kwa
kufuata Roho.

*Warumi 8:1 NKJV*

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Kwa mujibu wa Ellen White, dini ya kweli ni ipi?*

   ---

2. *Nini kilicho muhimu kama kumruhusu Yesu aingie mioyoni mwetu?*

   ---

3. *Je kazi gani ambayo imani yetu au tumaini katika Mungu hufanya kuhusiana na kumpokea Roho Mtakatifu?*

   ---

4. *Kwa nini ni muhimu kwamba uhusiano wetu pamoja na Yesu ujengwe kwenye tumaini katika Yeye na Neno Lake na wala siyo hisia zetu?*

   ---

5. *Kristo anapokaa ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo tabia Yake hujengeka ndani yetu, ambayo ni tunda la Roho. Je hii ina maana gani kwa ajili ya maisha yako?*

   ---

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*
  1. *Kwa ajili ya ufahamu na kudumisha dini ya kweli—ili Yesu aishi kwa imani mioyoni mwetu.*
  2. *Kwa ajili ya uthabiti katika kusalimisha mioyoni kwa Yesu.*
  3. *Kwa ajili ya uzoefu wa kina zaidi katika uwepo wa Roho Mtakatifu maishani mwetu.*
  4. *Kwa ajili ya uwekaji sahihi wa vipaumbele wa hisia zetu na jinsi ya kushughulika nazo.*
  5. *Kwa ajili ya furaha ikuayo daima na ionekanayo zaidi—furaha aletayo Kristo.*

Siku ya Sita

# Matokeo ya "Kristo ndani Yangu"

## *Jinsi gani tunapata ukombozi dhidi ya nguvu ya dhambi? Je tutakuwa tena watu wa "mwilini" kwa kutenda dhambi?*

### Ellen White kuhusu "Kristo ndani yako"

"Watu wa Mungu wanapokuwa wamoja katika umoja wa Roho, Ufarisayo wote, hali yote ya kujihesabia haki, iliyokuwa dhambi ya taifa la Kiyahudi, itatoweshwa kutoka mioyoni. … Mungu ataweka wazi siri iliyokuwa imesitirika kwa vizazi vyote. Anaweka bayana jinsi ulivyo 'utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu' (Kol. 1:27)."[71]

### Yusufu, Danieli na wenzake

"Unapaswa kujiandaa kufuata mfano wa vijana hawa waadilifu. Kamwe usiogope rangi zako; zivae, zikunjue zitazamwe na wanadamu pamoja na malaika. Usitawaliwe na adabu bandia, wala busara duni inayokupendekezea mwelekeo wa matendo kinyume na ushauri huu. Kwa uchaguzi wako wa maneno na mwelekeo thabiti wa matendo, kwa utaratibu wako, kwa utauwa, fanya maungamo thabiti ya imani yako, kusudia kwamba Kristo atatawala katika enzi ya hekalu la nafsi; kisha weka talanta zako miguuni Pake bila kizuizi ili ziweze kutumiwa katika huduma Yake."[72]

### Maisha ya Familia

**Kristo Katika Kila Moyo Ataleta Umoja**—"Iwapo mapenzi ya Mungu yakitimizwa, mume na mke wataheshimiana na

71 Ellen G. White, Selected Messages, book 1, uk. 386.
72 Ellen G. White, Messages to Young People (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2003), uk. 28.

kukuza upendo na ujasiri. Chochote ambacho kingeharibu amani na umoja wa familia kinapaswa kudhibitiwa kwa dhati, na ukarimu na upendo vinapaswa kudumishwa. Yule anayeonesha roho ya huruma, ustahimilivu, na upendo atagundua kuwa roho hiyohiyo itaakisiwa kwake. Mahali ambapo Roho wa Mungu anatawala, hayatakuwepo mazungumzo yoyote ya kutofaa kwa mahusiano ya ndoa. Endapo Kristo hakika akifanyika ndani, tumaini la utukufu, utakuwepo umoja na upendo nyumbani. Kristo akaaye moyoni mwa mke atakuwa katika upatanifu na Kristo akaaye moyoni mwa mume. Watakuwa wakipambana pamoja kwa ajili ya makao ambayo Kristo ameenda kuwaandalia wale wampendao."[73]

"Unataka nyumba yako iwe kama ile ya Ibrahimu. Aliongoza nyumba yake ifuate maelekezo yake. Aliwafundisha kutii amri za Mungu. Haya ni masomo, akina mama, mnayopaswa kuwafundisha watoto wenu kwa subira. Hampaswi kudiriki kutumia muda mkijifunza fasheni za wakati. Wafundisheni kwamba wao ni mali ya Kristo. Tunajenga tabia leo. Vijana wa kiume na wa kike, mnaamua leo hali yenu katika wakati ujao. Mruhusuni Kristo aingie ndani. Atawalinda dhidi ya majaribu."[74]

## Kushinda

*"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."* (2 Wakorintho 5:17) Kupitia nguvu ya Kristo, wanaume na wanawake wamekata minyororo ya mazoea ya dhambi. Wamekana ubinafsi. Mtukanaji amekuwa mstahivu, mlevi amejitawala, mpotovu amekuwa safi. Roho ambazo zilikuwa zimebeba mfanano wa Shetani zimebadilishwa katika sura ya Mungu. Badiliko hili kwa lenyewe ni muujiza wa miujiza. Badiliko lililofanywa na Neno, ni mojawapo ya siri za kina zaidi katika Neno. Hatuwezi kulielewa; tunaweza tu kuliamini,

73 Ellen G. White, The Adventist Home (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2002), uk. 120.

74 Ellen G. White, Temperance (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2004), uk. 290, 291.

kama ilivyobainishwa kwenye Maandiko, ni *'Kristo ndani yako, tumaini la utukufu.'* [Kol. 1:27]."[75]

### Nyaraka/Barua za Yesu

"Katika kila mmoja miongoni mwa watoto Wake, Yesu anatuma barua kwenda ulimwenguni. Endapo wewe ni mfuasi wa Kristo, anatuma ndani yako barua kwa familia, kijiji, mtaa, mahali unakoishi. Yesu, akaaye ndani yako, anatamani kusemesha mioyo ya wale wasiomfahamu. Pengine hawaisomi Biblia, au hawaisikii sauti iwasemeshayo katika kurasa zake; hawaoni upendo wa Mungu kupitia kazi Zake. Lakini kama wewe ni mwakilishi halisi wa Yesu, pengine kupitia kwako wataongozwa kufahamu kitu fulani kuhusu wema wake na kuongolewa wampende na kumtumikia."[76]

### Upande binafsi wa upendo wa Mungu

Kupitia uhusiano huu wa karibu, ambao Kristo anahitaji kuuanzisha pamoja nasi kupitia Roho Mtakatifu, anatuonesha kwa namna ya pekee upande binafsi wa upendo mkuu wa Mungu. Ni jambo lisiloeleweka kwamba Kristo anaishi ndani yangu. Lakini Neno Lake linatuhakikishia juu ya hili, ambalo hulifanya liwe kweli.

Baba mmoja alikuwa katika safari nchi za ng'ambo akiwa pamoja na mwanawe na alitaka kuuelezea upendo wa Mungu. Baba huyo akasema, "Angalia juu ya guberi ya meli hii, na sasa shetri—huu ndio urefu wa upendo wa Mungu. Na sasa angalia kushoto na kulia—huu ni upana wa upendo wa Mungu. Sasa angalia juu angani—hicho ni kimo cha upendo wa Mungu. Sasa angalia juu ya maji. Bahari ina kina kirefu zaidi chini yetu. Hicho ni kina cha upendo wa Mungu." Kijana huyo akatafakari kwa muda kuhusu maelezo haya kisha akatahamaki uso ukimng'aa: "Baba, hivi unajua sehemu muhimu ya jambo hili ni nini? Tuko katikati yake."

Kila mmoja ambaye kila siku huyaweka wakfu maisha yake kwa Kristo na kujazwa Roho Mtakatifu yuko katikati ya upendo

75 Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 476.
76 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 115.

wa Mungu. Hakuna mahali bora zaidi ya hapo tuwezapo kuishi. Naomba kila siku kwamba Baba yetu wa pekee ajabu atanidumisha mahali hapa.

**Mafanikio ya juu kabisa: uzima tele**

Katika Waefeso 3:19, Paulo anataka tuuelewe upendo wa Yesu kwa ajili yetu, na kwamba kupitia upendo huu tunajazwa utimilifu wa Mungu. Aya hii inasema: *“Na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.”*

Je tunaweza kuona nini kinachotegemea Kristo kuishi ndani yetu? Ni njia pekee ya kufikia utimilifu wa Mungu. Katika Yohana 10:10, Kristo anasema kwamba alikuja ili tuweze kuwa na uzima tele. Wakolosai 2:9, 10 anasema, *“Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye.”* Je unao utimilifu wa Mungu? Mungu anataka kukupatia karama hiyo. Chukua hatua stahiki!

**Majibu zaidi ya maombi yetu**

Tunaweza kuomba kwamba Bwana ajibu maombi yetu kadiri ya ahadi Yake katika Waefeso 3:20: *“Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.”* Tunaweza kuomba, tukidai ahadi hii, kwamba Bwana wetu wa pekee ajabu siyo tu anajibu maombi yetu kama ambavyo tumesihi, lakini kupita hitaji letu, fahamu zetu, hubariki sana kadiri ya utajiri Wake wa utukufu na uweza. Pamoja na hilo, tunaweza kuomba kulingana na Yeremia 33:3 kwamba Mungu anajibu maombi yetu na kutudhihirishia mambo makuu na adhimu: *“Niite, Nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.”* (NIV)

**Je maisha ya Yesu yana matokeo gani ndani yangu?**

*“Bali kwa Yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi.”* (1 Kor. 1:30) Kristo amefanywa kuwa hekima yetu. Tunaweza kutenda kwa hekima Kristo akiwa ndani yetu. “Maana hekima ni bora kuliko marijani; wala vyote

vinavyotamanika havilingani nayo." (Mithali 8:11) *"Ndipo nilipoona ya kuwa kweli hekima hupita upumbavu, kwa kadiri nuru ipitavyo giza."* (Mhubiri 2:13) Bila kuwa ndani ya Kristo, tunaweza kuwa na akili sana, lakini wakati huohuo tukawa wapumbavu. Hebu tuwakumbuke Adamu na Hawa. Walikuwa na uwezo wa juu wa kiakili lakini walitenda kipumbavu pale walipojiamulia kufuata makusudi ya nafsi zao badala ya kumtumaini Mungu. Kuwa kwangu 'ndani ya Kristo' huamua endapo nina akili na busara. *"Hekima ni nguvu zake mwenye hekima , zaidi ya wakuu kumi waliomo mjini."* (Mhubiri 7:19, NIV)

Kristo amefanywa kuwa haki yetu. Hii humaanisha kwamba haki iliyopotezwa wakati wa anguko la jamii ya wanadamu inaweza kurejeshwa kupitia Yeye. Andiko la thamani ni Warumi 8:3, 4: *"Mungu, kwa kumtuma Mwanawe Mwenyewe… aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho."* Tafadhali zingatia kwamba andiko hilo linasema kwamba haki hutimizwa kupitia Yesu ndani ya wale wanaoenenda katika Roho. Hivi ndivyo Kristo aishivyo ndani yetu.

Dennis Smith anaandika: "Haki kwa imani ina nyanja ya kuthibitisha na kutakasa. Haki humaanisha kwamba Mungu humweka huru muumini kutoka dhambini na kutoka katika adhabu na kumvika haki ya Kristo mdhambi aliyetubu (utii kamili)."[77]

Hivyo mbadilishano wa kustajaabisha zaidi hutokea: Kristo huitwaa hatia yangu na kunikirimia haki Yake. Kupitia mbadilishano huu, tunasimama mbele ya Baba kana kwamba kamwe hatukuwahi kutenda dhambi. "Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi." (Zab. 103:12) Kwa neema ya Mungu tunaweza kwenda maishani tukiwa huru bila hatia.

Kristo amefanywa kuwa utakaso wetu. Je utakaso humaanisha nini? "Utakaso wa kweli humaanisha upendo

77 Dennis Smith, 40 Days: Prayers and Devotions to Revive Your Experience With God, book 2, uk. 18.

kamili, utii kamili, kufuata kikamilifu mapenzi ya Mungu."[78] Umuhimu wa Kristo kukaa ndani yetu ili kuleta matokeo ya maisha ya utii wenye furaha, utajadiliwa kwa kina zaidi katika sura ya 4 "Utii kupitia Yesu." Kristo amefanywa kuwa wokovu wetu, yaani, msamaha wa hatia yote, uhuru kutoka kwenye kifungo cha dhambi, uzima wa milele katika utukufu wa Mungu. Yesu alilipia fidia hiyo kwa kafara Yake.

Katika kipindi cha biashara na usafirishaji wa watumwa Barani Afrika, wafungwa walikuwa na ukosi wa chuma uliofungwa kuzunguka shingo zao kisha ukaunganishwa kwa wafungwa wengine kwa mnyororo. Mara kadhaa mmojawapo wa watu hawa maskini alikombolewa njiani. Mara baada ya fidia kulipwa, mfungwa huyo aliwekwa huru kutoka kwenye ukosi wake wa chuma. Yesu ametukomboa—amelipia fidia kwa ajili yetu.

Mtazamo wa Yesu utaimarishwa hatua kwa hatua ndani yetu. Tunaweza kudai Wafilipi 2:5 tunapoomba: *"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu."* Tunapomruhusu Kristo aingie ndani, basi ataruhusu mtazamo Wake wa fikra na mwenendo ujidhihirishe ndani yetu. Ndipo tutapenda apendacho. Tunakaa mbali na mambo asiyotaka.

### Yesu hutelekeza kazi njema kupitia kwangu

Neno la Mungu linasema katika Waefeso 2:10: "Maana tu kazi Yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo." Mungu ameandaa kazi njema kwa ajili yangu na wewe—kama tupo "katika Kristo"—ili tuweze kuzitekeleza. Kwa kutimiza jukumu hili, Bwana wetu ametayarisha njia makini. Kwa kumtendea kazi na kuwahudumia wengine katika kazi hii, mambo matatu hutokea:

1. Uponyaji endelevu wa ubinafsi wangu sababu nawahudumia wengine

78 Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 565.

2. Wengine hupokea baraka kupitia kwangu.
3. Bwana hunirejeshea baraka tele.[79]

Tutakua kupitia hilo kwa imani; uwezo wetu kivitendo, wa kiakili, na kiroho utaimarika, furaha na nguvu yetu vitaongezeka, na katika mchakato huo, tunatenda kazi kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Jukumu hili litatuandaa kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

Lipo swali lingine kuu linalohusika: Je namfanyia Mungu kazi katika nguvu zangu za kibinadamu au Bwana hutenda kazi kupitia kwangu kwa uwezo Wake wa kiungu?[80]

### Huniwezesha kuwa shuhuda/shahidi Wake

Kwa vile Yesu alikuja "kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" (Luka 19:10), atawaongoza watu kwa asili kupitia kwangu ili wapate wokovu. "Yesu, akaaye ndani yako, ana shauku ya kuzungumza na mioyo ya wale wasiomfahamu."[81] "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu." (Matendo 1:8). Tutarejelea mada hii katika sura ya 5 "Imani Inayovutia kupitia Yesu".

Mungu anatuhimiza tuendelee "kuomba katika Roho Mtakatifu" (Yuda 20). Kristo anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo tunaweza kuomba katika Roho Mtakatifu pamoja na kuomba katika jina la Yesu. Yesu anatuhakikishia: "Nanyi mkiomba lolote kwa jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." (Yohana 14:13) Tunaambiwa bayana: "Hatupaswi tu kuomba katika jina la Kristo, bali pia kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu."[82]

Nini maana ya kuomba katika jina la Yesu? "Kuomba katika jina la Yesu ni zaidi ya kutaja tu jina hilo mwanzoni na mwishoni mwa maombi. **Ni kuomba katika nia na roho ya Yesu, ilhali tukiziamini ahadi Zake, tukitegemea neema**

79 Kitabu cha 3 katika mfululizo mdogo uitwao Hatua za Uamsho Binafsi wenye kichwa kisemacho "Washirika wa Yesu Waliojawa Roho—Nawezaje Kuwa Hivyo?" (2019).
80 Kwa vidokezo vya kina zaidi, angalia: www.steps-to-personal-revival.info kwenye "Development."
81 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 115.
82 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 147.

**Yake, na kuzifanya kazi Zake.**"[83] Hivyo, kuomba katika jina la Kristo kuna vipengele vinne:

1. Kuomba katika roho ya Yesu humaanisha kujazwa Roho Mtakatifu.
2. Kuamini katika ahadi Zake, kudai ahadi ilhali tukiomba.
3. Kutegemea neema Yake, kwa imani, katika uhusiano wa kipekee pamoja na Mungu.
4. Kutenda kazi Zake, mfano kupitia Roho Wake aliye mtii katika mambo yote.

Tunapodumu katika Kristo, ndipo masharti haya yote ya msingi hutimizwa kwa neema Yake. Hivyo, kuomba katika jina la Yesu humaanisha kuomba katika uwezo Wake.

Aliahidi kujibu maombi yetu. Hii huonesha kwamba Yesu ana imani kubwa sana katika wale wakaao ndani Yake. Tunaweza kujinufaisha kwa ahadi zote kupitia Kristo ndani yetu.[84] *"Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika Yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika Yeye ni Amin."* (2 Kor. 1:20) *"Kwa kuwa uweza Wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake Mwenyewe [hii humaanisha uhusiano wa kina pamoja na Yesu Kristo]. Tena kwa hayo ametukirimia* ***ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu."*** (2 Pet. 1:3, 4) Zingatia njia adhimu ya Mungu: tayari ametupatia tunachohitaji ili kuishi kwa kufuata mwenendo wa utauwa. Tunapokea karama hizi kupitia uhusiano wa kina pamoja na Kristo. Vitu hivi hukirimiwa kwetu katika uhusiano huu kupitia kudai ahadi katika maombi, yaani, kupitia maombi ya imani ili tuweze kushiriki asili ya uungu.

### Kukombolewa kutoka kwenye nguvu ya dhambi

*"Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima* [yaani,

83 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 100, 101.

84 Kudai ahadi katika maombi kunaelezewa kwa kina katika Hatua za Uamsho Binafsi Na H. Haubeil, Sura ya 5: Ufunguo wa Uzoefu wa Utendaji

nguvu ya Roho Mtakatifu iletayo uzima] *ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."* (Rum. 8:1, 2)

Kwa nini hakuna hukumu kwa wale walio katika Kristo Yesu? Kwanza, kwa sababu Kristo amejitwisha hatia yangu ya dhambi. Pili, anapokuwa ndani yetu, kifungo cha dhambi juu yetu huvunjwa; tunawekwa huru kutoka kwenye sheria ya dhambi. Hii humaanisha kwamba hatulazimiki tena kuendelea kutenda dhambi, japo inawezekana kutenda dhambi. Wagalatia 5:16 inasema jambo fulani muhimu kuhusu kukombolewa kutoka kwenye nguvu ya dhambi: "Enenda katika Roho [ikimaanisha: ishi daima pamoja na Roho Mtakatifu], ndipo hutatimiza tamaa ya mwili."

Maandiko yanayofuata katika Wagalatia 5, aya ya 17 na 18, hueleza kwamba hii inahusiana na maisha pamoja na Roho Mtakatifu. Aya ya 19–21 huorodhesha kazi za mwili, tusizopaswa kuendelea kuzifanya tena tunapoishi pamoja na Roho Mtakatifu. Kristo ndani yetu hutulinda dhidi ya dhambi na kazi ya malaika walioanguka, kama ambavyo 1 Yohana 5:18 huthibitisha: *"Twajua ya kuwa wale walio watoto wa Mungu hawaendelei kutenda dhambi. Mwana wa Mungu huwalinda salama. Yule mwovu hawezi kuwadhuru."* (NIrV) Kristo huijaza mioyo yetu kwa Roho Mtakatifu kiasi kwamba uovu hauna nafasi tena. Hata hivyo, katika hatua hii, lazima pia tuzingatie kwamba *"Utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku"* (2 Kor. 4:16).

### Kristo ndani yetu hutuhimiza tusitende dhambi

Katika 1 Yohana 3:6–9, tunasoma maneno yafuatayo yenye umuhimu kuhusu dhambi: *"Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi, kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua. Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye. Yeyote atendaye haki yuna haki, kama Yeye alivyo na haki. Atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi. Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi kwa sababu uzao wake wakaa ndani*

*yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu."* (ESV)

Wataalamu wa Kiyunani cha kale hutuambia kwamba maneno haya bayana kuhusu kutenda dhambi hurejelea mazoea ya kutenda dhambi. Kwa mujibu wa maandishi asili ya Kiyunani, yanasema, "hatendi dhambi mfululizo, yaani, kimazoea (lakini mara chache anaweza kuanguka dhambini). Tukiwa kama watoto wa Mungu tunafanya yaliyo mema na tunashika amri za Mungu."[85] Hii humaanisha kwamba tukiwa na Kristo ndani yetu, tunaweza kuachana na mazoea yetu ya dhambi. Maisha yetu pamoja na "Kristo akiwa ndani yetu" hutusaidia kupata ushindi dhidi ya dhambi zinazotusumbua.

### Je tutakuwa "watu wa mwilini" tena kwa kutenda dhambi?

Hebu tuzingatie akilini kwamba kupitia badiliko hili la pekee ajabu hatuifikii hali ya kutokuwa na dhambi. Tunaweza kuanguka dhambini kupitia udhaifu, harara, au upumbavu. Endapo jambo kama hilo likitokea, basi tunahitaji "kupumua kiroho." Hii humaanisha kuungama dhambi yetu, kuukubali msamaha, na tena kuomba kujazwa Roho Mtakatifu. Kadiri ambavyo "tunapumua kiroho," tutaendelea kubaki kuwa Wakristo wa kiroho na wala hatuwi watu wa mwilini tena. Dhambi haikatishi uhusiano wetu wa kiroho pamoja na Mungu; hata hivyo, ni usumbufu ambao lazima tuukabili.

Tunakuwa watu wa mwilini tena endapo tukiruhusu hali ya kutoamini ikite mizizi na tukiacha "kupumua kiroho." Asili yetu ya dhambi hudumu nasi hadi ujio wa pili wa Kristo. Hakuna mtume aliyewahi kudai kuwa hana dhambi. Hata hivyo, "Kristo ndani yetu" hufanya badiliko la dhati katika uhusiano wetu na dhambi.

### Matokeo halisi

Mtume Yohana anaandika: *"Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye*

85 Werner E. Lange, Hrgb., Unser größtes Bedürfnis (Lüneburg: 2011), S. 31.

*Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.”* (1 Yohana 2:1) Mungu anatamani tuishi maisha yasiyo na dhambi ndani ya Kristo, lakini kama tukitenda dhambi, basi tunaweza kumwomba Wakili wetu msamaha na kuupokea. Ellen White anasema, “Dhambi ingeweza kupingwa na kushindwa tu kupitia utendaji madhubuti wa nafsi ya tatu ya Uungu, ambaye angeweza kuja bila nguvu pungufu, bali katika utimilifu wa uweza wa kiungu.”[86]

Kwa njia ya Kristo aishiye ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, nguvu ya dhambi juu yetu huvunjwa na hatimaye itapunguza mwenendo wetu wa/kiwango chetu cha kutenda dhambi.

## Afya Maridhawa

Kristo ndani yetu atatufanya tuzingatie kutunza afya zetu: *“Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.”* (3 Yohana 2) *“Mungu wa amani Mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, Naye atafanya.”* (1 Thes. 5:23, 24)

Katika mhadhara uliowasilishwa na mwanajenetikia/mtaalamu wa sayansi ya vinasaba katika seli za viumbe hai aitwaye Dkt. Sang Lee, alisisitiza kwamba kupitia uhusiano wa kumtumaini Kristo jeni zetu/vinasaba vyetu hufanya kazi vizuri na kuzalisha homoni zenye afya bora.

Uhusiano kati ya imani na afya ni ujumbe ambao ulimwengu unahitaji haraka. Ujumbe huu unaweza tu kubebwa na wanafunzi wa Yesu, ambao kila siku hujitoa kikamilifu pamoja na vyovyote walivyo na yote waliyo nayo, ambao kila siku wanaomba na kumpokea Roho Mtakatifu, na ambao binafsi wanaishi kwa kufuata ushauri wa matengenezo ya afya.

Tafiti zilizofanywa kwa watu 35,000 katika kipindi cha zaidi ya miaka thelathini chini ya usimamizi wa Profesa Grossarth-Maticek zilionesha kwamba kigezo thabiti zaidi katika afya maridhawa ni uhusiano na Mungu wenye upendo na wa hiari. Uhusiano huu unapokuwepo, basi vigezo vingine vya

86 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, Januari 5; uk. 13.

afya, mathalani lishe bora, mazoezi, na siha huimarika mara nyingi zaidi.[87] Hii huonesha wazi maana ya andiko lifuatalo la Biblia: *"Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye."* (1 Tim 4:8) Katika kitabu cha 3 cha *mfululizo wake wa 40 Days, : Kanuni za Mungu za Afya kwa ajili ya Watu Wake wa Siku za Mwisho,* Dennis Smith huonesha mbinu tofauti kabisa ya kuzingatia afya kuliko ile ambayo kwa kawaida tumeifahamu. Anabainisha jinsi gani Roho Mtakatifu anavyohamasisha na kutenda kazi ili kubadili mitindo ya maisha. Hivyo, afya ya kihisia ina umuhimu mkubwa.

Smith anaeleza: "Masomo haya 40 ya maombi yatatuonesha jinsi tuwezavyo kushirikiana na Mungu ili kuweza kupata badiliko kamili la kimwili, kihisia, na kiroho, hali anayotaka tuipate.."[88]

Mfanyabiashara mmoja aliandika: "Niliukubali ujumbe wa afya kupitia kujazwa Roho Mtakatifu kila siku .. Kabla ya tukio hili, hakuna hata semina moja ya afya iliyowahi kuwa na manufaa yoyote kwangu. Nilipenda nyama na wala sikujali sana kwamba ilikuwa aina gani; pia nilikunywa kahawa na chai ya majani ya chai.. Sikudhani hili ni tatizo. Mara kadhaa pia nilikunywa bia. Tangu mwaka 2009 nimekuwa nikiomba kila siku kujazwa Roho Mtakatifu. Alinishawishi niachane na ulaji wa nyama, unywaji wa kahawa, chai ya majani ya chai, na bia. Nimekuwa vejeteriani/Sili nyama. Nimegundua kwamba maisha pamoja na Roho Mtakatifu ni msingi wa ushindi katika mambo yote, mathalani kanuni za kiasi na mtindo wa maisha."[89]

Dada mmoja aliandika maelezo yenye kichwa cha somo kisemacho "Kujitoa kikamilifu kulibadili maisha yangu" (hapa

87 Kwa mujibu wa Medical Wellness mit Newstart—Plus, by Drs. Heide (Leipzig:, 2014), uk. 333, 334.

88 Dennis Smith, 40 Days: God's Health Principles for His Last-Day People, book 3 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2012), Siku ya 1.

89 Baruapepe kutoka kwa mfanyabiashara mnamo Machi 3 na Machi 21, 2013, imefupishwa na kutahasilishwa.

tunawasilisha vipengele vya afya tu): “Kila siku namwalika Roho Mtakatifu aishi na kutenda kazi moyoni mwangu. … Sili tena kila wakati. Hilo lisingewezekana kwangu kwa nguvu zangu mwenyewe. Naweza kufanya majukumu yangu ya kila siku kwa amani zaidi, na wala msongo haufanyi tumbo langu lijisokote tena. Pia Mungu alinipatia nguvu ya kuacha kunywa kahawa. Awali, hili lisingefikirika, sababu nilipoacha kunywa kahawa nilikumbwa na maumivu ya kutisha ya kichwa kwa siku tano. Hizi ni athari kali za kujitoa kwenye uraibu. Mara hii hata sikufikiria athari ambazo ningepata. Nilijua tu kwamba sikutaka kuendelea tena kufanya hivyo. Leo, sina tena shauku ya kahawa. Nilikuwa napitia uzoefu kama huo kuhusiana na nyama. Mimi na familia yangu kamwe hatukupenda kuachana na ulaji wa nyama. Leo ni rahisi kwangu—sina tena shauku ya kuila.”[90] Mmojawapo wa wataalamu wetu mahiri aliandika: “Hitaji halisi la wakati wetu siyo tu elimu ya afya—tunazo taarifa bora kabisa. Kinachohitajika ni taarifa ya afya pamoja na nguvu ya kuitekeleza kivitendo. Inahusu tu nguvu ya kufanya mabadiliko.”[91]

Injili inatupatia nguvu ya kufanya mabadiliko, kwa sababu ya Kristo ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu.

## Badiliko kubwa katika maisha ya Hudson Taylor

Wakati Hudson Taylor akisimamia Misheni ya China Bara, alipokea barua kutoka kwa mmishenari mwenziwe aitwaye McCarthy. Mungu alitumia barua hii kufumbua macho yake atambue ukweli adhimu wa kukaa kwetu ndani ya Kristo na Yeye kukaa ndani yetu. Ilidhihirisha ukweli kuhusu siri ya muunganiko kati ya muumini pamoja na Kristo. Kuanzia siku hii na kuendelea, njia ya Taylor ya kuenenda pamoja na Mungu ilikuwa njia ya amani, pumziko, na ushindi. Wamishenari wenzake waligundua badiliko hili la

90 Ushuhuda kamili unaweza kusomwa katika Kijerumani kwenye www.missionsbrief.de – Archiv – Missionsbrief Nr. 42, S. 17, Völlige HIngabe veränderte mein Leben.

91 Don Macintosh, Director Newstart Global, Weimar, USA, in D’Sozo, (Remnant USA), Dibaji.

kushangaza. Walizungumzia jinsi Taylor alivyokuwa akipitia njia mpya kama mtu mpya katika ulimwengu mpya ili kusimulia ushuhuda wake wa kile ambacho Bwana alikuwa amemfanyia.

Taylor alimwandikia dada yake barua huko Uingereza. Alijaribu kuuelezea ukweli huu adhimu aliokuwa ameugundua na uzoefu wa ajabu aliokuwa ameupata akiwa pamoja na Mungu. Aliandika: "Kamwe kazi yangu haijawahi kuwa pana, iliyojaa wajibu na ngumu kama sasa, lakini sasa shinikizo na msongo vimetoweka kabisa. Mwezi uliopita pengine ndio ulikuwa mwezi wenye furaha zaidi maishani mwangu. Natamani kukwambia kidogo juu ya kile ambacho Bwana amenifanyia. Sijui kama naweza kufafanua wazi jambo hilo, sababu hakuna hasa kitu fulani kipya au cha ajabu au cha kushangaza lakini kila kitu ni kipya! Kwa ufupi: 'Mahali nilipokuwa kipofu, sasa naweza kuona!' Mzigo wangu ulipokuwa mkubwa zaidi, Mungu alitumia sentensi katika barua kutoka kwa McCarthy ili kusababisha magamba yaanguke kutoka machoni mwangu. Roho wa Mungu alinifunulia ukweli kuhusu umoja wetu na Yesu kiasi ambacho kamwe sikuwahi kujua hapo kabla."

Taylor aliendelea katika barua yake kuelezea jinsi Bwana alivyokuwa amefungua fahamu zake ili ayatambue maneno ya Kristo—kwamba Yeye ni Mzabibu na waumini ni matawi. Aliandika: "Ni furaha ilioje kuuona ukweli huu!" Kisha akaendelea: "Sehemu tamu zaidi—kama mtu anaweza kuzungumzia sehemu moja kuwa tamu kuliko nyingine, pumziko ambalo huletwa kwa njia ya kujiweka karibu [mapatano na kujitoa] kikamilifu na Kristo. Sina tena wasiwasi kuhusu chochote, ninapotambua hili; maana Yeye, najua, anaweza kutimiza mapenzi Yake, na mapenzi Yake ni yangu. Haijalishi ananiweka wapi, au kwa namna gani. Ni muhimu zaidi kwamba anazingatia hili kuliko mimi. Maana katika hali rahisi zaidi lazima anikirimie neema Yake, na katika hali ngumu zaidi neema Yake inatosha."

Dennis Smith anasema yafuatayo kuhusu uzoefuwa Taylor: "Hudson Taylor alipata siri ya ushindi katika safari yake pamoja na Mungu. Aligundua jinsi ambavyo angeweza kupata

amani kuu katika kila hali katika huduma yake kwa ajili ya Kristo. Mungu huwapatia watoto Wake wote ushindi kama huo na amani kama hiyo. Je unatamani ushindi na amani ya namna hiyo? Ni ombi langu kwamba kila mtu … apate hasa ushindi na amani hii katika Kristo—furaha ambayo hapo awali ilionekana kutowezekana."[92]

Naungana katika wito huu na kumtakia kila mmoja ambaye Kristo anakaa ndani yake kupitia Roho Mtakatifu apate maisha maridhawa na yenye mafanikio tele kwa ajili ya Kristo, ambayo hubainishwa kwa nguvu isiyo ya kawaida ya Roho Mtakatifu. *"Akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana."* (Yohana 15:5)

Yesu anasema kuhusu Yeye Mwenyewe: *"Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake."* (Yohana 14:10) Yesu ana shauku kuu kwamba mimi na wewe tuweze kusema, Yesu Kristo, aishiye ndani yangu, anatimiza kazi Zake. "Kristo moyoni, Kristo maishani, huu ni usalama wetu."[93]

***Sala:*** *"Bwana Yesu, nashangaa sana kuhusu ukweli kwamba unataka kuingia maishani mwangu. Ninapokupatia maisha yangu, unayajaza Roho Mtakatifu. Nataka kukusifu na kukushukuru kwamba kupitia neema ya Mungu umekuwa hekima, haki, utakaso na ukombozi kwa ajili yangu (1 Kor. 1:30). Tafadhali nipatie ukuaji wa furaha na uonekanao bayana kupitia ushirika pamoja Nawe kupitia Roho Mtakatifu. Amina."*

92 Dennis Smith, Spirit Baptism and Abiding in Christ, uk. 10, 11. Mapendekezo ya usomaji zaidi: Dennis Smith, 40 Days: Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming, book 1 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2009), hususan Siku ya 4: "Christ in You," uk. 18, pamoja na sehemu ya nne ya kitabu kiitwacho, Spirit Baptism and Abiding in Christ, uk. 81–102.

93 Ellen G. White, The Ministry of Healing, uk. 511.

**Mungu anatungoja tuwe na shauku ya Roho Mtakatifu**

"Nguvu ya Mungu hungojea kudai na kupokea kwao. Baraka hii iliyoahidiwa, ikidaiwa kwa imani, huleta baraka zingine zote pamoja nayo. Hukirimiwa kadiri ya utajiri wa neema." DA 672.1 #13

## Wanandoa na Roho Mtakatifu

**Ukaribu Mkuu katika Wanandoa**

Mimi na mume wangu tulibarikiwa tuliposoma Hatua za Uamsho Binafsi. Tunakisoma pamoja mara ya 3! Huweka uzoefu wa maisha yetu katika maneno na huonesha hali zenye changamoto za maisha. Kwa kusoma na kuomba pamoja kimetuongoza katika ukaribu na umoja ambao kamwe hatujawahi kuwa nao hapo kabla! Ni jambo la pekee ajabu kuwa timu! Kutenda kazi, kuomba, kuwaelimisha na kuwatumikia wengine ni ridhaa ilioje! Ni wapi tunaweza kununua boksi za vitabu hivi? A.C. imefupishwa, #119

**Uzoefu wa Kushangaza**

Kitabu kiitwacho 40 Days kilitu-patia uzoefu wa pekee ajabu. Kwanza kabisa ulikuja uamsho binafsi. Kupitia kujifunza pamoja na kubadilishana mawazo nyakati za asubuhi, tulizidi kukaribiana pamoja kiroho kama wanandoa. Baada ya kuomba pamoja, tuliuona mkono wa Mungu uongozao kila siku—hata kwenye mazingira ya kawaida sana. Haielezeki ni nguvu kiasi gani tulipokea ili kukamilisha majukumu ya kila siku. C.a.K.R. (imefupishwa), #3

**Nilipambana katika maisha ya ndoa yangu**

Namsifu Mungu kwa kufumbua macho yangu kiroho tangu nisome *Hatua za Uamsho Binafsi.* Mimi si Mkristo yuleyule tena. Kwa vile nilikuwa Mwadventista, nilidhani mimi ni Mkristo mwenye uzoefu, lakini ndani hasa nilitambua kitu fulani kinakosekana. Nilipambana katika maisha yangu ya ndoa kwa ajili ya kudumisha uhusiano na mume wangu, ambaye pia ni mshiriki wa kanisa. Sasa tunaomba pamoja na kuhimizana kuhudhuria kanisani. #120

**Kitabu hiki huwasaidia wanandoa pia**

Nilienda kwenye duka la vitabu la Kiadventista. Nilioneshwa kitabu, Hatua za Uamsho Binafsi. Sikutaka niwe nacho. Mwanamke muuzaji alinihimiza na kusema, “Kitabu hiki huwasaidia wanandoa pia. Mpwa wangu alikuwa ametengana na mume wake. Kitabu hiki kiliwaleta tena pamoja. Sasa wanaomba pamoja na kuhudhuria kanisani pamoja.” Hivyo, nilinunua kitabu hicho na tumekiona kama tunu adhimu. #120 a

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Yapi matokeo mbalimbali ya kuwa mmoja na Kristo?*

   ______________________________

2. *Nini maana ya kuomba katika Roho ya Yesu?*

   ______________________________

3. *Nini ambacho Kristo hukitimiza ndani yetu katika kuikabili dhambi?*

   ______________________________

4. *Je tunafikia hali ya kutokuwa na dhambi kupitia Kristo?*

   ______________________________

5. *Kuna uhusiano gani kati ya imani na afya?*

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*

6. Kwamba "Kristo ndani yetu" aweze kuwa na matokeo *yaonekanayo bayana katika maisha yetu kila siku.*

7. *Kwa ajili ya ufahamu na uwezo wa kuomba katika Roho ya Yesu.*

8. *Kwa ajili ya uzoefu unaoleta uhuru wa kushinda mazoea ya dhambi.*

9. *Kwamba atulinde dhidi ya kiburi cha kiroho na hali ya kukosa kiasi.*

SURA YA 4

# Utii Kupitia Yesu

*Jinsi gani naweza kuishi katika utii wenye furaha?*
*Furaha ni nini?*
*Kwa nini utii ni kwa ajili ya manufaa yangu?*
*Jinsi gani utii kupitia "Yesu ndani yangu" unatenda kazi?*
*Je utii kwa imani ni ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu?*
*Je Mungu anafanya nini?*
*Mwanadamu anafanya nini?*

### Biblia na ratiba ya treni

Wakati wa mkutano fulani huko Frankfurt am Main, Germany/Ujerumani, wanafunzi wa theolojia walimuuliza mzee mmishenari Hudson Taylor, "Unaweza kuaminije kila neno kwenye Biblia?"

Jibu lake lilikuwa, "Ukitaka kusafiri kwenda nyumbani kesho, utafungua ratiba ya treni na kutazama nyakati za kuondoka. Na kama ukigundua kwamba treni inaondoka saa 1:00 asubuhi, basi hutauliza maswali mengine zaidi, bali unaenda kwenye kituo cha treni siku inayofuata na kuipata treni yako tayari kwa kuondoka. Kama tu ambavyo unatumia ratiba yako ya treni, nimefanya hivyo kuhusiana na Biblia na amri na ahadi zake kwa kipindi cha miaka 50 iliyopita. Nimeona mafundisho yake kwamba wakati wote ni kweli kwenye maisha yangu marefu na katikati ya mamia ya hatari za kufisha. Mfano, Biblia inaposema: *'Bali utafuteni kwanza ufalme Wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.'* (Mat. 6:33) Nilifuata maelekezo haya na kamwe sijafadhaishwa

katika hali yoyote tatanifu. Endapo ukifanya vivyohivyo, basi utakuwa na uzoefu wa jinsi hiyo."[94]

Kuakisi utii kupitia Kristo kutatupatia furaha kuu. Tunataka kufanya hilo sasa. Utii huu una jina maalum: utii wa imani.

## Kwa lengo gani Mungu huwaita wachungaji?

Katika Warumi 1:5, nilipata maelekezo yenye umuhimu mkubwa kwangu kama mchungaji: *"Ambaye kupitia Kwake [Yesu Kristo] tumepokea neema na utume ili kuleta utii wa imani kwa ajili ya jina Lake miongoni mwa mataifa yote."* (ESV)

Hii humaanisha kwamba Mungu huwaita watu waje kwenye huduma Yake ili wawaongoze wengine katika utii wa imani. Hii hudai kwamba nielewe suala hili vizuri, na kwamba kwa msaada wa Mungu niwe mfano mzuri. Ninapofanya hivi, basi natenda katika jina lake, ambapo humaanisha katika mamlaka ya Yesu Kristo.

## Jinsi gani utii wa imani hutokea?

Maneno ya mwisho ya waraka kwa Warumi huongeza wazo lingine: jinsi gani Mungu anataka kutimiza utii huu wa imani. *"Sasa na atukuzwe Yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, lakini sasa imedhihirishwa, na kwa maandiko ya manabii, kama alivyoamuru Mungu wa milele, ikajulishwa kwa mataifa yote kwa ajili ya* ***utii wa imani****: Kwa Mungu pekee mwenye hekima, utukufu uwepo, kupitia Yesu Kristo milele. Amina."* (Rum. 16:25–27, KJV)

**Aya hizi hueleza kuwa siri ilidhihirishwa kwa ajili ya kusudi mahususi—ili kuinua utii wa imani,** ingawa hazielezei siri hiyo ni nini. Tunapata maelezo katika Wakolosai 1:27: *"Kwa hao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu."*

94 Taarifa iliyoandaliwa na Prof. Dr. Karl Heim katika mwongozo wa ibada, ambayo kwa sasa sina mkononi

**Siri hii ni: Kristo ndani yetu.** Na matokeo ni yapi pale ambapo utii wa imani unapotimizwa katika Kristo? *"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."* (2 Kor. 5:17) Tuna maisha mapya Kristo akiwa ndani yetu. Andiko lingine huelezea maisha haya mapya kama ifuatavyo: *"mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu."* (Efe. 3:19)

## Tunayatambuaje maisha katika utii wa imani?

Mtazamo wetu kuhusu amri Zake hubadilika. *"Wala amri Zake si nzito."* (1 Yohana 5:3) *"Nira Yangu ni laini,"* alisema Yesu (Mat. 11:30). *"Nami nitajifurahisha sana kwa maagizo Yako"* (Zab. 119:47), kwa sababu *"ni njema kwangu, kuliko maelfu ya dhahabu na fedha"* (aya ya 72), "ni matamu sana kwangu, kupita asali kinywani mwangu" (aya ya 103), na *"Naifurahia ahadi Yako"* (aya ya 162). Hunipatia *"amani nyingi"* (aya ya 165). Utii wa imani ni jambo linalopendeza.

## Tunahitaji msingi imara kwa ajili ya maisha yetu

Mshairi wa Kijerumani Matthias Claudius anaandika: "Mwanadamu anahitaji nanga imara zaidi, kitu fulani ambacho hakitegemei nafsi yake, bali kitu anachoweza kukitegemea."[95] Siku hizi watu wengi wanakabiliwa na wasiwasi wa kihisia, kwa vile hawana msingi thabiti kwa sababu wamekosa imani. Kupitia uhusiano pamoja Naye, Mungu anataka kutupatia msingi imara uliojengwa katika Neno Lake.

Mkristo mshairi huyu hutuonesha kwamba tunahitaji msingi imara nakanuni imara maishani mwetu. Ni wapi tunaweza kupata msingi imara? Mungu aliweka msingi huu muda mrefu uliopita. Jina Lake ni Yesu Kristo. *"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo."* (1 Kor. 3:11) Yesu ndiye pekee awezaye kutupatia msingi imara kwa ajili ya maisha yetu.

95 Matthias Claudius (Edition Steinkopf, 1982), S. 10.

## Wapi tunapoweza kupata viwango bora kwa ajili ya maisha yetu?

Nani hata mwenye sifa za kuweka viwango hivyo? Nani awezaye kupambanua kile kilicho haki? Biblia inatupatia jibu bayana katika Zaburi 99:4: *"Wewe ndiwe umebainisha lililo adili."* (Sanifi ya Luther ya Kijerumani) Na Zaburi 111:7,8 huongeza: *"Matendo ya mikono Yake ni kweli na hukumu, maagizo Yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele, Yamefanywa katika kweli na adili."* (cf. Zab. 148:6)

Mungu, Muumbaji, amebainisha kile kilicho haki. Hakuna yeyote isipokuwa Mungu ndiye astahiliye kuweka viwango au kanuni. Muumbaji pekee, Mmiliki mkuu wa vitu vyote, anayo haki hii. Hakuna mwingineyo mwenye mtazamo dhahiri kuliko Yeye; Mungu pekee ndiye ajuaye yote na mwenye hekima yote.

Tabia ya Yule awekaye viwango ni yenye umuhimu mkubwa. Biblia inatuonesha kwamba Mungu ni upendo; Yeye ndiye Chanzo cha upendo na kweli, furaha na haki. Sababu ya tabia Yake ya pekee ajabu, uwezo na ufahamu Wake usio na kikomo, Mungu aliweza kuweka kanuni linganifu kwa ajili ya malaika, wakazi wa malimwengu mengine, jamii ya wanadamu, na wanyama. Muumbaji mwenye upendo aliumba mazingira maridhawa kwa ajili ya kutegemeza maisha.

Siyo kwamba alifanya hivi kwenye sheria za asili, katika, mfano, vitu visivyobadilika vya dunia hii—umbali kutoka kwenye jua hadi kwenye mwezi, mwelekeo wa mhimili wa dunia, na kadhalika—lakini pia aliweka sheria kwa ajili ya furaha ya wanadamu katika hidaya na maadili (cf. Yer. 7:23). Baba yetu wa mbinguni mwenye upendo alianzisha taratibu adhimu kwa ajili yetu.

Tunahitaji kudumisha wazo hili akilini wakati tukijadili shani ya kustajaabisha katika nyakati za mwisho—mkanganyiko mkuu kuhusu utii wa sheria za Mungu.

## Mkanganyiko kuhusu utii wa kanuni za Mungu

Paulo anasema katika 2 Wakorintho 4:3, 4, *"Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini,*

*isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu."*

Shetani hupofusha na kujificha. Akili iliyopofushwa huweza kudokeza mambo mawili: kwanza, kwamba mambo fulani hata hayaonekani, kiasi kwamba yamesitiriwa au kufichwa. Pili, inaweza kuwa na maana ya akili ambayo "imehadaiwa," ambayo huona maeneo yasiyo sahihi ikidhani ni sawa. Hatutambui jinsi gani dhana hizi zinavyoghilibishwa kwetu. Hali hii ya kificho na upofushaji huzuia mtazamo sahihi.

Andiko hili linasema kwamba hii huwatokea wasio waumini. Lakini tunafanya ugunduzi wa kushangaza kwamba jambo lilohilo huwatokea Wakristo wa mwilini. Wanamkiri Yesu lakini hawajajisalimisha kikamilifu Kwake. Ndiyo sababu "mungu wa dunia hii" anaweza kuwapofusha.

Nimeshawishika kwamba Shetani hujaribu hila hii ya kuwapofusha Wakristo wa kiroho vilevile. Yesu anasema katika Mathayo 24:24: *"Wapate kuwapoteza kama yamkini hata walio wateule." ."* (KJV) 1 Yohana 5:18 inasema kwa mujibu wa Sanifi ya Luther ya Kijerumani: *"... yule aliyezaliwa na Mungu humlinda salama wala mwovu hamgusi."* "Siyo tu kwamba Shetani anauongoza ulimwengu kuwa mateka, lakini madanganyo yake huyachachusha makanisa yanayomkiri Bwana wetu Yesu Kristo."[96] Kwa namna bayana Yesu anaelezea shani hii katika ujumbe Wake kwa Walaodikia katika Ufunuo 3:17.

Katika hotuba Yake kuhusu matukio ya siku za mwisho katika Mathayo 24 na 25, mara nne Yesu anataja ishara mojawapo mahususi katika siku za mwisho: udanganyifu. Tayari udanganyifu ni imara sana, lakini utaongezeka. Yule anayepofushwa, kwa nadra hulitambua hilo. Nadhani kila mmoja wetu anapaswa kujitathmini mwenyewe. Tunapaswa kutambua kwamba Roho Mtakatifu pekee ndiye anaweza kufumbua macho yetu na kutambua ukweli na udanganyifu. Eneo moja lenye udanganyifu mkuu linahusiana na utii wa mapenzi ya Mungu, kuhusu Neno la Mungu, na kuhusu sheria za Mungu. Wengi hawana utambuzi bayana ni aina gani ya utii

96 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 60, 61.

ambao Mungu anataka na jinsi gani inavyowezekana kwetu kuwa watii. Huu ni utii wa imani—aina maalum ya utii.

## Nini maana ya utii wa imani?

Tunakabiliana na chaguzi kadhaa katika kufasili istilahi hii ambayo mtume Paulo aliunda. Hakika ni utii ambao hufuata hasa mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi. Unahusiana na kuingia katika uhusiano halisi wa kumtumaini Yesu kupitia Roho Mtakatifu. Matokeo yake ni wokovu kupitia kafara ya Kristo. Kujisalimisha kwangu kwa Yesu kunajumuisha kuzishika amri kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu. Siyo utii kupitia juhudi zangu mwenyewe.

Paulo alichukua msimamo wa makusudi dhidi ya sheria ya kifarisayo ya utii, iliyomaanisha kujitengenezea njia ya kuuingia ufalme wa Mungu kwa juhudi binafsi kwa kutii kisahihi amri za Mungu. Anabainisha wazi kwamba utii ni lazima kwa ajili ya uanafunzi wa kweli, lakini utii huu hutofautiana na ule wa Mafarisayo. Huanza kwa kuukubali wokovu kwa furaha kupitia Yesu Kristo. Huzalisha matendo ya utii maishani mwa mhusika kama mwanafunzi wa Yesu.

Utii huu umejengwa katika tumaini, ambalo hutokea moyoni. Dennis Smith anaandika: “Mtu fulani anapoishi katika uhusiano wa karibu pamoja na Mungu kupitia Roho Mtakatifu, basi utii huja kwa asili  na hutokea moyoni, bila kufikiria sana.”[97] Ni utii ambao hufanywa uwezekane kupitia ushirikiano kati ya uungu na ubinadamu.

## Mungu amefunua siri

Kwa kufupisha Warumi 16:25,27: Kwa amri ya milele ya Mungu, siri ilidhihirishwa, ili kuanzisha utii wa imani. Kwa agizo la Mungu, siri hii ya Kristo ndani yetu hufanikisha utii wa imani. Hivyo utii wa imani ni utii wa hiari uliojengwa kwa imani, tumaini, na upendo. Tunaingia katika uhusiano wa tumaini pamoja na Mungu na kwa kuzingatia tumaini hili

97 Dennis Smith, 40 Days: Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming, book 1, uk. 21, 22.

na katika ufahamu wetu kwamba sheria Zake ni kwa ajili ya manufaa yetu bora, tunaamua kuwa watii.

"Badala ya kumwachilia mwanadamu asitii, ni imani, na imani pekee, ndiyo itufanyayo washirika wa neema ya Kristo, ambayo hutuwezesha kuonesha utii."[98]

## Je siri hii inajumuisha nini?

Paulo anatuonesha katika Wakolosai 1:25–27 kwamba alifanywa *"mhudumu Wake, sawasawa na uwakili wa Mungu… ili kutimiza neno la Mungu; hata* ***siri iliyokuwa imesitirika kwa zama zote … bali sasa imefunuliwa*** *kwa watakatifu Wake."* (KJV) Hii ilikuwa siri ya aina gani? *"Mungu angewajulisha [watakatifu Wake]* ***jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii… ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.*** *"* (KJV)

Siri hii, iliyokuwa imefichwa na sasa imefunuliwa, ni kwamba Yesu Mwenyewe anataka kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Andiko hili husema kwamba hili ni tumaini la utukufu kwa ajili yetu, na humaanisha kwamba utimilifu wa uhai ambao Mungu anataka kutukirimia sasa na uzima wa milele katika utukufu unaweza kupatikana na umehakikishwa. Uhusiano huu wa kina ambao Kristo anataka awe nao pamoja nasi kupitia Roho Mtakatifu, huonesha upendo mkuu wa Mungu kwa namna tofauti kabisa. "Kristo ndani yetu" ndiyo kiini cha siri hii; kwa maana pana zaidi, hiyo ni injili au mpango wa ukombozi.

Warumi 16:25, 26 hutuambia kwamba kupitia siri hii, utii wa imani huanzishwa au hutekelezwa. Hii humaanisha kwamba kupitia Kristo tunaweza kutii, na pia tuna shauku ya kutaka kufanya hivyo.

## Jinsi gani Kristo anakuwa ndani yetu?

Inawezekanaje Kristo kuishi ndani yetu? Tunasoma katika Waefeso 3:16, 17, 19: "[Kwamba Baba] awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa

98 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 60, 61.

mioyoni mwenu kwa imani; kwamba, ninyi, ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo … mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu.”

**Tunaambiwa:**

1. Kupitia Roho Mtakatifu tunapokea nguvu maridhawa kwa ajili ya utu wetu wa ndani.
2. Kupitia Roho Mtakatifu, Kristo huishi ndani yetu kwa imani.
3. Hivyo, tutakuwa tumekita mizizi na kujenga katika upendo. Yesu Kristo anapoishi ndani yetu, basi hujenga tabia Yake ya upendo ndani yetu. Biblia vilevile huliita hili “tunda la Roho” (Gal 5:22).
4. Hii hutuongoza katika maisha yenye “kujazwa utimilifu wote wa Mungu” (angalia pia Yohana 10:10; Kol. 1:9,10).

Kristo ndani yetu humaanisha kwamba utii wetu sasa unawezekana, sababu huletwa na Yesu ndani yetu. Ellen White anasema: “Nafsi inapompokea Kristo, hupokea nguvu ya uzima wa Kristo.”[99] Yesu anaishi ndani yetu tunapomtumaini kikamilifu, yaani, pale tunapokuwa tumeadhimisha nafsi zetu kikamilifu Kwake. Utii unaotokea ni utii wa imani. Kristo anataka kuishi maisha Yake ya ushindi ndani yetu.

Wazo lingine la thamani linapatikana katika Wagalatia 4:19. Paulo anasema hapo: “Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.” Paulo ana shauku ya dhati kwamba Kristo aishi ndani ya waumini. Alisema, “mpaka Kristo aumbike ndani yenu.” Inachukua muda mrefu kiasi gani ili mtu apevuke kikamilifu? Huhitaji angalau miaka kumi na sita au kumi na saba. Naamini kwamba hapa Paulo alikuwa akizungumzia mchakato wa ukuaji. Pale tunapoweka wakfu maisha yetu kwa Kristo halafu tukaomba kila siku kwa imani tupewe Roho Mtakatifu, basi yu ndani yetu, lakini kuna mchakato wa ukuaji katika uhusiano huu.

99 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 60, 61.

## Masuala tata/Dondoo zenye utata

Kwa namna fulani, dondoo kadhaa si dhahiri kuhusiana na utii. Kwanza, tunataka kuangalia dondoo zipi Yesu alitaja kuhusu maisha yetu ya imani: "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." (Yohana 15:5) Hii pia linahusu eneo muhimu la utii.

Pili, hebu tuangalie kauli husiani kutoka kwa Ellen G. White zinazoelezea kanuni za msingi juu ya utii: "Yule ajaribuye kuifikia mbingu kwa matendo yake mwenyewe katika kushika sheria, anathubutu kisichowezekana. Mwanadamu hawezi kuokolewa bila utii, lakini matendo yake hayapaswi kuwa yake mwenyewe; Kristo anapaswa kutenda kazi ndani yake ili kunia na kutenda mapenzi Yake mema."[100]

**Dondoo tatu muhimu zimewasilishwa:**

1. Haiwezekani kuifikia mbingu kwa matendo yangu mwenyewe. Hii humaanisha kwamba kutaka kustahili kujipatia kitu fulani kutoka kwa Mungu (kama katika haki kwa matendo) ni kosa.
2. Hata hivyo, utii ni sehemu isiyoepukika ya maisha pamoja na Mungu, kwa vile wanafunzi wa Yesu wanaitwa kuishi kwa kuyafuata mapenzi ya Mungu.
3. Utii haupaswi kuwa kazi yetu, usiotokana na nguvu yetu, bali kunia na kutenda kunapaswa kutekelezwa na Kristo ndani yetu.

Sasa, tunataka kuangalia kwa ukaribu zaidi jinsi hili linavyofanikishwa.Wapowengiwaaminiokwambawanapaswa kustahili kuingia mbinguni ama kwa sehemu au kikamilifu. Wanadhani wanapaswa kufuata mwelekeo huu potofu sababu hawajui njia adhimu ambayo Mungu amewakirimia. Wanajaribu kujipatia kitu fulani kisichowezekana. Kila mtu ambaye hana Yesu aishiye ndani yake kupitia Roho Mtakatifu, anadiriki kisichowezekana, haijalishi kwamba orodha yao ya hatua za utii ina urefu au ufupi kiasi gani..

100 Ellen G. White, The Review and Herald, Julai 1, 1890, par. 11.

Maandiko hufundisha kwamba hatuwezi kuokolewa kwa matendo yetu wenyewe (matendo ya sheria), bali kwa imani tu katika Mungu. Warumi 3:28 inasema: "Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria." "Hakuna wazo lipaswalo kuzingatiwa kwa dhati zaidi, kurudiwa mara nyingi zaidi, au kuhimizwa kwa uthabiti zaidi akilini mwa wote kuliko lile la kutowezekana kwa mwanadamu aliyeanguka kustahili chochote kwa matendo yake mema kabisa. Wokovu hupatikana kupitia Yesu Kristo pekee."[101]

**Utii ni Lazima**

Yesu anasisitiza utii. Maneno Yake ya mwisho yalikuwa: *"[Wafundisheni] kuyashika yote niliyowaamuru ninyi."* (Mat. 28:20) Hapa ni bayana anazungumzia utii. Amri alizoandika Yesu kwa mkono Wake Mwenyewe halafu akampatia Musa pale Sinai, hudai utii wetu. Matarajio haya kutoka kwa Mungu, ambayo Biblia huyashuhudia, hufupishwa kama ifuatavyo: "Tunu Zake zote zinaahidiwa kwa sharti la utii."[102]

Katika *Christ's Object Lessons,* tunasoma pia: "Tabia ya Mungu hubainishwa katika sheria Yake; na ili uweze kuwa katika upatanifu na Mungu, lazima kanuni za sheria Yake ziwe chemchemi za kila tendo lako."

"Kristo hapunguzi madai ya sheria. Katika lugha isiyokuwa na utata, anawasilisha utii kwayo kama sharti la uzima wa milele."[103]

Mtume Yohana hutuonesha kwamba utii hudhihirisha endapo tunamjua Mungu ama la: *"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika amri Zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake."* (1 Yohana 2:3, 4) *"Naye azishikaye amri Zake hukaa ndani yake Yeye, Naye ndani yake."* (1 Yohana 3:24)

Utii pia ni kiashiria kinachoonesha endapo tunampenda Mungu: *"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; wala amri Zake si nzito."* (1 Yohana 5:3)

101 Ellen G. White, Faith and Works (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 1999), uk. 18.

102 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 145.

103 Ibid, uk. 391.

Biblia hutuonesha kwamba utii ni ishara ya masalia, kanisa la siku za mwisho, pale inapowazungumzia wale "wazishikao amri za Mungu" (Ufu. 12:17). *"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu."* (Ufu. 14:12)

Charles Finney, pengine mhubiri wa uamsho aliyefanikiwa zaidi katika wakati wetu, alisema: "Uamsho ni mwanzo mpya wa kumtii Mungu."[104] Pia tunataka kunukuu *Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Watu Wazima kuanzia* Agosti 31, 2011: "Utii siyo njia ya wokovu, bali ni hali inayodhihirisha matokeo na baraka za wokovu katika maisha ya waliokombolewa."

## Utii katika na kupitia Kristo

Tunaweza tu kuwa watii kupitia Kristo ndani yetu. Yeye pekee ndiye anaweza kufanikisha hili. Akiwa kama mwanadamu, Kristo alikuwa kielelezo cha utii kwetu. *"Ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata."* (Ebr. 5:8) *"Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa mwasisi wa wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."* (aya ya 9)

Matendo 5:32 huthibitisha jambo hili: Mungu huwapatia Roho Mtakatifu wale wanaomtii. Je hii humaanisha kwamba utii wetu kwa amri za Mungu ni sharti la ukombozi wetu? Sivyo kabisa! Badala yake, Paulo anataka kusisitiza tena kwamba njia ya ukombozi ni kwa imani pekee, na kwenye njia hii tunapaswa kuwa watii kwa Mungu. Ndipo atatenda kazi kupitia Roho Mtakatifu kwa namna ya pekee ajabu, kiasi kwamba tuishi kama Mungu apendavyo.

Hiki ndicho hasa aandikacho Paulo katika Warumi 8:3, 4: "Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe Mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Mungu alisema, "Nami nitatia Roho Yangu ndani yenu, na

---

104 Imenukuliwa katika Unser größtes Bedürfnis (Our Greatest Need), Lüneburg: Werner E. Lange, 2011, S. 102

kuwaendesha katika sheria Zangu, nanyi mtazishika hukumu Zangu, na kuzitenda." (Eze. 36:27)

### Kuishi daima katika Roho Mtakatifu

"Kuenenda kwa kufuata mambo ya Roho" humaanisha kuishi daima katika Roho Mtakatifu. Andiko hili huonesha kwamba utii unaohitajika hutimizwa kupitia Kristo ndani yetu, yaani katika wale ambao Roho Mtakatifu anakaa ndani yao. Mungu alimtuma Mwanawe ili haki inayotakiwa na sheria iweze kutimizwa ndani yetu kupitia Kwake. Tafadhali zingatia kwamba andiko hili halisemi kwamba haki inatimizwa kupitia kwetu, bali hutimizwa ndani yetu.

Nini asemacho Paulo katika Wagalatia 2:20 kuhusu maisha yake? "Ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu." Paulo anabainisha wazi kwamba Kristo anaongoza maisha yake. Katika Ezekieli 36:27, Mungu anatuambia, "Nami nitatia Roho Yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria Zangu, nanyi mtazishika hukumu Zangu, na kuzitenda."

Je ni bayana vile lisemavyo andiko hili? Mungu anataka kutukirimia Roho Wake na hivyo atatuumba tuwe watu wazishikao amri Zake. Hii humaanisha kwamba Mungu atashughulikia utii wetu kupitia Roho Mtakatifu.

Hapa tunaona wazi kwamba utii hufanyika kupitia Roho Mtakatifu na Kristo ndani yetu. Ni utii wa dhati moyoni. Bila ushirika huu, tunaweza kuonesha tu utii wa nje usiotosheleza. "Ni kweli kwamba unaweza kuwepo usahihi wa nje wa mwenendo bila nguvu ya Kristo ibadilishayo. Kupenda kuwa na ushawishi na shauku ya kuheshimiwa na wengine huweza kuleta matokeo ya maisha yenye utaratibu mzuri. Kujiheshimu kunaweza kutuongoza kuepuka mwonekano wa uovu. Moyo wa ubinafsi unaweza kutenda matendo ya ukarimu."[105] Pengine tunataka kushika amri za Mungu kwa msukumo wa wajibu au sababu hutegemewa kutoka kwetu. "Mtu anayejaribu kushika amri za Mungu kwa msukumo wa wajibu tu—sababu anatakiwa kufanya hivyo—kamwe hataweza

---

105 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 58.

kuingia kwenye furaha ya utii. Anakuwa hatii. Pale maagizo ya Mungu yanapotazamwa kuwa mzigo sababu yanapinga mwelekeo wa kibinadamu, tunaweza kujua kwamba maisha hayo siyo maisha ya Kikristo. Utii wa kweli ni utendaji wa kanuni kutoka ndani."[106]

### Jinsi gani Kristo anaweza kuishi ndani yetu?

Uhusiano pamoja na Yesu huanza kwa kujitoa kikamilifu Kwake. Hulijibu hili kwa kuzaliwa kwetu upya kiroho (angalia Yohana 3:1–21). Maisha yetu haya mapya, tuliyopewa na Mungu, hudumishwa kwa kufanya upya kila siku uhusiano wetu pamoja na Kristo. Inahitaji kujiweka wakfu kila siku pamoja na maombi yetu kila siku ili kujazwa Roho Mtakatifu—kuburudishwa na Roho. Kwa namna hii Yesu anaishi ndani yetu. *"Ili mwimarishwe kwa nguvu… kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani."* (Efe. 3:16, 17)

Jichunguzeni wenyewe, endapo Kristo anaishi ndani yenu. Maandiko yanatualika tujichunguze endapo Kristo anaishi ndani yetu. *"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa."* (2 Kor. 13:5)

Mungu anataka tuijue hali yetu ya kiroho. Je lini tunakataliwa au tunaonekana kutofaa? Kwa vile tunastahilishwa kupitia Kristo ndani yetu, tunapojazwa Roho Mtakatifu, hivyo kutofaa ni kuwa na maisha yakosayo ujazo wa Roho Mtakatifu. Biblia huiita hii/hali hii nia ya mwilini.

Wakati gani gari letu "halifai"? Pale ambapo halikimbii tena. Kama halina mafuta, nini tuwezacho kufanya? Pengine tunaweza kujaribu kulisukuma au tukanunua mafuta. Kwa kweli, tunajaza mafuta gari. Bila Yesu mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu, utii wetu hufanana na mtu fulani anayejaribu kulisukuma gari lisilo na mafuta.

Je inazidi kuwa bayana kwako jinsi gani Yesu alivyo muhimu kwa ajili ya imani na maisha yetu? Yesu hana mbadala. *"Yeye*

---

106 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 97.

*aliye naye Mwana, anao huo uzima."* (1 Yohana 5:12) *"Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi."* (Yohana 14:6) Tunamhitaji Yesu. Bila Yeye hatuwezi kuokolewa. Hatutakuwa na maisha maridhawa hapa duniani wala uzima wa milele.

Je unaelewa vema jinsi gani utii unavyofanyika? Tunamwonesha Yesu utayari wetu kupitia kujitoa kwetu kila siku na kumwomba atukirimie Roho Mtakatifu ili aweze kutimiza utii ndani yetu. Tunalielewa hili vema tunaposoma 1 Wakorintho 1:30: *"Bali kwa Yeye [Mungu] ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu,* ***aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi."*** Yote haya Kristo anataka na anaweza kutimiza ndani yetu. Na Biblia inaposema kwamba Kristo alikuwa utakaso kwa ajili yetu, basi humaanisha wazi kwamba hilo lilitokea ili tuweze kuishi katika utii.

### Wakati gani tunaokolewa?

Kwa nini jibu la swali hili ni muhimu sana? Ninapokuwa tayari nimeokolewa, basi ni bayana kwamba utii wangu huja kama matokeo ya wokovu wangu. Wala siyo sharti la awali la wokovu wangu. Naokolewa wakati wa hatua yangu ya kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu Kristo. *"Kwa maana* ***mmeokolewa*** *kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."* (Efe. 2:8, 9)

Wakati ule mtume Paulo alipowaandikia Waefeso, aliwaarifu kwamba tayari walikuwa wameokolewa. Hata hivyo, katika Warumi 8:24, anaandika, ***"Kwa maana tuliokolewa kwa taraja."*** Tunao uhuru wa kudumu pamoja na Mungu au la.

Baada ya wokovu wetu (kwa tumaini), shauku yetu kuu ni kukaa katika Kristo hadi mwisho wa maisha yetu au hadi ujio Wake wa pili. Tuliokolewa kwa imani (Efe. 2:8), na baada ya hilo, ni muhimu sana kudumu katika imani hii. *"Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye."* (Kol. 2:6) Wazo la msingi ni kudumu ndani ya Kristo kupitia kujitoa. Dennis Smith anaandika yafuatayo kuhusu

kukaa ndani ya Kristo: "Kukaa ndani Yake siyo kazi tupaswayo kufanya kama sharti la awali kwa ajili ya wokovu wetu. Badala yake hiyo ni ridhaa yetu ya kumruhusu afanye lolote kwa ajili yetu, ndani yetu na kupitia kwetu."[107]

Kwa nini kujitoa kikamilifu ni lazima? Nini manufaa yake?

Kujitoa kikamilifu kunahusiana na kukombolewa kutoka kwenye udhalimu wa ubinafsi wetu. Ubinafsi wetu ndiyo chanzo cha matatizo yetu. Usemi fulani unatuambia: Tatizo kuu zaidi la kila mtu ni nafsi yake mwenyewe. Ubinafsi wetu unakwazwa, unajeruhiwa, na kukasirishwa; hutaka kujitwalia mamlaka yake; una husuda, na kadhalika.

"Mungu ana shauku ya kutuponya, kutuweka huru. Lakini kwa vile hili huhitaji badiliko la nafsi yote, ufanywaji upya wa asili yetu yote, lazima tutoe nafsi zetu Kwake kikamilifu … Huweka mbele yetu kimo cha baraka anachotamani kutufikisha hapo kwa neema Yake. Anatualika tujikabidhi Kwake, ili aweze kutekeleza mapenzi Yake ndani yetu. Ni wajibu wetu kuchagua endapo tutawekwa huru kutoka kwenye kifungo cha dhambi, kushiriki uhuru mtukufu wa wana wa Mungu."[108]

Maisha chini ya utawala wa ubinafsiwetu ni maisha ya utumwa wa dhambi. Maisha pamoja na Kristo ndani yetu ni maisha ya uhuru mtukufu kwa ajili ya watoto wa Mungu. Mfinyanzi anaweza tu kuufinyanga udongo ulio mikononi mwake. Kujisalimisha kwetu kuna umuhimu mkubwa kabisa. Baada ya kujisalimisha kwetu huja hatua ya kukaa katika Kristo. Na tunapodumu ndani Yake, basi wokovu utaendelea milele. Hata hivyo, huo utaingia kwenye nyanja mpya kabisa baada ya Yesu kuja mara ya pili.

## Utii wa kibiblia

Utii wa kibiblia haupaswi kuhusiana na ama hidaya au haki kwa matendo. Ni matokeo ya kimantiki ya hatua yangu

107 Dennis Smith, 40 Days: Prayers and Devotions to Revive Your Experience With God, book 2 (Hagerstown, MD: Review and Herald Publishing Association, 2011), uk. 35.

108 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 43, 44.

ya kumtumaini Mungu, kujisalimisha kwangu, na uhusiano wangu na Kristo. Utii wa Kibiblia kwa Mkristo aliyezaliwa upya, yule aliyejazwa Roho Mtakatifu, si lingine isipokuwa upendo kwa Mungu unaooneshwa katika matendo. Utii kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu huleta furaha na raha:

"Utii wote wa kweli hutokea moyoni. Ilikuwa kazi ya moyoni kwa Kristo. Na kama tukiridhia, atajinasibisha kwa dhati kwenye mawazo na makusudi yetu, atafungamanisha kwa kina mioyo na nia zetu katika kuyatii mapenzi Yake, kiasi kwamba wakati wa kumtii Yeye tutakuwa tukitekeleza misukumo yetu wenyewe. Nia, ikisafishwa na kutakaswa, itapata furaha yake kuu zaidi katika kutekeleza huduma Yake."[109]

Inapaswa kuwa bayana kwetu kwamba hatuwezi kuwa watii kwa juhudi zetu wenyewe. Bwana anatuambia kuhusu watu wa Israeli: "Hawakuwa na dhana halisi ya utakatifu wa Mungu, ya hali ya dhambi iliyokithiri mioyoni mwao, kutoweza kabisa, kwa nafsi zao wenyewe, kutii sheria ya Mungu."[110]

Hatuwezi kushika amri za Mungu kwa uwezo wetu wenyewe. Siri ya utii ni Yesu ndani yetu kupitia ujazo wa Roho Mtakatifu. Kama kweli tunampenda na kumtumaini Yesu, kama akiishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, basi utii huleta furaha. Yesu anapoishi ndani yetu, ndipo hutuhakikishia kwamba tunayo sheria Yake mioyoni mwetu. Sheria hii ni sheria ya uhuru, Amri Kumi (Yak. 2:12).

---

109 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 668.

110 Ellen G. White, Patriarchs and Prophets (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2005), uk. 371.

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Nini maana ya utii wenye uaminifu na unachukuliwaje ?*

2. *Jinsi gani na wakati gani naokolewa? Je wokovu huu hauwezi kubadilika tena?*

3. *Nini matokeo ya asili ya imani ya kibilia kuhusu mambo tuyafanyayo au tusiyoyafanya?*

4. *Je Mungu hutegemea kitu fulani kutoka kwetu? Matendo yana kazi gani kuhusiana na wokovu?*

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*

  1. *Kwa ajili ya uelewa wa kina zaidi wa wokovu na utii.*
  2. *Kwa ajili ya furaha itokanayo na uhusiano wetu pamoja na Mungu.*
  3. *Kwa ajili ya uhakikisho wa wokovu kwenye Biblia.*
  4. *Kwa ajili ya upendo kwa Mungu unaooneshwa kwa matendo.*
  5. *Kwa ajili ya uelewa sahihi wa upendo na utakatifu wa Mungu.*

Siku ya Nane

# Jinsi gani utii kupitia “Yesu ndani yangu” hutenda kazi? Mungu amekusudia: Ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu

**Muujiza wa utii harusini**

Sote tunajua kisa cha harusi huko Kana, ambapo Yesu alitenda muujiza Wake wa kwanza. Aligeuza maji kuwa divai, divai isiyochachushwa, ambayo tungeiita juisi ya zabibu. Nini kilitokea hapo?

Mariamu, mama yake Yesu, alisikia hapakuwepo tena na divai halafu akamwarifu Yesu. Lakini Yesu hakutenda kama mama Yake alivyokuwa ametarajia. Hata hivyo, alikisia kwamba kwa namna fulani Yesu angenusuru hali hii, sababu aliwaambia watumishi: *“Lolote atakalowaambia [Yesu], fanyeni.”* (Yohana 2:5) Hivyo, Mariamu alijenga imani ya watumishi kwa Yesu.

Hatimaye Yesu aliposema: “Jalizeni mabalasi maji,” waliamua kufanya hivyo hasa. Kisha akasema: *“Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza,”* nao wakafanya hivyo (aya ya 7, 8).

Tunataka kusisitiza yafuatayo: Kwa vile watumishi hawa walikuwa na imani juu ya Yesu, waliamua kutii maagizo Yake kwa hiari. Kwa maneno mengine, utayari na uamuzi wao vilikuwa hatua dhahiri kuelekea kwenye utii—kwa kufanya kile Yesu alichowaamuru. Kupitia utii wao, Yesu aligeuza maji kuwa kinywaji kitamu. Alitenda muujiza Wake wa kwanza.

**Je hatua husika zilikuwa zipi?**

- ▶ Kwa maagizo yake, Mariamu alijenga tumaini la watumishi hao kwa Yesu.
- ▶ Watumishi walionesha tumaini na utayari wao kwa kufanya kile Yesu alichosema.
- ▶ Si Mariamu wala watumishi hao walihusika katika kitendo hasa cha kugeuza maji kuwa divai. Yesu pekee ndiye alitenda muujiza huu.

Lakini hivi muujiza huu ungekuwa umetokea bila hatua hizi za maandalizi? Ni muhimu kwamba tumtumaini Yesu, kwamba tuweke utashi na chaguzi zetu chini Yake na kulieleza hili kwa hatua za utii. Kwa kufanya hivyo, Yesu—na Yesu pekee—atatenda muujiza huu. Yeye pekee ndiye pia atendaye muujiza wa utii ndani yetu. Hivi ndiyo utii wa imani utendavyo kazi. Yesu amefanywa kuwa hekima, haki, utakaso, na ukombozi kwa ajili yetu (1 Kor. 1:30). Uamuzi wetu wa kuyakubali mapenzi Yake na hatua zetu za maandalizi ili kutii ni vifungua-mlango kwa ajili ya utii, ambao Yesu hutenda maishani mwetu.

### Ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu

Ellen White anaeleza jinsi ambavyo hatua za utii zilitenda kazi maishani mwa Danieli: Wakati Mungu alikuwa akitenda kazi ndani ya Danieli na wenzake ili "kutaka na kutenda mapenzi Yake mema," wao walikuwa wakitimiza wokovu wao wenyewe (Wafilipi 2:13). Hapa panadhihirishwa utendaji wa kanuni ya kiungu ya ushirikiano, ambao pasipo huu hakuna mafanikio ya kweli yanayoweza kupatikana. Juhudi za mwanadamu hazifai chochote bila nguvu ya kiungu; na bila bidii ya mwanadamu, juhudi ya kiungu kwa wengi hazina manufaa. Ili kuifanya neema ya Mungu iwe yetu, lazima tutende sehemu yetu. Neema Yake imekirimiwa kwetu ili kuleta ndani yetu nia na kutenda, na wala siyo mbadala wa juhudi zetu. …

… Na kwa ukirimiwaji wa Roho Wake, ataimarisha kila kusudi la kweli, kila uamuzi adilifu. Wale waenendao katika njia ya utii watakabiliana na vikwazo vingi. … Katika nguvu Yake wanaweza kushinda kila jaribu, wakashinda kila tatizo gumu.[111]

"Bwana anakusudia kwamba nguvu ya kiungu itashirikiana na juhudi ya kibinadamu."[112] Mark Finley aliandika, "Kutenda kazi pamoja na Mungu huleta furaha maridhawa na utimilifu mkuu."

Ni sehemu gani tunayofanya? Yesu anafanya sehemu gani ndani yetu?

1. Tunaamua kujenga tumaini letu katika Yesu, ambaye huibua ndani yetu nia na utendaji. Hujenga ndani yetu angahewa la utayari, nasi tutajua tupaswacho kutenda. Lakini hungojea uamuzi wetu.
2. Ni wajibu wetu kuamua kufanya mapenzi ya Mungu. Kwa vile Mungu huheshimu kabisa silika na utashi wetu, anaweza na ataingilia kati tu baada ya kuwa tumefanya uamuzi wetu. Analingojea hilo.
3. Ni wajibu wetu kufanya uamuzi wetu uwe dhahiri ili kumtumaini Yesu na kuubainisha katika hatua zetu za utii. Hatua hizi za utii huweza kutofautiana sana kwa uzito.

Mungu hufanya sehemu ya msingi peke yake, na pia hutusaidia katika kujenga tumaini na maandalizi. Lakini hatupaswi kusahau kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kujaribu kufanya uamuzi na hatua za utii katika nguvu zetu wenyewe au endapo tukiufanya kwa uwezo wa Mungu. Sehemu yetu hufanywa kwa nguvu ya Mungu, Yesu anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Hili hufanya utii uwe furaha, ama katika mambo madogo au mambo makubwa.[113]

## Maswali

Yapo mawazo kinzani kuhusu nani anayefanya utii uwezekane. Baadhi hudumisha mtazamo kwamba utii ni

111 Ellen G. White, Prophets and Kings, uk. 486, 487.

112 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, January 2, uk. 10.

113 Mark Finley, Decisions: Persuading People for Christ (Silver Spring, MD: General Conference of Seventh-day Adventists, 1984).

matokeo ya ushirikiano wa uungu na ubinadamu. Wengine wanasema kwamba Mungu au Kristo hulifanya hilo peke yake. Sasa linafanyikaje?

Katika wakati wa Yesu, watu wengi waliamini kwamba ilitosha tu kuuamini ukweli. Katika The Desires of Ages, tunasoma: "Udanganyifu mkuu zaidi akilini mwa mwanadamu katika siku za Kristo ulikuwa kwamba kuridhia ukweli tu kuliunda haki."[114]

Mungu hatarajii kwamba tustahimili mapenzi Yake pasipo kufanya lolote, bali anatarajia tuitikie kwayo, tuwe waitikiaji. Hii humaanisha kwamba Kristo akiwa mioyoni mwetu, tunafanya uamuzi chanya na kuutekeleza kwa vitendo. "Mwanadamu ameteuliwa ili kuvaa silaha, kupigana vita vizuri vya imani. Ameteuliwa ili atumie nyenzo ambazo Mungu ameweka kwenye himaya yake. … Ameteuliwa ili awe na imani daima."[115] "Hebu mwanadamu yeyote asiwasilishe dhana kwamba mwanadamu ana wajibu mdogo wa kufanya au hana kabisa katika kazi kuu ya kushinda; kwa vile Mungu hamfanyii mwanadamu lolote bila ushirikiano wake. … Tangu mwanzo hadi mwisho, mwanadamu anapaswa kuwa mtendakazi pamoja na Mungu. … Ushirikiano pamoja na Kristo humaanisha ushindi. …

"Kamwe usiache dhana mawazoni kwamba kuna wajibu mdogo wa kufanya au hakuna kabisa kwa upande wa mwanadamu; lakini badala yake mfundishe mwanadamu ashirikiane na Mungu, ili aweze kufanikiwa katika kushinda."[116]

Tunapoitambua kazi ya uamuzi wetu na hatua za maandalizi, basi ni bayana kwamba huu ni ushirikiano kati ya uungu na ubinadamu, japo hatua za maandalizi pia hufanywa kwa uwezo wa Mungu wakati Kristo akiwa ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu.

---

114 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 309.

115 Ellen G. White, Testimonies to Ministers and Gospel Workers (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2003), uk. 454.

116 Ellen G. White, A New Life (Revival and Beyond) (Payson, AZ: Leaves-of-Autumn Books, 1972), uk. 38, 39.

Kadiri nifahamuvyo, huu ni mtazamo sahihi, kwa vile Mungu anamheshimu mwanadamu kabisa na wala hafanyi lolote bila ridhaa yake. Mwanadamu anaonesha ridhaa hii kupitia hatua za utii. Ni wazi kwamba Mungu hufanya sehemu ya msingi sana. Tunahitaji kuona awamu zote za mchakato huo na halafu tuwaone wale wahusikao—Mungu na mwanadamu—wakitenda kazi pamoja.

Tunapata mfano mzuri wa ushirikiano kati ya uungu na ubinadamu kwenye vita kati ya Israeli na Waamaleki pale jangwani (angalia Kut. 17:8–16). Yoshua alipambana akiwa na askari wake, lakini walikuwa washindi kwa sababu Musa aliomba, akitegemezwa na Haruni na Huri.

## Ukubwa mbalimbali wa hatua za utii
## Mariamu, mama yake Yesu

Wakati malaika Gabrieli alipotangaza kuzaliwa kwa Yesu kwa Mariamu, mama huyu angeweza tu kueleza kuridhia kwake mapenzi ya Mungu. Alisema: "Mariamu akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema. Kisha malaika akaondoka akaenda zake." (Luka 1:38) Zaidi ya hilo, hakuna linginelo ambalo angeweza kufanya isipokuwa kungoja utendaji wa Mungu. Katika wakati huo, angeweza tu kuelezea utayari wake au kutoridhia. Ukubali huu wa mapenzi ya Mungu ulileta mabadiliko makubwa maishani mwake, na, kwa mtazamo wa kibinadamu, ilikuwa hatari kubwa. Kama tuonavyo, Mariamu aliishi katika hali ya kujitoa kikamilifu.

## Wakoma kumi

Wakoma waliokuja kwa Yesu walipaza sauti wakisema, *"Ee Yesu, Bwana mkubwa, uturehemu!" Yesu aliona imani yao, akawajibu, "Enendeni, mkajioneshe* kwa makuhani. Ikawa walipokuwa wakienda walitakasika." (Luka 17:13, 14)

Watu hawa walidhihirisha tumaini lao na uamuzi wao kwa kuondoka mara hiyo. Yesu hakwenda kwa ajili yao/badala yao. Je waliponywa kwa kuondoka kwao? La hasha! Waliponywa kwa sababu Yesu alifanya hivyo kutokana na utii wao wenye tumaini. Hawakuwa na sehemu yoyote

katika urejeshwaji wao halisi. Hata hivyo, tumaini lao na udhihirishaji wa tumaini lao kupitia hatua za utii vilifungua mlango kwa ajili ya muujiza ambao Yesu aliwatendea. Yesu pekee ndiye alitenda muujiza huo.

## Uponywaji wa Naamani

Je unakumbuka jinsi Naamani alivyoponywa ukoma? Maagizo ya Mungu kupitia Elisha yalikuwa kama ifuatavyo: *"Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi."* (2 Falm. 5:10) Naamani alikasirika kuhusiana na amri hii. Ni hadi pale alipokuwa ameshawishiwa na watumishi wake ndipo alipokuwa na tumaini la kutosha kufanya hivyo. Mungu hakumwondolea hatua ya kwenda Yordani na kujizamisha majini. Baada ya kujizamisha majini mara ya saba, aliponywa ukoma. Je kuzama kwake mara saba ndiko kulimponya? Hapana! Hatua za utii alizofanya kama matokeo ya imani yake ndogo, zilikuwa hatua zilizoachilia uponyaji wa Mungu. Tunaona tena kwamba imani ndogo kwa Mungu na hatua za utii zilisababisha muujiza wa Mungu. Naamani hakuwa na sehemu yoyote katika muujiza huo. Lakini bila hatua zake za maandalizi, hakuna chochote ambacho kingetokea.

## Rudi na Marie Ana Hirschmann

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, wanandoa wachanga ambao ndio tu walikuwa wamebatizwa katika Kanisa la Waadventista walikuwa wakiishi kwenye mji mdogo karibu na Bad Aibling, Ujerumani. Marie Ana alikuwa akitarajia mtoto wao wa kwanza na hivyo alilazimika kuiacha kazi yake kama mwalimu kwa sababu za kiafya.

Katika kujitafutia kazi, Rudi alienda Munich kila siku kwa majuma kadhaa bila kukoma, bila mafanikio. Akiba yao ikayoyoma hadi wakabakiwa na Maki sita (fedha za Kijerumani wakati huo). Pamoja na hilo, walikuwa na bahasha yenye fedha iliyokuwa mali ya Mungu. Ilikuwa fedha yao ya zaka, waliyokuwa wameitenga. Wangefanya nini?

Maria Ana alisema, “Rudi, fedha yetu itakapokuwa imeisha yote tutajaribiwa kutumia fedha za Mungu. Hivyo ingelikuwa bora tusiihifadhi hapa nyumbani. Utakapopanda treni kwenda Munich kesho, ondoka na fedha hizi kampelekee mhazini wa konferensi.”

Hivyo ndivyo alivyofanya Rudi. Alimpelekea mhazini fedha hizo. Alimuuliza Rudi jinsi walivyokuwa wakiendelea, naye akaelezea hali husika.

“Ngoja kidogo,” alisema kisha akapiga simu. Baada ya hapo akasema, “Nadhani tumepata kazi kwa ajili yako. Nenda kwenye maskani haya/eneo hili ukamuulizie Bw. Bauer.”

Nusu saa baadaye Rudi akaajiriwa. Familia ya Hirschmann ilikuwa imelipa zaka yao japo walikuwa na hali ngumu kiuchumi. Walionesha imani yao kwa kupiga hatua ya utii, Naye Mungu akaingilia kati wakati huohuo.[117]

**Kampuni ya utalii kwenye kisiwa cha Guam**

Wanandoa waliokuwa wakimiliki kampuni kubwa ya utalii kwenye kisiwa cha Guam waliongoka kuwa Wakristo. Mke alibatizwa kwanza kisha akafuatia mume mnamo Januari mwaka 2004. Walijiandaa kwa uadhimishaji Sabato kwa maombi ya kina sana kwenye kampuni yao. Walisitisha huduma zao zote hotelini siku ya Sabato. Mume alieleza sababu za hatua hizi kwa mawakala wa usafirishaji, hoteli, na mawakala wa mauzo walionufaika kwa huduma zao za utalii. Wengi miongoni mwa wateja walijibu kwamba wangepaswa kuzipatia kampuni zingine biashara yao, suala lililozua ushindani kwa wanandoa hawa. Waajiriwa wa bwana huyo waliogopa kwamba wangepoteza kazi zao. Uamuzi huu ulionekana kama hukumu ya kifo dhidi ya kampuni hiyo. Lakini sikiliza kile asemacho ndugu yetu: “Ningali naikumbuka Sabato ya kwanza tulipofunga. Siku ya Ijumaa jioni, tuliwasha mashine ya kujibia simu zinazoingia kuweka nafasi ya vyumba hotelini. Katika Jumamosi ya kwanza, tulifunga. Hali ya hewa

117 Maria Ana Hirschmann, I Changed Gods (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 1968), uk. 156.

ilibadilika ghafla, na mvua ikanyesha kwa wingi sana siku nzima. Wakati wa jioni tuligundua kwamba mashine ya kujibia ilikuwa imejaa nafasi kwa ajili ya Jumapili. Katika kipindi kilichofuata cha zaidi ya miezi sita, hali ya hewa ilidumisha mfumo huo: hali nzuri ya hewa Ijumaa, mvua nyingi sana siku ya Sabato, na hali nzuri ya hewa Jumapili. Mungu alitukimu."[118]

Sehemu ya wajibu wa wanandoa hawa kwenye muujiza huu ilikuwa kumtumaini Mungu na kuchukua hatua za maandalizi. Muujiza uliofuata ungeweza tu kutendwa na Mungu.

Hebu tukumbuke hili: "Kadiri utashi wa mwanadamu unavyoshirikiana na utashi wa Mungu, huwa wenye kudura (uwezo wa Mungu). Lolote linalopaswa kufanywa kwa amri Yake, huweza kutekelezwa katika uwezo Wake. Maagizo Yake yote ni wezeshi."[119] Mungu ameweka baraka kuu kwenye utii wa imani—kuishi kwa kufuata tumaini letu kwa Mungu na kujisalimisha kwake.

### Kwa nini utii ni kwa ajili ya manufaa yetu?

Mungu aliuunda kiasi kwamba utii uwe njia bora iwezekanayo kwetu. Yeremia 7:23 inasema, *"Sikilizeni sauti Yangu; Nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu Wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru **mpate kufanikiwa**."* Daktari yeyote wa utabibu angeweza kuthibitisha kwamba dawa inaweza tu kuponya kama ikitumiwa kwa uangalifu. Hii humaanisha kwamba lazima tufuate maelekezo ya daktari kama tunataka kuponywa. Tabibu bora kabisa hawezi kuponya endapo maelekezo hayafuatwi kwa usahihi. Utii siyo tu matokeo ya kimantiki ya tumaini na kujisalimisha kwetu, bali pia utii ni kwa ajili ya manufaa yetu bora, maana amri zote za Mungu ziliwasilishwa kwa ajili ya faida yetu.

Nini kilichotokea kuhusu nyoka wa shaba pale jangwani (angalia Hes. 21:4–9)? Watu hao walipomtazama nyoka kama ambavyo Mungu aliamuru, waliponywa. Je kugeuza vichwa

---

118 Steve Kasperbauer, Gott ist treu (Braunau/Austria: Copyright Brigitte Kinder, 2013). A full report about this experience is published in German in the MISSIONSBRIEF (mission letter) No. 40, Machi/Aprili 2014.

119 Ellen G. White, Christ's Object Lessons, uk. 333.

vyao kulisababisha uponyaji? La hasha. Waliponywa kwa sababu walionesha imani yao kwa Mungu kwa kumtazama huyo nyoka. Mungu pekee ndiye aliyewaponya. Utii ulikuwa kwa manufaa yao.

Vilevile, *"Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake."* (Ebr. 11:7).

Uundaji wa safina ulikuwa matokeo ya tumaini la Nuhu kwa Mungu, akaonesha kwamba imani yake ilikuwa halisi. Aliwekeza mali na muda wake wote kwenye ujenzi huu, na hakika hakujutia hilo. Hivi utii wake haukuwa kwa ajili ya manufaa yake? Hakujua kabla ya hapo, lakini aliishi kwa tumaini. Jambo moja ni bayana, uundaji wa chombo hiki ulifanywa kupitia uongozi na uwezo wa Mungu.

## Mawazo ya Upande Mmoja

Kinachosikitisha, leo, maagizo ya Mungu hutazamwa katika nuru isiyo na uwiano kabisa. Sheria ya Mungu hufikiriwa tu katika muktadha wa amri za makatazo zinazopaswa kufuatwa. Hata hivyo, amri za Mungu, awali ya yote, ni ahadi kwetu. Sheria za Mungu hutuonesha kile awezacho kufanya katika maisha yetu pale tunapokuwa tumeungana Naye kwa uhusiano wa tumaini na upendo.

Amri za Mungu ni sheria za baraka. Utii ni mtazamo tu wa kifikra ambao kupitia hapo tunaweza kupata hekima na nguvu kwa ajili ya kukimu mahitaji yetu ya kila siku. Tunapotazama utii kwa namna hii, basi hofu yetu hutoweka na tunauona kama jambo la furaha.

## Utii, karama kutoka kwa Mungu

Yesu anaposababisha utii ndani yetu, basi humaanisha kwamba utii ni karama. Tunapotazama utii kama karama, hutusaidia kuepuka hatari mbili: (1) upotofu wa "neema rahisi" na (2) jaribu la ushupavu wa sheria.

"Neema rahisi" kwa kawaida humaanisha kwamba mtu anaokolewa pale wanapomkubali Yesu na anadhani hakuna utii wowote ulio muhimu. Wanasema kwamba sheria

imebatilishwa sababu tusingeweza kuishika kwa vyovyote vile. Hiki ndicho Wakristo wa mwilini waaminicho. Lakini kwa uwezo wa Mungu tunataka na tunaweza kutii.

Kwa upande mwingine, juhudi binafsi ya kuungia ufalme wa Mungu siyo tu kwamba ni mtego, bali pia—kama ikizingatiwa kwa dhati—ni mzigo mzito. Huu ni mtego wa ushupavu wa sheria.

Yesu anaposababisha utii ndani yetu kufuatana na uamuzi na shauku yetu, basi tunaona kwamba utii ni muhimu nasi tunatambua kwamba hauna sifa ya kustahili kwa wenyewe, kwa sababu ulileta kama tunu.[120]

Utii ni lazima kama matokeo, kama tunda la uhusiano wetu na Mungu na wokovu wetu, lakini siyo sharti la awali. Kila mtu anaweza kuja kwa Yesu bila masharti ya awali, kama tu vile alivyo. Lakini hakuna anayeweza kubaki kama alivyo. Hivi tungefikiri kwamba mwizi anapokuwa ameongoka—ameokolewa—anaweza kuendelea kuwanyang'anya watu?

## Kujiweka sisi pamoja na mahangaiko yetu kwenye mikono mikuu zaidi

Ni muhimu kuachilia nafsi zetu na mahangaiko yetu halafu tuvikabidhi katika uongozi wa Mungu. Hatupaswi kujiona kuwa muhimu sana kupita kiasi. Hii inahusika na kila eneo la maisha. Hatupaswi kuzuilia chochote. Je nizuilie kitu fulani wakati naweza kukiweka chote kwenye mikono mikubwa na imara zaidi—mikono ya Mungu? Hiyo itakuwa busara kweli?

Kama tunataka Bwana atuhudumie, akidhi mahitaji yetu, atulinde dhidi ya maadui, atuongoze katika njia bora, basi ni mantiki kwamba tunapaswa kuifuata sauti Yake na kuiendea njia anayotuchagulia. *"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri Yeye, Naye atayanyosha mapito yako."* (Mit. 3:5, 6)

Tunaweza kuelewa ushauri huu vema siku hizi. Madereva wengi wa magari hutumia mfumo wa uongozaji leo. Tunategemea mtazamo mpana zaidi wa mfumo husika. Lakini

120 Angalia Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Watu Wazima, Machi 31, 2011

hilo halimaanishi kwamba ufahamu wetu hauna budi kuacha kutumika. Unahitajika. Bado ni kazi yetu kuendesha. Tukiwa njiani tumeunganishwa na “kiongozi” mwenye mtazamo mpana zaidi na hutuambia mahali pa kuelekea, endapo tunapaswa kupitia njia mchepuko kwa sababu ya msongamano wa magari, au tunaendesha sana, na kadhalika. Kwa neema ya Mungu tunaweza kusonga mbele maishani tukiwa na “mfumo wa uongozaji” wa kiungu. Kwa hiyo, ni muhimu kutegemea kwa moyo wetu wote Mwongozo adhimu wa mbinguni na Mpaji wa ufahamu. Anaahidi kutuongoza kwa usahihi. Hata anadhamini hilo kwa sifa Yake. *“Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina Lake.”* (Zab. 23:3). Hapa utii pia ni kwa ajili ya maslahi yetu wenyewe.

Kwa kufuata sheria za kiungu, ama sheria za asili, au sheria za kiroho, yapo matokeo chanya kwa ajili ya kila mtu. Hata wasio waumini wanaweza kupata matokeo chanya kama wakifuata sheria hizi za kiungu. Naita hii baraka asilia. Lakini mengi zaidi hutokea, hata miujiza, pale sheria za kiroho zinapofuatwa. Naita hii baraka isiyo ya kawaida.

Tumaini na utii hushamirishana. Katika Yakobo 2:22, tunasoma: *“Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale?”* Tumaini katika Mungu hukuza utii, na utii hukuza tumaini letu kwa Mungu.

Ningependa kurudia nukuu makini kutoka kwa Dennis Smith: “Mtu fulani anapoishi katika uhusiano wa karibu pamoja na Mungu kupitia Roho Mtakatifu, basi utii huja kwa asili na hutokea moyoni, bila kufikiria sana.”[121]

Tunapoelewa utii kwa usahihi, basi tutaelewa vema zaidi kauli adhimu katika Zaburi (hususan Zab. 19 na 119) kuhusu sheria ya Mungu. Zinaonesha kwamba wokovu, ukombozi, na sheria vinahusiana pamoja. Mtu aliyeokolewa ataipenda sheria ya Mungu na, kupitia maisha yake katika Roho Mtakatifu na pamoja na Yesu moyoni mwake, atakuwa mtiifu na mwenye furaha. Naamini kwamba Mkristo wa mwilini hawezi kuelewa

---

121 Dennis Smith, 40 Days – Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming (R&H 2009) uk. 21, 22

kauli mbalimbali katika Zaburi 119. Pengine atazifikiria kuwa ukuzaji wa jambo. Kwa upande mwingine, Mkristo wa kiroho anaweza kukubaliana na kile ambacho mtunzi wa Zaburi aliandika.

Mungu ametuambia: "Kadiri tuenendavyo siku kwa siku katika nuru anayotuletea, katika utii wa hiari kwa maagizo Yake yote, uzoefu wetu hukua na kutanuka hadi tunapofikia kimo timilifu cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu."[122]

### Ni utii kiasi gani anaotegemea Mungu?

Ni utii kiasi gani ambao Yesu anataka kuufanikisha ndani yangu? Kiasi kidogo, kiasi kikubwa, au timilifu?

Mfano bayana huonekana katika maisha ya Musa katika Kutoka 4:24–26. Akiwa kwenye jangwa la Midiani, Musa alitumwa kuwaongoza watu wa Israeli watoke Misri. "Akiwa njiani kutoka Midiani [kwenda Misri], Musa alipokea onyo la kushtua na kutisha juu ya kuchukizwa kwa Bwana. Malaika alimtokea kwa namna ya kuogofya, kana kwamba angemwangamiza mara hiyo. Hakuna maelezo yaliyowasilishwa; lakini Musa alikumbuka kwamba alikuwa amepuuza mojawapo ya maagizo ya Mungu; kwa kuukubali ushawishi wa mkewe, alikuwa amepuuza kutekeleza kaida ya tohara kwa mwanawe mdogo." Mvulana huyo alifanyiwa tohara mara hiyo. "… Ndipo malaika akamruhusu Musa aendelee na safari yake. Katika utume kwa Farao, Musa angewekwa mahali penye hatari kubwa; maisha yake yangehifadhiwa tu kupitia ulinzi wa malaika watakatifu. Lakini endapo angeishi kwa kupuuza wajibu unaojulikana, asingekuwa salama; maana asingekingwa na malaika wa Mungu."[123]

Somo la kujitwalia kutokana na kisa hiki huweza kupatikana vilevile katika Wazee na Manabii: "Katika wakati wa taabu mara tu kabla ya ujio wa Kristo, wenye haki watahifadhiwa kupitia huduma ya malaika wa mbinguni; lakini hautakuwepo usalama kwa mwasi wa sheria ya Mungu. Ndipo malaika

122 Ellen G. White, Messages to Young People, uk. 15, 16.
123 Ellen G. White, Patriarchs and Prophets, uk. 255, 256.

hawatawahifadhi wale wanaopuuza mojawapo ya maagizo ya kiungu."[124]

Uadhimishaji wa amri zote za Mungu ni kwa ajili ya ulinzi wetu, furaha yetu, na ustawi wetu. tunajua kwamba Adamu na Hawa walilazimika kuondoka Edeni kwa sababu moja tu. Nadhani hili ni jibu dhahiri la swali linalohusu kiasi gani cha utii anachotegemea Mungu kutoka kwetu. Inaeleweka kwamba Mungu anategemea utii katika mambo yote, tunapodumisha akilini kwamba Yesu anatimiza utii huu ndani yetu, na ni kwa ajili ya manufaa yetu. Yesu anataka kutimiza mapenzi ya Mungu ndani yetu, kama tu alivyofanya akiwa mwanadamu hapa duniani. Mwenendo Wake kama mwanadamu ulikuwa: "Kuyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; naam, sheria Yako imo moyoni mwangu." (Zab. 40:8) Aliwaambia wanafunzi Wake, "Kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu." (Yohana 15:10)

Aidha, kama utii kamili huleta furaha kamili na uzima tele hapa duniani na umilele, basi ni wazi kwamba utii pungufu humaanisha kupoteza baraka. Yeyote aliyemo na atakayekuja kuuingia ufalme wa Mungu atamtii Mungu kwa furaha. Hii huhakikisha upendo na upatanifu kwa viumbe wote.

### Dondoo za Mwisho

Yeremia 7:23 anafupisha mada hii yote. Maneno haya waliambiwa Israeli wakati wakiondoka Misri. *"Sikilizeni sauti Yangu; Nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu Wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa."*

Hapa Bwana ametukirimia ahadi ya thamani sana. Nini anachoahidi kama tukilitii Neno Lake? *"Nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu Wangu."* Lakini anaongeza kwamba lazima tuipite njia nzima kwa ajili ya ustawi wetu wenyewe. Tunaweza kutumia andiko hili kama ahadi katika maombi kwa ajili ya moyo wenye utii.

124 Ibid., uk. 256.

### Nini kilimpata mtume Yohana?

Tunaweza kuyaona matokeo adhimu ya utii wa imani katika maisha ya Yohana, mwanafunzi wa Yesu. Katika Njia Salama, tunasoma: "Siku kwa siku moyo wake ulielekezwa kwa Kristo, hadi alipoacha ubinafsi kwa kumpenda Bwana wake. Hulka yake ya ghadhabu na tamaa ya makuu ilisalimishwa chini ya nguvu ya Kristo iumbayo. Ushawishi wa Roho Mtakatifu uongoao uliufanya upya moyo wake. Nguvu ya upendo wa Kristo ilileta badiliko la tabia. Haya ni matokeo ya hakika ya muungano na Yesu. Kristo anapokaa moyoni, asili yote hubadilishwa. Roho wa Kristo, upendo Wake, hulainisha moyo, hutiisha nafsi, na kuinua mawazo na shauku zielekee kwa Mungu na mbinguni."[125]

"Bwana amekusudia kwamba kila nafsi inayotii neno Lake itapata furaha Yake, amani Yake, nguvu Yake endelevu ya ulinzi."[126] Ni shauku na ombi langu kwamba waumini wote wastahimili ili kupata furaha kuu ya utii wa imani. Hebu Mungu atukirimie ushindi mkuu katika utii wa imani kupitia Yesu Kristo na Roho Mtakatifu. *"Yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele."* (1 Yohana 2:17)

*"Bali fadhili za Bwana zina wamchao tangu milele hata milele, Na haki Yake ina wana wa wana; Maana, wale walishikao agano Lake, na kuyakumbuka maagizo Yake ili wayafanye."* (Zab. 103:17, 18)

Tunataka kusikia kuhusu hatua kuu ya utii.

### Roho Mtakatifu amshawishi mwenye hatia aliyetoroka ili arejee gerezani.

Nilizaliwa katika familia ya Kiadventista. Nikiwa na umri wa miaka 19, nilibatizwa. Mnamo mwaka 2016, nilihukumiwa kifungo cha miaka 43 gerezani kwa hatia ya mauaji. Huu ni mwaka wangu wa tano gerezani sasa. Niliweza kutoroka gerezani mnamo mwezi Machi 2017. Baada ya Sabato ya

---

125 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 73.

126 Ellen G. White, In Heavenly Places (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 1999), uk. 53.

kwanza, nilikutana na mwanamke mmoja aliyenionesha kitabu “Hatua za Uamsho Binafsi.” Siku ya Jumatatu baada ya hapo, nilikinunua kitabu hicho kwenye duka la vitabu la Waadventista. Kwa mshangao wangu, nilikisoma chote juma hilohilo. Niliweza kugundua utupu ndani ya moyo wangu, ambao nimekuwa nao maisha yangu yote—bila Roho Mtakatifu. Ndipo nikayatoa wakfu maisha yangu yote kwa Yesu. Nilirejea gerezani mnamo mwezi Oktoba 2018. Sikushtakiwa kwa kosa langu la kutoroka. Na bora zaidi, hukumu yangu sasa inafanyika mbele ya Mungu Mwenyezi. Nimekata rufaa kwenye Mahakama Kuu. Baada ya kukisoma kitabu hiki, nilibarikiwa sana kiasi kwamba nimeshawishika kwa kina: “Hakuna hali zisizokuwa na tumaini kwa Mungu! Sasa mimi ni kiongozi wa huduma ya maombi. Kijitabu hiki kiligawiwa kwa wafungwa hapa kwenye Gereza la Barawagi. Wafungwa wengi waliguswa na kijitabu hiki baada ya kukisoma. Nafurahi kwamba naweza kumtumikia Bwana na Mwokozi wangu Yesu Kristo. Kilikuwa na bado kingali baraka halisi kwetu.”[127]

**Sala:** “Baba, asante kwamba katika hekima Yako isiyo na kikomo, nguvu kuu ajabu na upendo mtukufu, umetupatia uongozi kamili ili kupata maisha maridhawa kadiri iwezekanavyo. Uliumba kila kitu kwa manufaa yetu bora. Nataka kukusifu na kukushukuru kwa ajili ya hili. Tafadhali, nipatie moyo wa tumaini kamili katika njia Zako, halafu nisaidie nikufuate katika mambo yote kwa moyo wangu wote katika kujisalimisha na utii.” Amina.

127 E. E. EE260419 Dhahama # 91 kwenye www.steps-to-personal-revival.info - Dhahama Mbalimbali

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Sehemu yetu ni nini katika kazi ya kiungu ifanywayo ndani yetu, pamoja na matendo yetu?*

 ____________________________________________

2. *Nini tofauti kati ya imani na kuuafiki tu ukweli?*

 ____________________________________________

 ____________________________________________

3. *Ni wakati gani kuuafiki ukweli ni muhimu kwetu?*

 ____________________________________________

 ____________________________________________

4. *Kwa nini utii ni baraka kuu kwetu?*

 ____________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*

 1. *Kutambua zaidi kazi yetu katika utendaji wa kiungu.*
 2. *Kwa ajili ya uwezo wa kutambua mahali palipo na imani ya kweli au kuiafiki tu maishani mwetu.*
 3. *Kwa ajili ya utii wenye uaminifu na baraka zinazoambatana nayo.*
 4. *Kwa ajili ya tumaini kamili katika uongozi wa Mungu na kanuni Zake.*

Siku ya Tisa

SURA YA 5

# Imani Yenye Mvuto Kupitia Yesu

*Jinsi gani umoja unaweza kupatikana miongoni mwa waumini?*
*Nini kinachofanya imani yetu ivutie kwa familia yetu na ulimwengu?*
*Mabadiliko gani ndani yetu hutufanya mashahidi?*
*Jinsi gani uamsho huanzisha utume?*

Mwanamaombi mwenzangu kutoka katika muda wa maombi wa siku arobaini aliwahi kusema: “Nina shauku ya kupata imani inayovutia ili watoto wangu nao waje kumfuata Kristo.”

Mary Jones, binti kutoka Wales, alikuwa anaweza kwenda mara moja kwa juma katika familia ya mbali ili kusoma Biblia yao. Hii ilifanyika kuanzia umri wa miaka kumi hadi kumi na tano. Aliipenda Biblia kwa moyo wake wote. Alifanya kazi nyingi za ziada ili kujipatia fedha za kununulia Biblia yake. Kwa miaka sita alitunza kila senti aliyoipata.

Alipokaribia umri wa miaka kumi na sita, Mary alitembea peku maili ishirini na tano ili kumwona mchungaji ambaye alitaka kununua Biblia kwake. Alisema kwamba bado alikuwa na Biblia mbili, lakini tayari zilikuwa zimeahidiwa kwa watu wengine. Mary akaanza kulia kwa uchungu. Mchungaji akamuuliza sababu ya kulia. Hivyo akamwambia jinsi alivyokuwa ametunza fedha kwa miaka sita ili kununulia Biblia. Mchungaji hakuwa tena na moyo wa kukataa, akamruhusu achukue Biblia. Akiwa na furaha tele, aliondoka kwenda nyumbani.

Je Biblia ilikuwa na mvuto kwake? Je imani ilikuwa na mvuto kwa binti huyu? Halafu, hili lilifanyika mnamo mwaka

1800. Uzoefu huu ulimgusa sana mchungaji kiasi kwamba alichukua hatua za kuanzisha jumuia ya kwanza ya Biblia ulimwenguni, Jumuia ya Biblia ya Uingereza na Ughaibuni. Baadaye, jumuia za Biblia zingine nyingi zilianzishwa.

Haya yote ni kwa vile binti mdogo aliipenda Biblia sana kiasi kwamba alitoa maisha yake ili aipate moja. Imani inayovutia ina matokeo maridhawa.[128]

## Maana ya "kuvutia"

Kamusi zinafasili kuvutia kama kivutiacho, kipendezeshacho, kivutiacho sana, kitamanishacho. Nani asiyetaka kuwa na imani kama hiyo? Naamini kuwa yeyote anayefikiria hasa jambo hilo ana shauku ya kupata imani vutivu, inayopendezesha .

## Jinsi gani naweza kupata shauku ya imani hiyo? Inapaswa kuonekanaje?

- Inapaswa kutupatia msingi thabiti na wa kutumainika kwa ajili ya maisha.
- Inapaswa kujengwa katika ukweli, siyo upotofu au uongo.
- Inapaswa kujengwa katika ufunuo wa Mungu wetu atupendaye na mwenye hekima yote, isiyochanganywa na mafundisho ya kibinadamu, ili iweze kukidhi maslahi yetu bora.
- Inapaswa kushawishi kikamilifu na kuleta furaha kuu.
- Inapaswa kuleta faida mahususi kwa ajili ya maisha yetu.
- Inapaswa kuweza kunitegemeza katika mazingira magumu—katika maradhi, katika fadhaa, katika mauti.
- Inapaswa kuwasilisha tumaini la umilele.

Dondoo hizi zote zinahusiana na kile kinachotokea ndani ya maisha yetu. Lakini imani inayovutia inapaswa kuwa na ushawishi mwingine zaidi. Mwanamaombi mwenzangu

128 Imechukuliwa kutoka katika Wikipedia, "Mary Jones."

alisema, “Nina shauku ya kupata imani inayovuti ili watoto wangu nao waje kumfuata Kristo.”

- ►Imani inayovutia inapaswa kuwaongoza wapendwa wetu na watu wengine kupata shauku kwayo na watake kuwa nayo wao wenyewe.

**Nini maana ya imani inayovutia?**

Imani inayovutia ni Ukristo wa kiroho—maisha pamoja na Yesu Kristo ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Tunapaswa kudumisha akilini ibara ya Biblia ifuatayo: *“Kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani; kwamba ninyi ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo… ili mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu.”* (Efe. 3:16, 17, 19)

Aya hizi zinasema kwamba Roho wa Mungu hutuimarisha na hivyo Kristo huishi ndani yetu Naye anafunua asili Yake ya upendo ndani yetu. Hii hutuweka huru kutoka kwenye utumwa wa nafsi. Tunapata uhuru mtukufu wa kuwa watoto wa Mungu.

Yesu anasema: *“Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi.”* (Yohana 14:6) Yesu anapokuwa moyoni mwangu kupitia Roho Mtakatifu, basi pia anakuwa njia yangu ya kwenda kwa Baba, kiongozi wangu wa kuujua ukweli. Yeye ndiye namna ya kufikia maisha ya kiwango cha juu kabisa.

**Jinsi gani Yesu anaelezea imani inayovutia?**

Yesu alizungumzia utimilifu asioweza kutupatia mtu yeyote. Ni amani makini ya ndani na furaha ya kweli, sababu Mungu wa upendo na amani ameruhusiwa kuishi moyoni. Hali hii haitegemei mazingira ya nje; hata hivyo, hutegemea tumaini na imani kama ya mtoto mdogo katika uwezo wa Mungu. Paulo aliwaandikia wafuasi wa Yesu: *“ili mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu.”* (Efe. 3:19b)

Yesu mioyoni mwetu. Hicho ndicho tunahitaji, “Maana utimilifu wote wa asili ya kiungu hukaa ndani ya Kristo, katika

ubinadamu Wake, nanyi mmepewa maisha timilifu kwa kuungana pamoja Naye" (Kol. 2:9, 10, GNT). Hiki ndicho kimo cha juu zaidi tuwezacho kufikia katika maisha haya. Ni kile ambacho Mungu anataka kutukirimia kutokana na upendo Wake mkuu.

Mwanamke katika kisima cha Yakobo alipitia uzoefu huu. Yesu alitumia mfano wa maisha ya kila siku ili kuonesha utimizwaji wa shauku hii. Zamani katika nyakati hizo, maji yalikuwa kitu cha thamani zaidi alichohitaji mtu. Kupitia Yesu tunakuja kwenye "chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele" (Yohana 4:14), jambo ambalo humaanisha kwamba tunaweza kunywa kutoka kwenye chemchemi hii na shauku yetu itatoshelezwa.

Watu wote wana shauku ya kupata furaha. Hawajui kwamba kihalisia, ni shauku ya kupata uhusiano binafsi pamoja na Mungu, sababu kwa mujibu wa Mhubiri 3:11, "[Mungu] ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao." Yeyote ambaye hajapata ushirika wa kina pamoja na Mungu ana ombwe moyoni mwake, kulingana na Blaise Pascal. Matokeo yake ni kwamba wana shauku daima ya kupata zaidi na zaidi. Yesu anatualika tuwe na imani katika Yeye, kumtumaini Yeye. Matokeo yatakuwa dhahiri kwa yule atendaye, kwa sababu "mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake" (Yohana 7:38). Wana maisha yabubujikayo baraka, haiba inayovutia, na huwa na ushawishi utakaowaimarisha wengine.

Imani inayovutia ni maisha maridhawa na timilifu katika ulimwengu huu na hata kwa kiwango kikubwa zaidi kisichofikirika katika umilele.

## Neno la Mungu huonesha kwamba imani yangu inavutia kwa wengine

Hebu tusome sala ya Yesu katika Yohana 17:20–23: *"Wala si hao tu ninaowaombea lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja kama wewe Baba, ulivyo na dani yangu nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili*

*wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi..”* (NIV)

Yesu aliomba kwamba wanafunzi Wake waweze kuwa wamoja katika vizazi vyote. Kwa namna hiyo, alikuwa pia akiniombea mimi na wewe. Siyo tu kwamba Yesu alikuwa akiombea umoja wetu, ili tujisikie vema katika uhusiano wetu na kusaidiana sisi kwa sisi, lakini pia alisema kwamba umoja wa wanafunzi hao ungekuwa wa kuvutia kwa watu ulimwenguni: *“Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.”* (Yohana 13:34, 35) Anatuonesha kwamba kwa sababu ya umoja wa wanafunzi, ulimwengu utaamini na kujua mambo haya matatu muhimu.

**Nini ambacho ulimwengu hukitambua ndani yetu?**

1. Ulimwengu unajua kwamba watu ni wanafunzi wa Yesu kwa upendo ndani ya kundi la waumini na ndani ya kanisa. Hii humaanisha kwamba ulimwengu unatutazama. Ulimwengu hutambua kwamba mwenendo wa upendo miongoni mwa wanafunzi ni matokeo ya ushirika wao pamoja na Yesu. (“Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.”)
2. Kwa sababu ya umoja miongoni mwa wanafunzi wa Yesu, ulimwengu huamini kwamba Yesu ni Balozi wa Mungu. (“Ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma.”) Watu ulimwenguni hutambua kwamba Yesu ni Mkombozi aliyetumwa na Mungu sababu ya upamoja wenye upendo wa wanafunzi Wake.
3. Kinachoshangaza, watu ulimwenguni hutambua kwamba Mungu huwapenda kwa sababu ya mwenendo wa upendo miongoni mwa wanafunzi Wake. (“Ulimwengu uweze kujua kuwa Wewe … umewapenda wao [ulimwengu] kama ambavyo umenipenda Mimi.”)

Kiufupi, kupitia umoja miongoni mwa wanafunzi wa Yesu, watu

(1) watatambua uhusiano wao kwa Yesu, (2) watatambua kwamba Yesu alitumwa na Mungu, na (3) watatambua kwamba Mungu anawapenda. Yesu atatambuliwa na ulimwengu kupitia mwenendo wa wanafunzi waliojazwa Roho kadiri wanavyohusiana wao kwa wao. Yesu anaweza kuwa na mguso huu makini kupitia Wakristo wa kiroho. Uamsho husababisha utume.

**Kwa nini inatokea kwamba watu hujifunza kitu fulani kuhusu Mungu kupitia tabia ya upendo ya wanafunzi?**

Hata hivyo, kila mtu ni tofauti. Tuna talanta na uwezo mbalimbali; wapo wanaume, wanawake, watoto na wazee. Kwa kawaida tuna misingi tofauti ya kielimu au kitamaduni. Tuna silika tofauti, mawazo na uzoefu tofauti. Katika ulimwengu, mara nyingi tofauti hizi husababisha mivuto miongoni mwa watu. Pia huweza kusababisha uhasama na ushindani. Ndiyo maana watu wanastaajabishwa na kuvutiwa na makundi ya watu ambao miongoni mwao kuna upendo, upatanifu, na hali ya kusaidiana.

Nilipokuwa mchungaji huko Munich, Ujerumani, nilimtembelea rafiki wa zamani mfanyabiashara kwenye mji mdogo wa jirani. Aliishi kwenye mtaa ambapo idadi kubwa ya jamaa wa Kiadventista waliishi pamoja katika nyumba moja. Akijua kwamba mimi ni Mwadventista, aliniambia, "Mtaa mzima unashangaa kwamba watu hawa kumi na tano au ishirini wanaweza kuishi pamoja kwenye maskani ya pamoja kwa upatanifu na bila migogoro yoyote." Majirani hao walitambua kitu fulani: hii ilikuwa imani inayovutia.

Walter Schlund, ambaye sasa ni mshiriki wa kanisa dogo huko Ujerumani, anasimulia mfano mwingine wa tukio hili la ajabu: "Kabla sijawa Mkristo, tulitaka kutembelea Romania na kuishia kwenye ukanda wa mafuriko. Bado tulikuwa na maili 75 ili kufika mwisho wa safari yetu, lakini tusingeweza kuendelea zaidi. Hivyo tuliomba uelekeo. Kwa bahati, tulizungumza na Mwadventista, aliyetuongoza kwenye familia ya Mchungaji

Biró. Familia hiyo ilitualika tukae pamoja usiku huo nyumbani hapo, jambo tulilokubali kwa shukrani. Ni wakati huu tukiwa pamoja na familia hii ndipo nilifanya uamuzi wa kusalimisha maisha yangu kwa Kristo nikawa Mwadventista. Ni namna wanafamilia walivyotendeana—maisha patanifu ya familia, amani iliyotawala, angahewa la kirafiki, ibada za familia. Nilipata uzoefu wa ubora wa maisha yaliyonigusa kwa kina. Nilitaka kuwa nayo pia."[129] Hii ilikuwa imani inayovutia.

Nakumbuka wakati nikiwa huko Regensburg, Ujerumani, kwa kipindi fulani niliwatembelea baadhi ya watu katika eneo la makazi, nikagundua makazi yao daima yalikuwa yamejawa mivutano na migogoro. Inapendeza sana unapokuwa na fursa ya kupitia uzoefu wa ziara kwa watu tofauti, ambao mioyo yao imejawa upendo.

### Kwa nini imani inayovutiai huweza kuja kutoka kwenye Neno la Mungu pekee?

Imani inayovutiaadinati imejengwa tu katika Neno la Mungu—yaani Agano la Kale na Jipya.

Yesu aliposema, "Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena" (Yohana 7:38), alimaanisha Agano la Kale, maana ndilo pekee lililokuwepo wakati huo. Katika Yohana 17:14, alibainisha dhahiri zaidi aliposema kuhusu Baba Yake: "Mimi nimewapa neno Lako." Na katika aya ya 17, anabainisha: "Uwatakase kwa ile kweli; neno Lako ndiyo kweli."

Kila dini ulimwenguni ni njia kumwendea mungu au miungu ambayo imevumbuliwa na wanadamu. Imani pekee ambayo haikuvumbuliwa na wanadamu, lakini imedhihirishwa na Mungu Mwenyewe, ni imani ya kibiblia. Kwa vile Mungu ni upendo na pia ana hekima na uwezo usio na kikomo, alianzisha kila kitu kwa ajili ya manufaa yetu makuu. Kwa hiyo, imani ya kibiblia ndiyo imani inayovutia zaidi miongoni mwa zilizopo. Kihalisia, ndiyo imani pekee inayovutia ulimwenguni. Hatuhitaji kwamba tuwe tumeelewa vizuri mafundisho ya Biblia na tuishi kwa kuyafuata kupitia Roho. Kwa mujibu wa

129 BWgung, jarida la habari la Waadventista Wasabato huko Baden-Württemberg (Ujerumani), Nr. 6/2012, S. 24.

mfano wa wanawali kumi, takriban nusu ya kanisa hawana imani hiyo.

Kupitia tumaini letu kwa Yesu, tunaweza kupata uzoefu wa furaha na amani na kupata utoshelevu wa kiu yetu ya kiroho. Mungu wetu anatamani kwamba upendo Wake uweze kuonekana kwa wengine maishani mwetu. Hilo hufanya imani yetu iwe na mvuto kwao.

**Jinsi gani umoja miongoni mwa wanafunzi unawezekana?**

Inahusu kuwa wamoja katika ndoa na familia, kanisani na katika huduma mbalimbali. Yesu anasema: "Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo umoja." (Yohana 17:22).

Nini ambacho Yesu ametupatia? Utukufu!

Hii ina maana gani? Neno "utukufu" hutumika kwa namna mbalimbali kwenye Biblia. Kwanza, hutumika kwa ajili ya uweza na ukuu wa Mungu; pili, kwa ajili ya utukufu wa uumbaji, na tatu, kwa ajili ya asili ya Mungu adhimu ya upendo. Katika hatua hii tunapaswa kutazama Kutoka 33:18, 19, ambapo Musa anamwambia Mungu, *"Nakusihi unionyeshe utukufu Wako."* Naye Bwana anajibu, *"Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako."*

Utukufu wa Mungu ni tabia Yake, ambayo hubainishwa kwa upendo na wema. Wema ni upendo unaosaidia katika utendaji. Hii hutusaidia kuelewa kauli ya Yesu kwamba ametupatia utukufu wa Mungu ili tuweze kuwa wamoja pamoja Naye. Sharti la kwanza muhimu zaidi kwa ajili ya umoja ni kupendana pamoja na heshima na tumaini. Mbinu ya Mungu ya utume ni kuwapenda wanadamu kupitia sisi, yaani upendo wa agape, upendo wa Mungu. Hii ni aina ya upendo ambao Mungu anataka kuupatia ulimwengu kupitia kwetu.

Baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, mambo makuu ajabu husimuliwa kuhusu kanisa la awali: *"Hata walipokwisha kumwomba Mungu … wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri. Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja…. Na mitume wakatoa*

*ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote.”* (Matendo 4:31–33)

### Umoja siyo ufananishaji

Umoja ni muunganiko wa nia, kusudi, na msingi. Wakati huohuo, silika ya kila mtu inadumishwa. Hauondoi silika yetu. Ni umoja wa watu tofauti wenye tabia tofauti. Na hili hasa ndilo linaloibua mshangao mkubwa: umoja wa watu tofauti.

Ellen White anasema: “Ushuhuda thabiti zaidi kwamba Mungu amemtuma Mwanawe kuja ulimwenguni ni uwepo wa upatanifu na umoja miongoni mwa watu wenye mielekeo tofauti wanaoliunda kanisa Lake. …

… Wasio waumini wanatazama ili kuona endapo imani ya wale wanaodai kuwa Wakristo inaleta mguso utakasao maishani mwao.”[130] Kwingineko anaandika: “Badiliko la tabia [kwa wanafunzi] ni ushuhuda kwa ulimwengu kuhusu Kristo akaaye ndani.”[131]

### Jinsi gani umoja unaweza kupatikana?

Umoja wa wanafunzi hupatikana kwa Kristo kuishi ndani yao kupitia Roho Mtakatifu. Yesu alisema,

Yohana 17:21: *“Hao nao wawe ndani Yetu.”*

Yohana 17:23: *“Mimi ndani yao, Nawe ndani Yangu.”*

Yohana 15:4: *“Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu.”*

Mtume Paulo huliweka namna hii,

Wakolosai 1:27: *“Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.”*

Wagalatia 2:20: *“Mimi ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu.”*

Hivyo, umoja unawezekana pale Kristo akiwa ndani yangu na ndani yako. Haiwezekani bila sisi kujazwa Roho Mtakatifu. Ndipo tu tunaweza kutendeana wema sisi kwa sisi. Ellen White

130 Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 549, 550.

131 Ellen G. White, Prophets and Kings, uk. 233.

anaandika: "Tunapaswa kutafuta kwa dhati kabisa ili kuwa na nia moja, kusudi moja. Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na wala siyo kinginecho, huweza kutuleta mahali hapa. Hebu kwa kujikana nafsi tuiandae mioyo yetu impokee Roho Mtakatifu ili kazi kuu iweze kufanywa kwa ajili yetu …"[132]

Kwingineko anaandika: "Watu wa Mungu wanapokuwa wamoja katika umoja wa Roho, Ufarisayo wote, hali zote za kujihesabia haki, zilizokuwa dhambi ya taifa la Kiyahudi, zitatoweshwa mioyoni. Uumbaji upya wa Kristo utakuwa kwa kila mshirika binafsi wa mwili Wake, na watu Wake watakuwa vyombo vipya ambamo anaweza kumiminia divai Yake mpya, divai hii mpya haitaharibu vyombo husika. Mungu atadhihirisha siri ambayo imesitirika kwa vizazi vingi. Anabainisha jinsi ulivyo 'utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu' (Kol. 1:27)."[133]

## Walipata umoja

Uzoefu wa pili tumeushuhudia kwenye jamii nyingine katika mtaa wetu. Mtangulizi wangu alisema, "Unahitaji ujasiri mwingi sana kwa ajili ya kanisa hili sababu unaenda katika mazingira hatarishi hasa!" Haraka tulitambua kwamba mivutano ilikuwa mikubwa sana. Ilikuwepo migogoro, migawanyiko, majeraha na hali za kutosamehe. Milipuko ya mihemko isiyotawalika na mashambulizi binafsi ilijaza jamii nzima kwa wingu jeusi. Ilikuwa huzuni kuona washiriki wa kanisa walionaswa kwenye mtego huu walivyokuwa katika utando wa hali ya kutosameheana na hawakutambua kwamba wasingeweza kupata ufumbuzi kwa juhudi zao wenyewe. Baada ya vikundi vya nyumba mbalimbali kuanzishwa, kijitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi kiligawanywa ili kusomwa kwenye makundi haya. Washiriki waliitikia kwa namna chanya nao walikuwa na shukrani sana kwa ajili ya kijitabu hiki.

132 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, Novemba 5; uk. 318.
133 Ellen G. White, Selected Messages, book 1, uk. 386.

Hapa pia, washiriki binafsi walianza kufunga na kuomba siku 10. (10 Days – Prayers and Devotions to Experience the Baptism of the Holy Spirit kilichoandikwa na Dennis Smith) Mwishowe, shauku ilielezwa ya kulifanya hilo pamoja kama kanisa. Mikutano ilifanyika tena saa kumi kamili alfajiri. Mwanzoni hawakuwepo washiriki wengi, lakini taratibu wengi zaidi wakajiunga ndipo likawepo angahewa adhimu, tulivu la kiroho. Mtu angeweza kutambua kwamba Mungu alikuwa akitenda kazi. Aliliandaa kanisa kimuujiza kwa ajili ya hatua ya mwisho iliyokuwa ngumu sana kwalo: hatua kwa ajili ya msamaha wa kweli. Hatimaye, ukuta ukaanguka na mtu mmoja baada ya mwingine akaomba msamaha hadharani. Wengine walikuwa wakizungumza moja kwa moja na watu fulani waliokuwa wamezozana nao huku wakiomba msamaha. Walikumbatiana. Machozi yakatiririka. Nyuso za huzuni zikawa na furaha tena halafu upendo ukarejea mioyoni mwao. Daima ni tukio la pekee ajabu kuona na kulipitia. Mungu pekee ndiye awezaye kuwaongoza watu kupitia Roho Wake Mtakatifu. Kuna tumaini kwa ajili ya maeneo hatarishi! Mchungaji F.H. na mkewe, #85b

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Je "kuvutia" humaanisha nini? Hivi imani inayovutia ni ipi?*

   ---

2. *Wapi katika Biblia tunapoweza kusoma kuhusu hii imani inayovutia?*

   ---

3. *Jinsi gani imani ya namna hii huoneshwa kivitendo maishani?*

   ---

4. *Ni mambo gani wajuayo watu wanapoona umoja miongoni mwa waumini?*

   ---

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*

  1. *Kwa ajili ya imani inayovutia, iliyo baraka kwetu na inayoweza kuwa baraka kwa wengine.*
  2. *Kwa ajili ya utambuzi wa kuona mahali ambapo hii imani inayovutia inakosekana kwenye maisha ya kila siku.*
  3. *Kwa ajili ya uongozi na nguvu ya Mungu itusaidie kuandaa nafsi? zaidi kwa ajili ya imani hii ivutiayo.*
  4. *Kwamba imani yako iwahimize wengine wawe radhi kwa ajili ya utendaji wa Mungu.*
  5. *Kwamba Kristo aishi ndani yetu na daima aendelee kuonekana zaidi.*

Siku ya Kumi

# Mabadiliko gani ndani yetu hutufanya mashahidi? Jinsi gani uamsho huanzisha utume?

## Jinsi gani Kristo anaishi ndani yangu?

Maelezo yanaweza kupatikana katika Waefeso 3:16, 17: *"Kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani; … ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo."* Kama ambavyo tumegundua hapo kabla, Kristo anaishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Kwa vile utu wetu wa ndani "unafanywa upya siku kwa siku" (2 Kor. 4:16), ni muhimu kuifanya upya hali ya kujitoa kwetu kwa Yesu kila asubuhi na kumwomba kwa imani—hususan kwa kudai ahadi kama vile Luka 11:13—ili tuweze kujazwa Roho Mtakatifu.[134] Umoja wa watu binafsi pamoja na Yesu husababisha wanafunzi wawe karibu zaidi wao kwa wao. Hivyo "kuwa kwetu ndani ya Kristo" ni msingi wa umoja.

"Huu [umoja, muungano] ni karama, ambayo waumini hupewa kwa Kristo kuishi ndani yao [Yohana 17:22, 23]. … Kwa hiyo, umoja huanza kwa kila mtu."[135]

## Ni matokeo gani yapatikanayo Yesu akikaa ndani yetu?

Kuna matokeo matatu makuu ya Yesu kuishi ndani yetu: tunda la Roho, karama za Roho, na uwezo wa kushuhudia.

Tunda na karama za Roho ni muhimu sana kwa ajili ya mafanikio ya hali ya kukaa pamoja. Halafu maeneo haya mawili yana athari kubwa kwa eneo la tatu: ushuhuda wetu kuhusu Yesu.

---

134 Luka 11:13: "Basi, Ikiwa ninyi , mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, , je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (KJV)

135 Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Watu Wazima, Novemba 21, 2012.

Badiliko letu binafsi ni sharti la awali kwa ajili ya ushuhuda wetu na umoja wetu kama wanafunzi. Mwenendo husika unaotokea hutumiwa na Bwana ili kuwavuta watu ambao hawajaokoka na ili kutuwezesha kushuhudia. Kupitia ushuhuda wetu tunakuwa watendakazi pamoja na Yesu, kwa sababu alikuja *“kutafuta na kuokoa kile kilichopotea”* (Luka 19:10).

Hebu tuangalie kwa ukaribu zaidi katika maeneo haya matatu:

1. **Tunda la Roho.** *“Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.”* (Gal. 5:22) Sifa hizi zote hutenda kazi ya msingi katika maisha ya kila siku. Ni sharti muhimu la awali kwa ajili ya umoja katika ndoa na familia, katika makundi ya uanafunzi, katika makanisa na huduma mbalimbali.

Paulo huzungumzia umuhimu wa jumla wa tunda moja, ambalo ni kujifunua kwa asili ya Mungu kwetu. Katika Waefeso 3:17, tunasoma: *“Kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani; kwamba ninyi ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo”* (KJV; msisitizo umeongezwa) Tunda analozungumzia ni upendo. Katika Kiyunani huitwa agape. Upendo huu ni asili ya Mungu. Ni upendo usio na ubinafsi ambao hutafuta yaliyo mema kwa ajili ya Mungu na mwanadamu. Eva von Tiele-Winckler anaelezea tunda la upendo wa Mungu kama ifuatavyo:

- ▶ Furaha ni upendo wa kufurahia.
- ▶ Amani ni upendo wa utulivu.
- ▶ Uvumilivu ni upendo utegemezao.
- ▶ Upole ni upendo angavu.
- ▶ Wema ni upendo wa kusaidia.
- ▶ Imani ni upendo wa kutumaini.
- ▶ Unyenyekevu ni upendo wa kutojihami.
- ▶ Utauwa ni upendo safi.

Nadhani ni dhahiri kwamba tunda la sifa hizi zitokanazo na Roho ni upendo. Hii ndiyo sababu huzungumzia tunda katika hali ya umoja na wala siyo katika wingi. Ellen White anasema kuhusu sifa hizi: “Badiliko la tabia ni ushuhuda kwa ulimwengu juu ya Kristo akaaye ndani yetu.”[136]

---

136 Ellen G. White, Prophets and Kings, uk. 233.

2. **Karama za Roho.** Matokeo mengine muhimu ya maisha ya Yesu ndani yetu ni kupokea karama za Roho. Mungu ametupatia talanta mbalimbali. Katika 1 Wakorintho 12, Paulo analinganisha kanisa, yaani idadi mahususi ya watu, na mwili wa mwanadamu. Mwili umeundwa kwa ogani nyingi/viungo vingi tofauti. Ni muhimu kwa uhai na afya kwamba kila ogani itende/kiungo kitende kazi vizuri. Hii huonesha kwamba ni wajibu wetu kuhudumiana kwa kutumia talanta zetu mbalimbali na kwa njia hiyo kuchangia katika mafanikio ya jumla ya familia, kundi, kanisa. Kila mmoja amepangiwa kazi tofauti. Mungu ametupatia uwezo mbalimbali.

Orodha ya karama katika Agano Jipya siyo timilifu. Zilikuwepo karama zingine nyingi katika kanisa la awali; na katika zama zetu za sasa, zipo karama za ziada.

| Karama za maneno | Karama za miujiza | Karama za huduma |
|---|---|---|
| Maneno ya hekima<br>*1 Kor. 12:8* | Imani ya kimuujiza<br>*1 Kor. 12:9* | Karama ya uongozi<br>*Rum. 12:8; 1 Kor. 12:28* |
| Maneno ya maarifa<br>1 Kor. 12:8 | Karama za uponyaji<br>1 Kor. 12:9, 28 | Huduma za jumla<br>Rum. 12:7 |
| Maneno ya kinabii<br>*1 Kor. 12:10, 28; Rum. 12:7* | Lugha (usemi)<br>*1 Kor. 12:10, 28* | Karama ya kusaidia<br>*1 Kor. 12:28* |
| Karama ya ufundishaji<br>*1 Kor. 12:28; Rum. 12:7;Efe. 4:11* | Ufasiri wa lugha<br>*1 Kor. 12:10, 30* | Karama ya utoaji<br>*Rum. 12:8* |
| Karama ya uinjilisti<br>*Efe. 4:11* | Roho mbalimbali<br>*1 Kor. 12:10* | Karama ya rehema<br>*Rum. 12:8* |
| Karama ya mitume<br>*1 Kor. 12:28; Efe. 4:11* | Nguvu za kimuujiza<br>*1 Kor. 12:10, 28* | Karama ya ukarimu<br>*1 Pet. 4:9* |
| Karama za mausia<br>*Rum. 12:28* | | Karama za kichungaji<br>*Efe. 4:11* |

Johannes Mager, Auf den Spuren des Heiligen Geistes (Lüneburg: Advent-Verlag, 1999), S. 121.

Ni muhimu sana kwamba vipengele hivi viwili—tunda la Roho na karama za Roho—vidhihirishwe katika asili yetu na

kupitia mazungumzo yetu, hisia, mawazo, na matendo. Kuna njia moja tu ambayo kwayo hili linaweza kutokea. Tunapaswa kujazwa Roho Mtakatifu.

Nyanja mbili muhimu za kuwa na maisha katika Roho Mtakatifu ni kuomba kila siku kwa ajili ya kujitoa kikamilifu kwa Mungu na kuomba imani ya kujazwa Roho Mtakatifu. Mfano wa ombi la namna hiyo unaweza kupatikana katika kijitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi, sura ya 4.* Wasomaji wameniambia uzoefu unaoonesha matokeo ya aina hii ya maombi. Hii inatoka Rheinland, Ujerumani: "Tumeweza kupata uzoefu wa kushangaza. Ndugu na kaka wengi wanaomba kwa kufuata mfano wa sala [kutoka *Hatua za Uamsho Binafsi*] pamoja kila siku, nami nimekuwa nikiomba hivyo pamoja na rafiki kwa muda wa miezi mitano. Siyo tu kwamba mambo yanaboreka kwetu binafsi, lakini pia nyumba zetu, mahusiano yetu, ndoa, katika maeneo ya kiroho, makanisani, lakini siyo katika namna inayoleta migogoro mikubwa. Badala yake, hutokea kwa namna tulivu na kawaida. Tunastaajabishwa na kuona ndani yake mchakato wa Mungu wa kusafisha, ambao huyafanya maisha yawe rahisi zaidi kwa namna fulani, kwa vile tunahisi uwepo wa Mungu zaidi na zaidi."

Je unaona jinsi ambavyo ushuhuda huu unaonesha kwamba "Kristo ndani yetu" kupitia Roho Mtakatifu huleta matokeo chanya katika upamoja wetu?

Taarifa hiyo inaendelea: "Hivi karibuni dada mmoja aliniambia: 'Hivi ndivyo ambavyo daima nimefikiria kuishi maisha mema na yampendezayo Mungu, lakini wakati wote kulikuwa na matatizo mengi njiani. Hatimaye, ndoto yangu imekuwa halisi. Na huu ni mwanzo tu!'"[137] Dada huyu alipata imani inayovutia.

3. **Kumshuhudia Yesu.** *"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* (Matendo 1:8) Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa watapewa nguvu na Roho Mtakatifu kuwa mashahidi Wake.

137 Baruapepe iliyotumwa kwa H. Haubeil mnamo Desemba 18, 2012.

Tunapokuwa tumejazwa Roho Mtakatifu, tutapitia uzoefu wa uamsho na matengenezo ya kiroho. ***Uamsho ni nini?*** Dennis Smith anaelezea: “Ni wakati ambapo maisha ya Mkristo yanafanywa upya katika Yesu. Furaha kuhusu wokovu huujaza moyo wake; shauku kwa ajili ya wokovu wa wengine huanza kumchoma ndani yake. Hii humaanisha kwamba kama Wakristo walioamshwa kiroho tunakuwa na shauku kwa ajili ya wokovu wa watu wengine.”[138]

Ellen White anasema: “Bila uwepo wa Roho wa Mungu, hakuna moyo utakaoguswa, hakuna mdhambi atakayeongolewa kuja kwa Kristo. Wanafunzi Wake wanapoungana na Kristo, pale karama za Roho zinapokuwa zao, hata maskini zaidi na wasiojua zaidi miongoni mwao watakuwa na nguvu itakayogusa mioyo. Mungu huwafanya kuwa mifereji kwa ajili ya utendaji wa mvuto wa juu zaidi ulimwenguni.”[139]

Mwinjilisti afahamikaye sana na pia mhubiri wa uamsho R. A. Torrey anasimulia uzoefuwa kustaajabisha. Mwanamama msaidizi mahiri sana alizungumza na bwana mmoja kuhusu wokovu wake kwa saa mbili lakini hakufanikisha lolote. Hivyo alimwomba Torrey azungumze naye. Baada ya dakika kumi bwana huyo akafanya uamuzi chanya. Mwanamama huyo akawa kimya, kwa vile Torrey alikuwa ametumia maandiko yaleyale ya Biblia aliyokuwa ametumia. Torrey akatoa maoni yafuatayo: “Kwa vile mwanamama huyo hakuwa amefanikisha lolote, yeye naye [Dkt. Torrey] alihofu kwamba hilo lingemtokea pia. Hivyo alimwomba Mungu katika hali yake ya kukosa msaada ili Roho Mtakatifu aifanye kazi hii—Naye Roho alifanya hivyo.”[140]

### Uamsho huleta utume

“Hadi wampokee Roho Mtakatifu, vinginevyo hawawezi kuwasilisha ujumbe huu kwa nguvu. Hadi wampokee Roho

138 Dennis Smith, 40 Days: Prayers and Devotions to Revive Your Experience With God, book 2, Siku ya 6; uk. 24.
139 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, Oktoba 25; uk. 307.
140 R. A. Torrey, Der Heilige Geist (Frankfurt/Main: 1966), S. 37, 38; dondoo fupi.

Mtakatifu, vinginevyo hawawezi kutambua kile ambacho Mungu anaweza kutenda kupitia kwao."[141]

Mungu amepanga kwamba watu watavutiwa na mwenendo wetu binafsi na umoja wetu wa upendo. Hii ni sahihi hasa kwa watoto wetu, vijana, na wanafamilia, lakini pia jamaa zetu, watu tunaofahamiana nao, majirani, watendakazi wenzetu, marafiki, wageni tunaokutana nao. Watu huwa na mwitikio kwa imani yetu, na Mungu anaweza kuwaongoza waje kwetu.

Maneno yafuatayo hutuonesha ushawishi mbaya unaoweza kusababishwa na mwenendo wetu: "Kama tungejinyenyekesha mbele ya Mungu, na kuwa wema na waungwana na wenye huruma na wasikitivu, wangekuwepo waongofu mia wanaopokea ukweli mahali ambapo sasa yupo mmoja tu."[142]

Lakini Roho Mtakatifu ni lazima awepo katika hili. Ellen White anaelekeza usikivu wa wachungaji katika yafuatayo: "[Washiriki wa kanisa] hawawezi kuwasilisha kweli kuu na tukufu za Neno Takatifu la Mungu ambazo zingesadikisha na kuongoa nafsi kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu. Nguvu ya Mungu hungojea kudai na kupokea kwao."[143]

### Jinsi gani uamsho wa kiroho hudumishwa?

Mnamo mwaka 1893, uamsho ulifanyika kwenye taasisi za Kiadventista huko Battle Creek, Michigan, lakini taratibu uamsho huo ukatoweka. Mungu alimpatia Ellen White dokezo kuhusu chanzo. Alisema: "Kama nafsi hizo zote nyingi, zilizoangaziwa wakati huo zingeenda kufanya kazi mara moja ili kuwapatia wengine kile ambacho alikuwa amewapatia kwa kusudi hilo hasa, nuru nyingi zaidi ingekuwa imewasilishwa, nguvu kubwa ingekuwa imekirimiwa."[144]

Tunapokea nuru zaidi na nguvu zaidi kwa kueneza injili. Tunapowahudumia watu wengine, basi huwa na matokeo yenye thamani maishani mwetu sisi wenyewe. Hii ndiyo

141 Ellen G. White, Ye Shall Receive Power, Oktoba 4; uk. 286.
142 Ellen G. White, Testimonies for the Church (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), 9:189.
143 Ellen G. White, Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 175.
144 Ellen G. White, Selected Messages, book 1; uk. 129.

sababu ni muhimu sana kuwahimiza watu kuwaombea wale ambao hawajafikiwa na injili katika kipindi cha siku 40 za ibada.[145]

### Wapi ambapo utume wetu unapaswa kuanzia?

Yesu aliwaambia wanafunzi Wake mahali ambapo wangepaswa kuanzia utume wao: wangepaswa kuanzia mahali walipokuwa. Kwetu sisi, hii humaanisha tunapaswa kuanzia nyumbani na mahali watu wanapotufahamu. Kwa nini Yesu alipanga namna hii? Mahali ambapo watu wanatujua, ushuhuda wetu utakubalika kama utaambatana na mwenendo husika wa upendo. Ushuhuda wa maisha yetu hauna budi kuendana na ushuhuda wa kinywa chetu. Inaweza kuonekana nyumbani endapo kweli tumejazwa Roho Mtakatifu.

### Amri mpya ya Yesu ina umuhimu gani?

Yesu anasema katika Yohana 13:34, 35: *"Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."*

Maisha yaliyojazwa Roho husababisha tunda lingine muhimu la Roho Mtakatifu: unyenyekevu. Unyenyekevu ni mtazamo wa Yesu na pia ni muhimu sana kwa ajili ya umoja uthabiti. Hii ndiyo sababu kwa nini Yesu aliwapatia wanafunzi Wake amri mpya mara tu baada ya kuwatawadha miguu. Kuwatawadha miguu ilikuwa ishara ya unyenyekevu.

Unyenyekevu siyo sifa ya mtu wa asili. Hata hivyo, tunaweza kumwomba Mungu kila siku atujalie unyenyekevu kwa kudai ahadi kama vile Mika 6:8.

Unyenyekevu ni sifa muhimu sana kwa ajili ya mtu aliyejazwa Roho, lakini kwa kawaida hukadiriwa vibaya kabisa. Katika amri hii mpya, Yesu anazungumzia kuhusu kupendana "kama vile nilivyowapenda ninyi." Yesu anatupenda kwa upendo wa kiungu. Tunaita aina hii ya upendo agape, neno la Kiyunani

145 Angalia Dennis Smith, 40 Days, kitabu cha 1 na 2, Utangulizi.

lenye maana ya upendo wa kiungu. Tunaweza kuwa na upendo huu pale tu tunapokuwa tumejazwa Roho Mtakatifu. Paulo aliandika, "*…pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*" (Rum. 5:5) "Upendo mkuu kwa ajili ya Mungu na upendo usio na ubinafsi kwa ajili yetu sisi kwa sisi—hii ni karama bora ambayo Baba yetu wa mbinguni anaweza kutujalia. Upendo huu siyo hisia, bali kanuni ya kiungu, nguvu ya kudumu. Moyo usiojitoa wakfu hauwezi kuuvumbua wala kuuzalisha. Ni katika moyo ule tu atawalao Yesu ndimo huweza kupatikana."[146]

Kwa hiyo uwepo wa unyenyekevu ni suala la ama Yesu yuko kwenye "enzi" ya moyo wetu. Je tunamruhusu aongoze kila kitu maishani mwetu? Je tumesalimisha kikamilifu maisha yetu Kwake? Hivi tunathibitisha hili kila siku?

## Habari gani kuhusu mimi?

Je nina imani inayovutia? Hivi Yesu anakaa moyoni mwangu kupitia Roho Mtakatifu? Ikiwa ndivyo, basi napaswa kujitunza na kukua katika imani hii inayovutia. Lakini kama nikitambua kwamba ningali sina imani inayovutia, basi bila shaka napaswa kukabili suala hili muhimu.

Zipo nyenzo zenye msaada katika kutafuta imani hii inayovutia (kwa wale wasio nayo bado) na kwa ajili ya kutunza imani hii (kwa wale wenye nayo tayari) katika kitabu changu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi na katika kitabu alichoandika Dennis Smith kiitwacho *40 Days – Devotionals and Prayers in Preparation of the Second Coming of the Lord.* Vitabu hivi viwili hukamilishana vyenyewe katika namna ya thamani sana. Naweza tu kupendekeza kwa moyo wangu wote kwamba usome vitabu hivi—naam, hata zaidi ya mara moja.

## Jinsi gani hali yetu binafsi ya kukosa Roho Mtakatifu ina athari kwa watu wengine?

Bila Yesu ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, sisi ni kama Wakristo wa mwilini (angalia 1 Kor. 3:1–3; Rum. 8:1–17; Gal

---

146 Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 551.

5:16ff). Hatuokolewi tukiwa katika hali hii (Rum. 8:9). Tunaishi kwa uwezo na nguvu zetu za kibinadamu. Matokeo yake ni kwamba familia na watoto wetu bila shaka nao pia watakuwa Wakristo wa mwilini, pamoja na athari zote za kujutia.[147] Hebu tuzingatie kwamba upendo wa Mungu unaweza tu kuwa mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu. Ellen White anasema, “Wale ambao kamwe hawajapata uzoefu wa kuwa na upendo wa dhati wa Kristo uongoao hawawezi kuwaongoza wengine kwenda kwenye chemchemi ya uzima. Upendo Wake moyoni ni nguvu inayohimiza, ambayo huwaongoza wanadamu wamdhihirishe Yeye katika mazungumzo, katika roho ya huruma na usikitivu, katika kuinua maisha ya watu wale wanaochangamana nao.”[148]

Yesu anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, basi atatuwezesha kumshuhudia Mungu katika namna ya asili kabisa. “Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake.” (Mat 12:34)

### Imani inayovutia ni ya thamani kiasi gani?

Tunaweza kuona jinsi imani hii inayovutia ilivyo na thamani tunapowaangalia Wakristo waliokumbwa na shida , mateso, kupoteza mali, au kufia imani badala ya kuikana imani hii. Nini kilichowafanya wawe wastahimilivu kiasi hicho katika matatizo haya makali? Ilhali tunaona uthibitisho kwamba walikuwa wamejawa Roho Mtakatifu, wafia-imani hawawezi kutuambia jinsi walivyojisikia katika maumivu yao ya mauti. Hata hivyo, taarifa za kipapa kuhusu kifo cha Hus na Jerome wakati wa kuchomwa moto huko Constance hutupatia kidokezo muhimu. Mtu fulani anapoungua, anaweza tu kupiga kelele. Lakini watu hawa wawili waliimba nyimbo za sifa. Jambo kama hilo linawezekana tu kwa msaada wa Mungu. Walikuwa na furaha kamili licha ya maumivu yao. “Mahali popote atawalapo Roho, hapo amani hukaa. Na hapo itakuwepo furaha pia.”[149]

---

147 Angalia Helmut Haubeil, Hatua za Uamsho Binafsi, uk. 36, 74, 76.

148 Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 550, 551.

149 Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 153.

Familia ya Waginoti ya Durant huko Ufaransa katika karne ya kumi na nane ni mfano wa kuvutia sana. Akina Durant waliteswa na kanisa kwa sababu ya imani yao ya Biblia. Baba alikaa gerezani miaka kumi na nne kabla ya kusamehewa. Mama alifia gerezani. Pierre mwanawe—mhubiri shupavu—aliteswa. Marie binti yao alishikiliwa mateka kwenye mnara pamoja na wanawake wengine. Angekuwa ameachiliwa kama angeikana imani yake, lakini hakufanya hivyo. Mnamo mwaka 1768, aliachiliwa huru baada ya miaka thelathini na nane ya kifungo. Kwa Marie Durant, imani ya Biblia ilikuwa imani inayovutia ambayo asingeweza kuikana.[150]

### Mifano ya matokeo makuu ya kimishenari

Danieli na marafiki zake walikuwa radhi kukubali mateso walipoomba mlo tofauti. Na Mungu alifanya nini? Alibariki utii wao. Walikuwa na sura zenye mvuto zaidi, walikuwa na afya bora, na wenye maarifa zaidi kuliko wengine. Walitunukiwa nyadhifa za juu. Tunajua taarifa kuhusu marafiki wa Danieli katika tanuru la moto na kuhusu usiku wa Danieli akiwa kwenye tundu la simba. Imani yao ilikuwa muhimu zaidi kwao kuliko maisha yao. Na matokeo yalikuwa yapi? Falme mbili za ulimwengu ziliweza kusikia ushuhuda wao katika maneno na matendo kuhusu Mungu wa kweli. Kielelezo chao kilikuwa na matokeo makubwa katika kazi ya utume.

Ndivyo ilivyokuwa pia kwa Yusufu huko Misri. Alikataa kufanya zinaa. Kwa sababu ya kashfa ya mkewe Potifa, alipelekwa gerezani. Lakini Mungu alitumia uaminifu wake ili kuujulisha ulimwengu wote utambue kuhusu Mungu wa kweli.

Je unamkumbuka binti mdogo aliyekuwa akifanya kazi kama mtumwa katika nyumba ya Naamani? Ushuhuda wake katika maneno na matendo hatimaye ulipelekea katika uongofu wa jemedari huyu. Nashawishika kwamba siyo tu kwamba alimfuata Mungu aliye hai kwa furaha kuu, lakini pia alimpatia binti huyu mdogo uhuru wake naye akaondoka kwenda kwao, pamoja na zawadi nyingi.

---

150 Imechukuliwa kutoka Wikipedia, “Marie Durant.”

Katika Mathayo 13:44–46, Yesu anasimulia juu ya mtu aliyepata hazina kondeni. Hazina hii ilikuwa ya thamani sana kwake kiasi kwamba aliuza kila kitu alichomiliki halafu akanunua shamba hilo. Aliacha kila kitu kwa ajili ya ufalme wa mbinguni—au kama ambavyo nimeelezea, imani inayovutia. Je tunaweza kuona namna imani hii ilivyo ya thamani?

## Dondoo za Mwisho

Ellen White anasema, "Wale wakaao katika Yesu watakuwa na furaha, uchangamfu, na raha katika Mungu."[151] Tayari imani inayovutia hutupatia maisha yenye raha, ushindi, na furaha pamoja na tumaini lenye msingi imara kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Hata katika nyakati ngumu, hata tungepitia bonde la giza, imani yetu bado itakuwa ya kuvutia kupitia uwepo wa Mungu.

Kupitia imani inayovutia tunaweza kuchangia katika upamoja wenye manufaa, na hivyo maslahi ya watu wengine yataamshwa katika imani yetu.

Hebu Mungu atusaidie ili tuelewe kikamilifu umuhimu mkuu wa umoja! Hebu atusaidie kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, Kristo akiwa ndani yetu, ili tukue na kufanana na Kristo kwa ajili ya furaha na baraka yetu wenyewe na pia kuwavutia wapendwa wetu na wanadamu wenzetu. *"Furaha ya Bwana ni nguvu zenu."* (Neh 8:10) **"Kama tunamwakilisha Kristo, tutaifanya huduma Yake ionekane inayovutia, kama ilivyo hasa."**[152]

151 Ellen G. White, Testimonies for the Church (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), 4:626.

152 Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 116.

**Sala:** "Baba wa mbinguni, nakushukuru kwa moyo wote kwamba kweli kumfuata Yesu kikamilifu huleta maisha yenye msisimko mkubwa zaidi. Tafadhali nisaidie nidumu katika uhusiano wa karibu pamoja na Yesu maisha yangu yote. Pia tumia maisha yangu kuwaongoza wapendwa wangu pamoja na watu wengine waje Kwake." Amina.

## Mawazo Binafsi na Mwongozo wa Mjadala

1. *Nini matokeo ya Kristo kuishi ndani yetu?*

   ___

2. *Yapi ni matunda ya Roho?*

   ___

3. *Zipi ni karama za Roho?*

   ___

4. *Je uamsho una matokeo gani katika maisha yetu binafsi? Jinsi gani huathiri mazingira yetu? Jinsi gani hutuhamasisha?*

   ___

5. *Ni mifano ipi ya Biblia tuliyo nayo ioneshayo, kupitia tumaini rahisi katika Mungu, kwamba mambo makubwa yanaweza kutokea?*

   ___

## Muda Wetu wa Maombi

- *Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.*
- *Omba pamoja na mwanamaombi mwenzio:*

   1. *Kwamba tunda la Roho liendelee daima kustawi.*
   2. *Kwa ajili ya uwezo wa kutambua karama za Roho na kuzitumia kisahihi.*
   3. *Kwa ajili ya ujasiri na furaha ya kuwa shuhuda wa Kristo aishiye ndani yako—kupitia maisha yako, kupitia maneno na matendo yako, ambayo hayafanyiki kwa nguvu zako mwenyewe, bali hutokana na imani inayovutia.*
   4. *Kwa ajili ya furaha katika kulisoma Neno la Mungu, na kwa ajili ya utulivu wa akili na hekima.*

## USHUHUDA

Shajara ya mabadiliko baada ya kujitoaMwanzoni mwa 2014, nilidumu kujiuliza, “Je siku moja Yesu ataniambia: ‘Sikujui wewe’? Hivi mimi ni mmojawapo wa wanawali wapumbavu?” Wazo juu ya hili halikuvumilika kwa vile nilitaka kupokea uzima wa milele kutoka kwa Mungu, lakini sababu ya mambo kadhaa maishani mwangu, daima nilikuwa na dhamiri ya hatia na wakati wote sikuwa kwenye njia sahihi.

Bahati njema, nilipata vitabu viwili, Hatua za Uamsho Binafsi na Kaeni Ndani ya Yesu. Baada ya kuvisoma mara ya kwanza, nilitambua kwamba kitu fulani kilipaswa kubadilika maishani mwangu. Nilisoma vitabu hivyo mara kadhaa ili kuelewa hasa kila kitu. Pamoja na hayo, nilisikia ushuhuda kutoka kwa dada mcha-Mungu aliyekuwa Mkristo wa kiroho miezi michache tu kabla ya hapo.

Sasa najua kwa hakika kwamba mwanzoni mwa mwaka nilikuwa mtu wa “mwilini” katika fikra zangu, na kama ningekufa, Yesu angeweza kuniambia, “Sikujui wewe.”

Kupitia kujitoa kikamilifu kwa Yesu, Mungu aliweza kubadilisha maisha yangu kabisa kwa mwezi mmoja tu.

Sasa naamka saa 10:30 alfajiri ili kujifunza Neno la Mungu. Kwa nguvu zangu mwenyewe, hili lisingefikirika—usingizi ulikuwa muhimu zaidi. Naomba kwa namna tofauti kama mtu aliyejazwa Roho. Namwomba Bwana kila siku kile anachotaka nifanye siku hiyo. Na Mungu anajibu. Kila siku namwalika Roho Mtakatifu aishi na kutenda kazi ndani ya moyo wangu. Nina mawazo makini zaidi na ninavaa kwa namna ya staha zaidi kama impasavyo mwanamke.

Aidha, sili kila wakati tena. Hilo lisingewezekana kwangu kwa nguvu zangu mwenyewe. Naweza kutimiza mahitaji ya kila siku kwa amani zaidi, na wala msongo haufanyi tumbo langu lijisokote tena. Mume wangu naye alitambua mabadiliko ndani yangu baada ya majuma matatu. Alisema, “Huna tena ulimi wa upanga kama ule.”

Wakati wa kujifunza Biblia, ghafla huwa napata maswali mengi sana ambayo sijawahi kuyapata hapo kabla. Sasa

nataka kuchimba kwa kina zaidi. Hapo awali, Roho Mtakatifu alikuwa ameniongoza mara chache tu kuwasilisha ushuhuda. Sasa inatokea kila siku. Sihitaji kuandaa hotuba. Mungu hunipatia maneno sahihi sababu Yeye pekee ndiye anamjua mtu ninayezungumza naye. Japo wakati fulani natenda dhambi, Mungu hunipatia utambuzi bayana kuona dhambi husika. Naweza kutubu na kubadili njia zangu.

Nimefikia hatua ya kutambua kuwa siwezi kufanya lolote bila Yesu na kwamba nahitaji uwepo wa Kristo kila hatua njiani. Vilevile nimetambua kwamba kinyume cha kiburi (jinsi nilivyo mwema, namna gani bora niwezavyo kutenda kitu fulani) ni unyenyekevu, jambo ambalo hutuonesha kwamba bila Yesu hatuwezi kabisa kutenda jema.

Pia Mungu alinipatia nguvu ya kuacha kunywa kahawa. Awali, hili lisingefikirika, sababu nilipoacha kunywa kahawa nilikumbwa na maumivu ya kutisha ya kichwa kwa siku tano. Hizi ni dalili kali za madhara/matokeo? ya kuacha kutumia kilevi. Mara hii hata sikufikiria athari ambazo ningepata. Nilijua tu kwamba sikutaka kuendelea tena kufanya hivyo. Leo, sina tena shauku ya kahawa. Nilikuwa na uzoefu huo kuhusiana na nyama. Mimi na familia yangu kamwe hatukupenda kuachana na ulaji wa nyama. Leo ni rahisi kwangu. Sina tena shauku ya kuila. Hatua ya mabadiliko maishani mwangu ilikuwa shauku kuu ya kupata uzima wa milele na kutambua kwamba hakuna lingine lolote lililo muhimu kuliko Mkombozi wangu, Kristo Yesu, licha ya matokeo.

Ezekieli 36:26, 27 huzungumza kweli: Yesu atatupatia moyo mpya na roho mpya. Anataka kutuumba tuwe watu wanaotunza amri Zake. Kwa miongo mingi, nilikuwa nimekabiliana na matatizo mbalimbali, lakini daima bila mafanikio. Nisingeweza kuyashinda mimi binafsi. Yesu alitaka kutimiza mapenzi Yake ndani yangu, na alihitaji tu utayari wangu.

Ellen White anasema kwamba yeyote anayejaribu kuifikia mbingu kwa matendo yake mwenyewe kwa kushika sheria, anathubutu kisichowezekana. Hili ndilo hasa nililopitia kwa miaka thelathini na tano. Kiakili nilikubaliana na amri hizi, lakini sikuweza kuzishika. Yesu pekee ndiye anaweza kutimiza

jema hilo ndani yangu. Anatupatia shauku ya kuyapenda mambo mema na yaliyo bora, Naye huondoa shauku yetu ya kutamani mambo mabaya.

Leo naweza kuthibitisha Warumi 8:14: *“Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.”* Kwa mujibu wa aya hii, nimeomba kila siku, kila saa, daima kwa ajili ya Roho Mtakatifu aishi na kutenda kazi ndani yangu—sababu Ibilisi halali usingizi.

Yesu alisema katika Mathayo 10:37: *“Apendaye baba au mama kuliko Mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko Mimi, hanistahili.”* Daima nilikuwa nimewaza: hilo haliwezekani tu. Sasa najua kwamba Yesu anapoishi ndani ya moyo wangu, ndipo Mungu mkuu wa ulimwengu wote hutenda kazi ndani yangu na kupitia kwangu halafu pia huwatunza watoto na familia yangu kwa namna bora kuliko ambavyo ningewahi kufanya. Ni Mungu pekee mwenye uwezo wote na mwenye maarifa yote. Kwa imani naweza kuweka maisha yangu mikononi Mwake kila siku, Naye atatenda kila kitu kwa usahihi, kadiri ya hekima Yake na mpango Wake. M. M.

# Kiambatisho

### Mapendekezo kwa ajili ya kujifunza zaidi

Pendekezo muhimu: Tafadhali soma kitabu hiki mara kadhaa. Utafiti wa elimu umeonesha kwamba ni muhimu kusoma au kusikiliza mada kwa ajili ya maisha yetu mara sita hadi kumi ndipo tutaielewa vilivyo. Jaribu hilo. Matokeo yatakushawishi. Niliposoma kwa kurudia mara kadhaa kitabu fulani, nilipata kwa mara ya kwanza maishani mwangu utimizwaji wa Roho Mtakatifu. Nimepokea shuhuda nyingi za shukrani na hamasa kuhusu kukua katika maisha yaliyojawa Roho pamoja na Yesu. Takriban wote walikuwa ni wasomaji waliorudia tena kwa kina kitabu hiki mara kadhaa.

### Uzoefu mpya katika maisha yaliyojawa Roho

Bwana wetu Yesu mpendwa alisema, "Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho [Mtakatifu]." (Yohana 7:38, 39)

**Nina ombi kwako:** Unapokuwa na uzoefu kupitia kujitoa kwako kwa Yesu na kuishi katika Roho Mtakatifu, basi nitashukuru sana endapo ungenitumia taarifa fupi, mimi Helmut Haubeil. Ni jambo la thamani sana kama tunaweza kusimulia uzoefu mbalimbali katika *www.steps-to-personal-revival.info* – shuhuda, katika makala, magazeti. Kama kanuni, huwa tunataja tu herufi za majina. Tafadhali kumbuka kwamba uzoefu wako utawaimarisha wengine ili waanze au waendelee kukua katika mwenendo uliojawa Roho kwa kujiadhimisha kwa Yesu Kristo, Mwokozi wetu wa pekee na ajaye hivi karibuni.

## *MAONI*

Hivi sasa nachunga makanisa mawili huko California. Mara ya kwanza nilipata masomo yako kwa kumsikiliza Mchungaji Dwight Nelson [angalia hapa chini] kwenye podikasti kila juma. Hii iligusa kabisa nafsi yangu mwanzoni. Nilikuwa nimesikia kuhusu masomo mengine juu ya Roho Mtakatifu hapo kabla, lakini nakiri kwamba kamwe sikuweza kujali sana. Naamini hakika kwamba kwa namna fulani, Mungu amechagua wakati huu wa sasa ili kuwafikia watu wengine zaidi kupitia Roho Mtakatifu. Nami nafurahi sana nimekipata kutokana na juhudi zako.

Jambo moja ninaweza kushuhudia kwako. Kwenye sura ya kwanza tu tunafunuliwa kwa namna rahisi kweli madhubuti sana ambazo hushurutisha akili zetu zitulie na kufikiri upya. Na mchakato wa kusoma mara nyingi una ufanisi mkubwa. Kwa kila mtu ninayezungumza naye, na kujadiliana naye na kumhubiria kuhusu kitabu hiki, mada ya Roho Mtakatifu hujirudia kuwa na mvuto zaidi na zaidi. Ni kana kwamba tunaisikia mara ya kwanza. Naweza kuliona hilo mimi binafsi. Nisingeweza kuhama sura ya kwanza kabla ya kuhubiri angalau mahubiri 3 kuhusu mada iliyojadiliwa hamo. Sijui tu namna ya kulielezea hilo, lakini sikuweza kuacha kusoma kitabu hiki, na matokeo yalitambulika kwenye makanisa yangu. Nilipaza sauti na mwaka huu uliopita, mtaa wangu umeonesha ukuaji maridhawa. Hayo yote ni sababu ya Mungu na uwezeshaji wa Roho Mtakatifu katika viungo vyetu. Nasi tunatarajia mengi zaidi yatokee katika mwaka huu mpya! D.R. Jan. 2018 Nukuu

***Mchungaji Dwight Nelson,*** Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kumbukumbu ya Waasisi – Chuo Kikuu cha Andrews, alisema kwamba kitabu hiki [Hatua za Uamsho Binafsi] "kilibadilisha utu wangu wa ndani. Nataka kikufanyie vivyo hivyo."

Alihutubu mfululizo wa mahubiri matatu:

***"Eneo na Matengenezo Mapya: Jinsi gani ya kubatizwa kwa Roho Mtakatifu?"***

Alinukuu kutoka "Hatua za Uamsho Binafsi" halafu akakipendekeza. Hiyo ilisababisha maelfu ya upakuaji na uagiziaji wa vitabu husika.

# *Kaeni Ndani ya Kristo*
# Yesu Kristo

Injili ya Yahana Sura 15:

**Fungu la 4-5** "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. . . akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana."

**Fungu la 7** "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

**Fungu la 11** "Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe."

**Kitabu hiki kinataka kukuonesha njisi unavyoweza kujenga au kuwa na uhusiano binafsi na Yesu Kristo. Ni jambo la pekee sana kumwamini Yesu.**

***Mimi nalikuja ili wawe na uzima,***
***kisha wawe nao tele.***
***Yohana 10:10***

**ISBN 978-9987-726-22-6**

Kibidula